# WAMACHINGA
*NA*
# HAKI-JIJI NCHINI TANZANIA






**Kimehaririwa na**
**SABATHO NYAMSENDA**

# WAMACHINGA NA HAKI-JIJI NCHINI TANZANIA

Kimehaririwa na Sabatho Nyamsenda

Dar es Salaam
2023

Kitabu hiki kimechapishwa na mradi wa Sauti za Mashinani chini ya ufadhili wa:

Rosa Luxemburg Foundation - East Africa
S.L.P. 105527
Dar es Salaam, Tanzania

ISBN: 978-9912-41-234-7

Usanifu wa Jalada na Kurasa: Rogers Mahanyu

Maudhui ya kitabu hiki ni msimamo binafsi wa waandishi na siyo lazima yaakisi mtazamo wa Rosa Luxemburg Foundation - East Africa.

Mchapishaji wa kitabu hiki anatoa ruhusa kwa mtu au taasisi yoyote kurudufisha, kunukuu na kuchapisha kitabu hiki kwa matumizi ya kielimu.

# YALIYOMO

Shukrani iv

Orodha ya Waandishi vi

Utangulizi wa Mhariri: 1
**Vuguvugu la Haki-Jiji Litafanikiwa**
*Sabatho Nyamsenda*

Sura ya 1: 33
**Mfumo wa Ubepari na Athari Zake kwa Afrika**
*Sabatho Nyamsenda & Abunuwasi L. Mwami*

Sura ya 2: 55
**Wamachinga Ndani ya Mfumo wa Ubepari**
*Sabatho Nyamsenda & Abunuwasi L. Mwami*

Sura ya 3: 85
**Mipango Miji na Wamachinga**
*Joseph Chiombola*

Sura ya 4: 109
**Dhana na Misingi ya Haki-Jiji**
*Sabatho Nyamsenda*

Sura ya 5: 143
**Uzoefu wa Wamachinga wa India na Afrika Kusini**
*Michaela Collord*

Sura ya 6: 151
**Kuelekea Ushirika Mpya wa Wavujajasho**
*Christina Mfanga*

# SHUKRANI

Japokuwa sura za kitabu hiki zimebeba majina ya waandishi, ukweli ni kwamba kitabu hiki ni zao la kazi ya pamoja ya uzalishaji maarifa katika jamii. Msingi mkuu wa kitabu hiki ni maarifa yaliyozalishwa na wavujajasho wenyewe kutokana na uzoefu wao katika ushalishaji na mapambano yao dhidi ya ukandamizaji. Pia, zipo kazi nyingi za kitaaluma kama makala za kitaaluma, vitabu, ripoti, chambuzi na taarifa za vyombo vya habari na nyinginezo ambazo zimetumika katika ujenzi wa kitabu hiki.

Tulipata wazo la kuandika kitabu hiki kutokana na semina zilizoendeshwa na mradi wa Sauti za Mashinani uliofadhiliwa na Rosa Luxemburg Foundation - East Africa kuanzia mwaka 2020 hadi 2022. Semina hizo, zilizolenga kuwaleta pamoja wavujajasho wa kada mbalimbali kwa ajili ya kubadilishana uzoefu kuhusu maisha na mapambano, zimezaa vitabu viwili. Kitabu cha kwanza ni *Jamhuri ya Wamachinga* ambacho bado hakijachapishwa na cha pili ni hiki. *Jamhuri ya Wamachinga* ni mkusanyiko wa masimulizi ya wavujajasho wanaofanya kazi zisizo rasmi (*informal labour*). Kitabu hiki, *Wamachinga na Haki-Jiji Nchini Tanzania*, ni nyongeza kidogo ya wasomi juu ya maarifa ya msingi ya wavujajasho yaliyomo katika *Jamhuri ya Wamachinga*. Kwa hiyo basi, tunatoa shukrani za dhati kwa Rosa Luxemburg Foundation - East Africa kwa kugharamia uchapishaji wa kitabu hiki. Shukrani zetu pia zifike kwa taasisi zifuatazo: Hakiardhi,

Ushirika wa Wanawake Wavujajasho wa Manzese (UWAWAMA), Shirikisho la Umoja wa Wamachinga Tanzania (SHIUMA) pamoja na Kariakoo Wamachinga Association (KAWASSO).

Kwa namna ya pekee kabisa, tunamshukuru Dorothee Braun, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Rosa Luxemburg Foundation - East Africa, kwa mchango wake wa mawazo na utayari wa kufanya kazi nasi ili kuandaa kitabu hiki. Tunawashukuru pia Zuhura Mtenguzi na Daudi Edward kwa kusaidia kusahihisha makosa ya chapa kwenye muswada wa kitabu hiki, na Consalva Mahengo kwa kuratibu mradi wa Sauti za Mashinani.

Wapo wengine wengi waliochangia kwa namna moja ama nyingine katika mchakato wa uandaaji wa kitabu hiki ambao majina yao hayajatajwa hapa kutokana na ufinyu wa nafasi. Tunawashukuru sana.

## Orodha ya Waandishi

**Abunuwasi L. Mwami** ni mhadhiri mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania kilichopo jijini Mwanza. Amewahi kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa zaidi ya miongo miwili kabla ya kustaafu mwaka 2013.

**Christina Mfanga** ni wakili wa kujitegemea na mwanachama wa Ushirika wa Wanawake Wavujajasho Manzese (UWAWAMA).

**Joseph Chiombola** ni afisa programu mwandamizi katika Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI) na wakili wa kujitegemea.

**Michaela Collord** ni mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nottingham nchini Uingereza.

**Sabatho Nyamsenda** ni mhadhiri msaidizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma.

# Vuguvugu la Haki-Jiji Litafanikiwa

SABATHO NYAMSENDA

Ungemuona kijana Kulwa Makasi kwa mbali ungeweza kudhani ni kijana mwenye furaha. Hujitahidi kumkaribisha mteja kwa bashasha japokuwa, tofauti na wenzake, angekuwa amekaa ndani ya kijibanda chake anamouzia viatu. Kijibanda hicho kilikuwa kimepangiliwa vizuri na kwa unadhifu mkubwa, kama vilivyokuwa vijibanda vingine vya wamachinga

katika eneo la Makoroboi jijini Mwanza. Ungeweza kudhani amepumzika tu kwenye kiti akisubiri wateja. Ni hadi pale ambapo ungekikaribia kibanda hicho ndipo ungeona kuwa Makasi alikuwa amekaa juu ya kiti chenye matairi cha walemavu. Na hapo ndipo ungegundua kuwa mmachinga huyo mlemavu ndiye pia mwenye baiskeli ya kunyonga kwa mkono, yenye matairi matatu, iliyoegeshwa nje ya kibanda hicho. Ukianza kuzungumza nae ndipo utaelewa kuwa ni mtu aliyepitia mateso makubwa na kwamba ulemavu wake ni kielelezo cha historia ya uonevu, dhuluma na uporaji wa bidhaa na maeneo ya kufanyia biashara unaofanywa na dola dhidi ya wafanyabiashara wadogo, maarufu kama wamachinga.

Mpaka kufikia Julai 5, 2011, Makasi alikuwa mzima wa afya, akitembea na kukimbia kwa miguu yake. Rafiki yake mmoja waliekuwa wakiishi pamoja anamsimulia kama kijana aliyekuwa na ndoto kubwa, mtanashati na mwenye bidii ya kazi. Julai 6, 2011 ndiyo siku ambayo Makasi alidhulumiwa uzima wa mwili wake na kuachiwa ulemavu wa kudumu. Kosa lake lilikuwa kuzaliwa katika familia maskini, hali iliyomlazimu kwenda jijini Mwanza kwa ajili ya kujitafutia maisha. Kama walivyo vijana wengi, baada ya kuhangaika huku na kule, hakuwa na chaguo zaidi ya kufanya biashara ya uchuuzi wa bidhaa na kuzipanga katika maeneo ya wazi kwa ajili ya kutafuta wateja.

Hata hivyo, kipindi hicho cha awamu ya nne (2005-2015), kilikuwa ni zama za giza kwa wamachinga nchi

nzima. Kama ambavyo imefafanuliwa katika sura ya pili ya kitabu hiki, awamu ya nne ilianza mamlaka yake kwa barua iliyoandikwa na Waziri Mkuu kwa viongozi wa wa mamlaka wa majiji na miji mikubwa nchini ikiwaamuru kuwaondoa wamachinga kutoka maeneo ya katikati ya majiji. Jijini Dar es Salaam pekee inakadiriwa kuwa wamachinga zaidi ya milioni 1 walitimuliwa kwa nguvu, na kusababisha hasara kubwa, ikiwemo majeraha na upotevu wa bidhaa. Timua timua ziliendelea katika kipindi chote cha awamu ya nne na kuzua mapigano kati ya wamachinga, waliokuwa wakipigania haki yao ya kubaki katikati ya jiji, na mgambo waliotumwa kuwaondoa wamachinga kwa nguvu. Mapigano hayo yalipelekea wakati mwingine askari kutoka Jeshi la Polisi kutumwa ili kuongezea nguvu kwa upande wa mgambo.

Hali kama hiyo ndiyo iliyotokea tarehe 6 Julai 2011, siku ambayo Makasi hataisahau maishani mwake. Kama kawaida, asubuhi na mapema, alikwenda eneo la Makoroboi kwa ajili ya kuanza biashara. "Nilipofika mjini," Makasi anasimulia, "nilikuta kuna taharuki ya maaskari na wamachinga. Maaskari walituamuru tuondoe biashara zetu mtaa wa Makoroboi." Yeye na wenzake walikwenda kwenye jengo moja ambalo lilikuwa halijaisha kwa ajili ya kuhamisha bidhaa zao. Wakati huo mabishano yalikuwa yakiendelea kati ya polisi na wamachinga. Polisi walitumia mabomu ya machozi kuwatawanya wamachinga pamoja na watu wengine waliokuja katika eneo hilo. Makasi na

baadhi ya wenzake walianza kukimbia kuelekea eneo la soko kuu kwa ajili ya kuokoa uhai wao. "Tukasikia sauti ikiamrisha, 'Piga risasi!' Ndio wakawa wamepiga risasi moja kwa moja zikawa zinatuelekea sisi." Risasi tatu ziliingia mwilini mwa Makasi - moja kichwani, nyingine mgongoni na nyingine kwenye paja. Makasi alianguka papo hapo na kupoteza fahamu. Alipozinduka alijikuta yupo katika hospitali ya Rufaa ya Bugando, ambako alilazwa kwa muda wa mwezi mmoja.

Madaktari wa Bugando waliokoa uhai wa Makasi lakini hawakuweza kumrejesha katika hali ya uzima. Risasi tatu ziliendelea kubaki mwilini mwake na kumsababishia ulemavu wa kudumu. Baadaye alihamishiwa katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambako alipelekwa na gari la kubebea wagonjwa la hospitali ya Bugando. Makasi, ambaye alisindikizwa na mama yake mzazi, anasema kuwa baada ya kumfikisha Muhimbili, daktari aliyemsindikiza kutoka Bugando alimwambia kuwa kazi yake imekwisha; ilikuwa zamu ya madaktari wa Muhimbili kumtibu. "Wakatutelekeza hapo, mimi nikiwa na mama yangu mzazi. Wao wakarudi Mwanza sisi tukabaki kupambana hapo Muhimbili." Makasi anadai kuwa hata hapo Muhimbili hakupewa matibabu ya maana zaidi ya dawa za maumivu. Madaktari wa Muhimbili walimwambia kuwa alitakiwa kwenda India ili aweze kufanyiwa upasuaji wa kuondoa risasi mwilini. Lakini familia ya Makasi haikuwa na uwezo wa kifedha wa kumpeleka India. Baada ya kukaa

Muhimbili kwa miezi mitatu bila kufanyiwa upasuaji wa aina yoyote, maisha yalizidi kuwa magumu. Licha ya kumsababishia ulemavu, Makasi anadai kuwa "serikali haikulipa hata shilingi moja" kwa ajili ya matibabu yake. Msaada pekee alioupata ni michango ya fedha kutoka kwa wamachinga wenzake. Baadaye alihamia hospitali ya Lugalo kwa ajili ya mazoezi ya viungo huku risasi zikiendelea kubaki mwilini mwake. Maisha yalizidi kuwa magumu jijini Dar es Salaam ambako kila kitu kilihitaji fedha: usafiri, chakula, malazi, dawa, vipimo vya hospitali, n.k. Makasi alirudi Mwanza miezi michache baadaye akiwa mlemavu wa kusukumwa kwenye kiti au kutembelea baiskeli ya kunyonga kwa mkono. "Mpaka sasa hivi unavyoniona, siwezi kusimama wala kutembea. Na ninatumia mpira kwa ajili ya haja ndogo," alisema Makasi huku akiutoa mpira wake wa kuhifadhi haja ndogo na kunionyesha.

Maisha ya Makasi yalikuwa magumu sana baada ya kurejea Mwanza kwani hakuwa na njia nyingine ya kujipatia kipato zaidi ya umachinga na serikali iligoma kuwaruhusu wamachinga kuwepo katikati ya jiji. Nuru ilionekana mwaka 2016 baada ya Rais wa awamu ya tano, John Pombe Magufuli, kuwaruhusu wamachinga wafanye shughuli zao katikati ya jiji huku akiweka wazi kuwa, iwapo utatokea mgongano kati ya haki-jiji ya wamachinga na mipango mingine ya serikali basi haki-jiji ipewe kipaumbele. Kama ilivyo kwa wamachinga wengine, Makasi aliupokea uamuzi huo kwa furaha, na yeye pamoja na wenzake walirejea Makoroboi na kujenga vibanda vyao kwa

unadhifu. Wakaendelea kuuza bidhaa zao na kipato chao kilizidi kuongezeka.

Nilipomtembelea katika eneo la Makoroboi tarehe 8 Oktoba 2021, Makasi alikuwa ni mtu mwenye huzuni kubwa. Kiongozi aliyekuwa ametambua haki-jiji ya wamachinga hakuwepo tena duniani na serikali mpya iliyoingia madarakani ilikuwa imeamuru wamachinga kuondolewa kutoka maeneo ya katikati ya miji na majiji nchini kote. Zikiwa zimebaki siku chache kabla ya kutimia siku 30 ambazo wamachinga walipewa kwa ajili ya 'kufungasha virago' vyao, tayari kulikwa na mazoezi ya kushitukiza ya kubomoa vibanda vya wamachinga na kupora vitu vyao katika maeneo mbalimbali nchini. Mazoezi hayo yalifanyika usiku wa manane wakati wamachinga wakiwa majumbani mwao.

Hapo Makoroboi, Mwanza, kulikuwa na taharuki kubwa kwani wamachinga walikuwa wameamriwa kuhamia kwenye eneo lijulikanalo kama Mchafu Kuoga ambalo liko nje kabisa ya jiji. Mmachinga humuuzia mteja kwa kumfuata aliko au kwa kupanga bidhaa sehemu yenye mzunguko mkubwa wa watu ili kushawishi wapita njia wanunue. Kuwatimua kutoka maeneo yenye mzunguko wa watu na kuwapeleka pembezoni ilikuwa sawa na kuua vyanzo vyao vya maisha. Kwa kuwapeleka wamachinga nje ya mji na kuwarundika katika eneo moja, serikali ilitarajia kubadili mantiki ya umachinga: badala ya mmachinga kumfuata mteja aliko, basi mteja ndiye amfuate mmachinga aliko.

"Wafanyabiashara wakikaa wote kwenye maeneo yanayolingana," alitamka mhandisi Robert Gabriel, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, "wanunuzi wote wataenda kwenye eneo hilo."[1] Akiwaamuru wamachinga wa Makoroboi kwenda Mchafu Kuoga, mkuu huyo wa mkoa alisema: "Wote mkae eneo moja, riziki itakuja humo humo, itakufuata. Wote tuingie kwenye maeneo hayo yote, wote tutakuja kununua huko huko." Hoja walizotoa wamachinga juu ya asili ya biashara yao hazikusikilizwa. Kila mara wamachinga waliposisitiza kuwa asili ya biashara yao ni kuwafuata wateja, serikali iliwajibu kuwa waende nje ya jiji, wateja wangekuja huko huko!

Wakati nikifanya nae mahojiano, Makasi alikuwa akizungumza kwa sauti ya chini na iliyojaa huzuni lakini tulipoanza kuzungumzia suala la kuhamishiwa eneo la Mchafu Kuoga, alipandisha sauti kwa hasira: "Siondoki hapa mimi! Nasema siondoki." Aliuliza,"Hebu tazama hali yangu hii kaka, niende wapi?" Alisema kuwa kama ni kufa, atafia hapo hapo Makoroboi. "Walishanipiga risasi na kunipatia ulemavu wa kudumu. Sasa waje wanimalizie kabisa." Mahojiano yangu na Makasi yaliyoanza saa 11 jioni yalimalizika majira ya saa 2 usiku. Nje ya kibanda cha Makasi, wamachinga wengi walikuwa wakifuatilia mahojiano yetu. Usiku huo wengi wao walikuwa wameamua kukesha katika eneo hilo ili kulinda bidhaa zao

[1]*Jambo TV*, "RC Mwanza Atinga Makoroboi: Shuhudia Kilichotokea Baadae Katika Mkutano na Wananchi," Oktoba 23, 2021. Imepatikana Novemba 21, 2022 kutoka https://www.youtube.com/watch?app=desktop&v=Ms7Wl28qmgQ.

kwani nyakati za usiku kulikuwa na bomoa bomoa za kushtukiza ambapo mgambo walipora bidhaa za wamachinga na kuondoka nazo. Siku sita baadaye, zoezi la aina hiyo lilifanyika katika maeneo mbalimbali ya wamachinga jijini Mwanza, ambapo mbali na kuporwa bidhaa zao, wamachinga walipigwa na kujeruhiwa. Kati ya waliojeruhiwa alikuwemo katibu wa wamachinga wilaya ya Nyamagana, Hidaya Juma, ambaye alilazwa katika hospitali ya Butimba.

Ilipofika Oktoba 22, 2021, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, alitembelea eneo la Makoroboi na kuwajulisha wamachinga kuwa hiyo ndiyo ingekuwa siku yao ya mwisho katika eneo hilo. Kuepusha shari, wamachinga waliondoa vibanda vyao lakini siku chache zilizofuata walifanya maandamano ya kupinga zoezi la kuwahamisha kutoka katikati ya jiji kwenda pembezoni. Hayo hayakuwa maandamano ya kwanza na wala hayakuwa ya mwisho. Mwezi Desemba 2022, wamachinga walijaribu kuandamana jijini Mwanza. Adam Malima, mkuu mpya wa mkoa wa Mwanza aliyerithi kijiti kutoka kwa mhandisi Gabriel aliamuru jeshi la polisi kufuatilia wachochezi wa maandano hayo, japokuwa yeye mwenyewe alikiri kuwa maeneo ambayo wamachinga walipelekwa hayakuwa rafiki kwa biashara zao na usalama wao. Malima aliweka wazi kuwa alipoyatembelea baadhi ya maeneo alishangaa kukuta yakiwa ni mapori ambayo hayakufanyiwa usafi na hivyo yalikuwa na wanyama hatari kama nyoka. Pia, hayakuwa na miundombinu ya msingi na yalikuwa katika maeneo

yasiyofikika.[2] Hii ni kusema kuwa muujiza wa mteja kumfuata mmachinga aliouhubiri mhandisi Gabriel haukuwa umetokea. Licha ya kukiri udhaifu huo, bado Malima, kama alivyokuwa mtangulizi wake, alishikilia msimamo kuwa wamachinga hawapaswi kurudi katikati ya jiji kwani mpango ni kuifanya Mwanza kuwa "mji wa kisasa, mji wa kitalii" na ingekuwa aibu kwa watalii kutembea barabarani wakakutana na wamachinga wakiuza mafenesi. Hii inadhihirisha wazi kuwa lengo la watawala kupanga upya miji sio kutimiza mahitaji wa wananchi walio wengi bali matamanio ya wachache. Iwapo wameondoa mamilioni ya wamachinga katikati ya jiji, tena kwa kutumia mabavu na kupora mali zao, kisha miaka miwili baadaye, watawala hao hao wanakiri kuwa mahali walipowahamishia hapafai kwa biashara zao, je, watawala hao waliwahi kufikiria kuwa ndani ya hiyo miaka miwili wamachinga hao waliishi vipi?

Kwa kuwa watawala hawatatui tatizo kwa kushughulikia kiini chake na badala yake hulifunika kwa kutumia mabavu ya dola, maandamano ya wamachinga yamekuwa yakilipuka mara kwa mara katika majiji yote nchini kupinga kuondolewa kwao katikati ya jiji. Hata hivyo, habari za maandamano hayo hazijitokezi sana kwenye vyombo vya habari na hata pale zinapojitokeza hazipewi uzito unaostahili. Ili kujua sababu za maandamano ya wamachinga

[2]*M24 Online Media*, "Msimamo Mkuu wa Mkoa Mwanza Machinga Kurudi Mjini!" Decemba 22, 2022. Imepatikana Januari 5, 2023 kutoka https://www.youtube.com/watch?v=6a_HcTFNHZQ.

kutokupewa kipaumbele katika vyombo vya habari, nitasimulia kisa cha mwanahabari wa umma Mabere Makubi na wamachinga.

**Mabere Makubi: Mwanahabari Shujaa**

Wakati mazoezi ya bomoa bomoa za usiku wa manane na uporaji wa mali za wamachinga yakiendelea mwezi Oktoba 2021, ni wanahabari wachache waliothubutu kutoa habari hizo na kupaza sauti za wamachinga. Mmoja wa wanahabari hao ni Mabere Makubi aliyekuwa ameajiriwa na kituo cha televisheni cha ITV. Kutokana na kutoa habari iliyohusu maandamano ya wamachinga wakipinga uonevu waliokuwa wakifanyiwa, mwanahabari huyo alizuiliwa kutangaza habari zozote za serikali katika mkoa wa Mwanza. Kwenye mkutano wa Msemaji Mkuu wa Serikali na wanahabari uliofanyika jijini Mwanza Oktoba 17, 2021, Makubi, kwa ujasiri mkubwa, alieleza kadhia aliyokumbana nayo:

> *Baadhi ya waandishi wa habari tunaoandika habari kwa ajili ya kuelimisha jamii, tunaingia kwenye misukosuko na kutishiwa na vyombo vya usalama. Mmojawapo, nataka niwe mkweli, ni mimi. Juzi nimeripoti habari ya wafanyabiashara wadogo wa Mwanza kuandamana kuja ofisini kwa Mkuu wa Mkoa kuelezea malalamiko yao kutokana na hatua inayodaiwa kufanywa na askari mgambo wa Jiji la Mwanza kwenda usiku wa manane majira ya saa 8 usiku kuvunja vibanda*

> *vyao na baadhi kudai kwamba hata mali zao zimeporwa. Nimefuatilia tukio hilo kuanzia eneo la Makoroboi mpaka ofisi ya Mkuu wa Mkoa getini. Hivi sasa tunavyozungumza, muda huu, Mkuu wa Mkoa, kupitia kwa msaidizi wake, Bwana Levy, ananiambia, "Wewe Makubi hutakiwi kwenda kwenye tukio kuandika habari kwa sababu ulishakuja kuandika habari. Sisi tunakwenda na watu wangu." Ina maana amechagua watu wa kwenda kufanya nao kazi. Mimi ni mwandishi wa habari. Nina haki ya kutafuta habari: nina haki ya kualikwa, nina haki ya kwenda bila kualikwa. Naomba kufahamu, ni lini tutafikia hatua ya kuacha ukiritimba wa namna hii? Waandishi tunapoandika habari ... zinazoweza kusaidia wananchi wanaolalamika kufikisha kilio chao, sisi ni daraja[3].*

Ilitarajiwa swali la Makubi lingesaidia kutanua wigo wa uhuru wa wanahabari na kuwaaibisha watawala wanaowatishia waandishi wanaotoa habari zinazohusu uonevu wanaofanyiwa watu wa tabaka la chini. Lakini haikuwa hivyo. Kwa kuuliza swali hilo, Makubi alionekana kama aliyetangaza vita na serikali ya mkoa wa Mwanza. Kilichofuatia ni yeye kusimamishwa kazi na mwajiri wake, japokuwa chombo cha habari kilichomwajiri ni cha binafsi. Hatua hii iliwaogofya wanahabari ambao sasa walijua

[3] *EastAfricaTV*, "Taarifa ya Msemaji wa Serikali Mwanza," Oktoba 17, 2021. Imepatikana Novemba 20, 2022 kutoka https://www.youtube.com/watch?app=desktop&v=4pKlD74Zut4.

kuwa dola lilikuwa limeweka mstari mwekundu ambao wanahabari hawakutakiwa kuvuka. Jambo hili lilifanya vitendo vya kionevu vilivyofanywa na dola kwa wamachinga visimulikwe na mtu yeyote.

Tofauti na zamani ambapo ilikuwa rahisi kwa mwanahabari kuachishwa kazi na chombo kimoja na kisha kuajiriwa na chombo kingine, katika kipindi hiki cha fungate mpya kati ya dola na mtaji, pamoja na sheria kandamizi ya huduma za habari, ni mwanahabari binafsi, badala ya chombo chake, ndiye huwajibishwa pale inapoandikwa habari isiyowapendeza watawala. Iwapo mwanahabari huyo atafukuzwa kazi na chombo kimoja, basi kila mwajiri ataogopa kumwajiri kwani wamiliki wa habari wanaangalia zaidi maslahi yao ya mtaji kuliko uhuru wa habari. Hicho ndicho kilichotokea kwa Makubi.

Baada ya kukaa mtaani, bila utetezi wowote kutoka kwa wanahabari wenzake, aliambiwa kuwa njia sahihi ya yeye kurejea kazini ni kuomba msamaha kwa serikali ya mkoa wa Mwanza. Hii ilikuwa ni fedheha kwa Makubi lakini hakuwa na namna zaidi ya kujishusha. Kwa unyenyekevu aliitisha mkutano na wanahabari mwezi Novemba 2021 na kuomba msamaha kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana kwa kutoa habari ambazo "ziliweza kusababisha pengine mamlaka za uteuzi [wao] ziweze kutaka kujua kulikoni kuhusiana

na suala hili."[4] Makubi alimsihi mkuu wa mkoa wa Mwanza "kama mzazi, kama kiongozi wa serikali, kama mtu ambaye anamjua Mungu na mtu ambaye amejipambanua kwa namna moja ama nyingine kama mtumishi wa Mungu" amsamehe.

Inavyoonekana safari hii watawala walikuwa wameamua kumtumia Makubi kama fundisho kwa wanahabari wengine. Kwa muda mrefu, Makubi alikuwa amejizolea sifa kama mwanahabari asiyeweza kutishwa na watawala na aliyefanya kazi yake kwa weledi bila uoga. Msimamo wake ulimletea misukosuko mara kadhaa. Mwaka 2011, Makubi alikuwa kati ya waandishi wanne walioshikiliwa na Jeshi la Polisi wilayani Tarime walikokuwa wamekwenda kusaka "taarifa za polisi kuua wananchi karibu na mgodi na kutupa maiti zao barabarani huku wakidai wamezipeleka kwa jamaa zao kwa mazishi."[5] Mwaka uliofuatia alinusurika kupigwa na kunyang'anywa kamera aliyokuwa akiitumia kurekodi mapigano baina ya vigogo wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) mkoa wa Mara katika mkutano wa uchaguzi wa jumuiya hiyo. Licha ya kumtishia

[4]*Matukio Daima TV*, "Nimesimama Kazi ITV kwa Taarifa ya Sintofahamu Juu ya Machinga - Mwanahabari Mabere Makubi." Novemba 22, 2021. Imepatikana Novemba 20, 2022 kutoka https://www.youtube.com/watch?v=mqSuvqgIhow.

[5]Ndimara Tegambwage, "Kilio Cha Wananchi, Waandishi Kuteswa, Kuuawa: Usalama wa Mwandishi wa Habari Tanzania." Mada Iliyowasilishwa kwenye Mkutano Mahususi wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Mei 14, 2013, Dar es Salaam. Imepatikana Novemba 20, 2022 kutoka http://ndimara.blogspot.com/2013/05/kilio-cha-waandishi-kuteswa-kuuawa.html?m=1.

kumshushia kipigo, vigogo hao wa UVCCM mkoa wa Mara hawakuweza kumnyamazisha Makubi wala kumnyang'anya vitendea kazi vyake. Vitisho havikukoma. Tarehe 9 Aprili 2021, Makubi alipokea vitisho kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Philis Nyimbi, aliyeripotiwa "kumtishia kumfanyia kitu kibaya mwandishi wa ITV Mabere Makubi ambacho kitamsababisha afutwe kazi. Hii ni kutokana na kutoridhishwa na habari aliyoitoa."[6] Vitisho hivyo vilitimia miezi 7 baadaye.

Licha ya kufedheheshwa kiasi cha kuomba msamaha bado mwanahabari huyo hakurejeshwa kazini! Hizo ni gharama ambazo Makubi alizilipa kwa kujaribu kuweka hadharani yaliyokuwa yakiendelea kwenye bomoa bomoa za vibanda vya wamachinga zilizokuwa zikifanyika usiku wa manane. Siku itakapoandikwa historia ya wanahabari wa umma na mashujaa wa haki-jiji nchini Tanzania, waliolipa gharama kwa kusimama na wamachinga dhidi ya uporaji, basi jina la Makubi litapaswa kuwemo.

## Maisha Yasiyo na Thamani

Nimeamua kuanza na visa hivi viwili vinavyohusiana. Kisa cha Makasi kinawahusu wavujajasho wanaojitafutia riziki katika majiji na madhila

[6] *DW-Idhaa ya Kiswahili*, "Polisi Tanzania Yashutumiwa kwa Kuhangaisha Wanahabari," Aprili 22, 2021. Imepatikana Novemba 20, 2022 kutoka https://www.dw.com/sw/polisi-tanzania-yashutumiwa-kwa-kuhangaisha-wanahabari/a-57285451.

wanayokumbana nayo, yakiwemo kuporwa bidhaa zao, kupigwa na risasi za moto, kulazwa mahabusu, n.k. Kisa cha Makubi kinahusu gharama ambazo wanahabari wa umma wanalipa kwa kujaribu kuweka hadharani uonevu wanaofanyiwa wavujajasho katika majiji.

Makasi anawakilisha tabaka la chini, tabaka la *walalahoi* ambalo hupitia uonevu wa kila siku unaofanywa na dola kwa kushirikiana na mabepari lakini kilio chao hakisikiki na uonevu wanaofanyiwa hauonekani. Haupigiwi kelele katika vyombo vya habari na wala hakuna asasi ya kupigania haki za binadamu inayopigania haki za wamachinga. Kwa hapa Tanzania, tabaka la kati (*walalahai*) linakubaliana na tabaka la juu (*walalaheri*) kuwa timua timua inayofanywa na dola dhidi ya *walalahoi* (wamachinga) ni zoezi la lazima kufanyika ili kulinda taswira na mandhari ya jiji pamoja na sheria za mipango miji. Kwa hiyo, ukatili na uonevu unaofanywa na dola huonekana kama jambo lisilozuilika na mara nyingi wamachinga hulaumiwa kwa ukaidi wao unaolifanya dola lisiwe na namna zaidi ya kutumia nguvu. Hizi ni fikra mfu zilizojikita katika ubinafsi wa kitabaka bila kufikiria kuhusu maisha ya watu wa tabaka la chini.

Rafiki yangu mmoja aliwahi kusema kuwa iwapo hata asilimia moja ya uonevu wanaofanyiwa wamachinga (ikiwemo kuporwa bidhaa zao) ungeelekezwa kwa watu wa tabaka la juu basi kungeibuka kelele za ajabu kutoka kwa wakubwa wa dunia kulaani uvunjifu

wa 'haki za binadamu'. Kelele hizo zingerudufishwa na asasi za kiraia za kutetea haki za binadamu na zingekuwa ajenda kuu ya vyombo vya habari vya kimataifa. Serikali iliyoko madarakani ingeitwa serikali ya kikomunisti na kungekuwa na vikwazo vya kila aina dhidi ya serikali hiyo. Bila shaka nchi za Magharibi zingekuwa zinajiandaa kuivamia Tanzania kwa ajili ya kurejesha 'demokrasia' na 'haki za binadamu' kwa kutumia mabomu ya NATO. Lakini wanaofanyiwa uonevu huo sio watu wa tabaka la kati au la juu bali watu wa tabaka la chini, ambao hawatazamwi kama binadamu wenye haki sawa na wengine. Ndani ya mfumo wa ubepari wa soko huria, maisha ya watu wa tabaka la chini ni maisha yasiyo na thamani (*unworthy lives*) ilhali yale ya watu wa tabaka la kati na juu ndiyo huonekana yenye thamani (*worthy lives*)[7] . Alimradi dola lilioloko madarakani linaendelea kutekeleza sera za soko huria, kuusujudia ubeberu na kutimiza maslahi ya matabaka ya walalahai na walalaheri, basi sauti za kupinga uonevu dhidi ya wamachinga hazitasikika.

Hii pia inatupatia taswira juu ya namna ambavyo dola linashughulika na matabaka katika mfumo wa ubepari wa soko huria (uliberali mamboleo). Kwa walalahai na walalaheri, wakiwemo wahisani na wawekezaji, dola la kiliberali mamboleo hujionyesha kama dola dhaifu na kwa maana hiyo watu hao hupata uhuru

[7]Edward S. Herman and Noam Chomsky, *Manufacturing Consent: The Political Economy of the Mass Media* (London: Vintage Books, 1994).

wao, iwe ni wa kufanya biashara, kuendesha shughuli zao kupitia asasi za kiraia na vyama vya siasa. Kwa walalahoi, dola la kiliberali mamboleo hujidhihirisha kama dola la kinyapara, lenye sheria kandamizi na linalojinaisha uwepo wa watu wa tabaka la chini katika miji na vijiji kwa kuwapora vyanzo vyao vya maisha. Baada ya kuitafiti kwa kina tabia hii ya dola katika nyakati za soko huria, mwanazuoni Loïc Wacquant alilitaja dola la kiliberali mamboleo kama 'dola kentauro' (*centaur state*), ambalo, ni nusu mtu na nusu mnyama. Linafanya utu kwa watu wa tabaka la juu na kati na unyama kwa watu wa tabaka la chini[8]. Japokuwa imekomazwa wakati wa mageuzi ya soko huria, mbinu hii ni mwendelezo wa mbinu ya utawala kwa misingi ya kibaguzi iliyopandikizwa wakati wa ukoloni ambapo, katika maeneo ya mijini, wazungu walikuwa raia kamili na wenye haki za binadamu na Waafrika, ambao walikuwa watawaliwa na siyo raia, waliishia kubaguliwa, kunyanyaswa na kuporwa[9]. Mgawanyo huu, kama inavyoonyeshwa katika sura ya pili ya kitabu hiki, haukuishia katika mfumo wa utawala tu bali pia katika utoaji wa huduma za kijamii, fursa za kiuchumi, n.k.

[8]Loïc Wacquant, *Punishing the Poor: The Neoliberal Government of Social Insecurity* (Durham: Duke University Press, 2009), 43 & 312.

[9]Mahmood Mamdani, "Historicizing Power and Responses to Power: Indirect Rule and Its Reform," *Social Research* 66, no.3 (Fall 1999): 875.

## Kwa Nini Kitabu Hiki?

Kama ilivyoelezwa hapo juu, Tanzania, kama zilivyo nchi zingine, imekuwa ikiwaondoa wafanyabiashara wadogo wadogo, maarufu kama wamachinga kutoka katika maeneo ya katikati ya jiji. Aghalabu, mazoezi hayo ya timua timua hutumia mabavu na kusababisha hasara, maumivu na utwezaji wa utu wa wamachinga. Kitabu hiki kinachambua mtazamo, sera na sheria zinazotumiwa na serikali ya Tanzania katika kupanga miji na kuwatimua wamachinga. Kinaonyesha kuwa zina asili ya uonevu wa kitabaka, ulioanza wakati wa ukoloni na kukomaa katika kipindi cha uliberali mamboleo.

Kila mara wamachinga wanapodai haki yao ya kujipatia kipato katikati ya jiji huonekana kama mahayawani wanaotoa madai yasiyotekelezeka. Kitabu hiki kinayaweka madai ya wamachinga katika muktadha na kuonyesha kuwa sio madai ya kihayawani bali ni madai halisi na yanayotekelezeka, yaliyojikita katika nadharia ya haki-jiji. Mifano ya sera, sheria na maazimio ya kimataifa juu ya haki-jiji pamoja na utekelezaji wake katika nchi mbalimbali imetolewa. Tanzania haipaswi kubaki nyuma. Kitabu hiki kinapaza sauti ya wamachinga katika kudai HAKI-JIJI SASA!

Kitabu hiki kina sura sita. Sura mbili za mwanzo zimeandikwa na waandishi wawili - **Sabatho Nyamsenda** na **Abunuwasi L. Mwami**. Sura ya

kwanza inatoa uchambuzi wa mfumo wa kibepari kwa kuainisha tabia zake na kuonyesha hatua ambazo mfumo huo umepitia. Athari za majilio ya ubepari katika bara laAfrika pia zimeainishwa. Hizo ni pamoja na unyonyaji wa nguvu-kazi na rasilimali za Afrika ambao umestawisha nchi za Magharibi na kuifukarisha Afrika. Sura hii pia imeonyesha namna ambavyo Waafrika wamekuwa wakipambana dhidi ya ubepari katika sura zake mbalimbali. Mapambano hayo, tangu enzi za Mkwawa hadi zama za Nyerere ni mapambano ya ukombozi. Katika zama za ubepari wa soko huria mapambano dhidi ya unyonyaji na uporaji hayajakoma, iwe ni kwa wafugaji wa Ngorongoro au wamachinga wa Dar es Salaam.

Sura ya 2 imewaangazia wamachinga ndani ya mfumo na jiji la kibepari. Sura hii imefafanua maana ya mmachinga na sababu za kuibuka kwa umachinga na kuonyesha ni jinsi gani mikanganyiko na mabadiliko katika ya mfumo wa ubepari vimepelekea uibukaji wa kundi kubwa la watu wasiokuwa na ajira, ambao hawana namna ya kuishi zaidi ya kujitafutia riziki katika kiitwacho sekta isiyo rasmi. Sura hii pia imechambua historia ya majiji, ikilitazama jiji la Dar es Salaam na namna lilivyosukwa kwa misingi ya ubaguzi wa rangi na wa kitabaka. Hata baada ya ukoloni kuangushwa na ubaguzi wa rangi kukomeshwa, ubaguzi wa kitabaka uliendelea kutamalaki na ulijidhihirisha kwa namna mabavu yalivyokuwa yakitumika kuwaondoa wavujajasho kutoka katika maeneo ya katikati ya jiji. Ujio wa uliberali mamboleo na dira yake ya ujenzi

wa jiji la viwango vya kimataifa umechochea zaidi ubaguzi wa kitabaka na miongoni mwa waathirika wa mazoezi ya timua timua na bomoa bomoa wamekuwa ni mafukara wanaojishughulisha na umachinga. Mazoezi haya yanayotumia mabavu makubwa ya dola yameacha dhahma kubwa kwa wamachinga, zikiwemo kuporwa bidhaa, kujeruhiwa na kuachwa na ulemavu wa kudumu. Iwapo mtu anataka kufahamu ukatili wa dola basi anapaswa kuutazama kwa namna dola linavyohusiana na watu wa tabaka la chini! Huko atagundua kuwa hakuna demokrasia licha ya majigambo ya utekelezaji wa demokrasia na haki za binadamu. Sura hii pia imepaza sauti ya wamachinga juu ya aina gani ya jiji wanalolitaka - jiji ambamo wana haki ya kuyafikia na kuyatumia maeneo yaliyo na mzunguko mkubwa wa watu kwa ajili ya kujipatia riziki zao.

Sura ya 3 iliyoandikwa na **Joseph Chiombola** inafanya uchambuzi wa sera na sheria za ardhi na mipango miji ili kuonyesha misingi yake. Mwandishi anatufahamisha kuwa uonevu unaofanyika dhidi ya wamachinga umelindwa na sheria hizi na hasa sheria ndogo zinazotungwa na halmashauri za miji na majiji kwa ajili ya kuratibu shughuli za umachinga. Chombo kinachotumiwa kuhukumu watu wanaodaiwa kukiuka sheria ndogo ni Mahakama ya Jiji iliyopo jijini Dar es Salaam. **Chiombola** anatufahamisha kuwa "kwa mazingira ya utekelezaji wa sheria ndogo za halmashauri na usikilizaji wa mashauri kwenye Mahakama ya Jiji, mmachinga huweza kukamatwa

asubuhi halafu mchana akafikishwa kwenye mahakama hiyo ya jiji na kufikia saa tisa akajikuta anaingizwa gerezani." Kwa ufupi, uonevu dhidi ya wamachinga unalindwa na sheria kandamizi na umewekewa vyombo ambavyo haviendeshwi kwa kufuata taratibu za kawaida za kimahakama za usikilizaji wa mashitaka!

Sura ya 4, iliyoandikwa na **Sabatho Nyamsenda**, inajenga msingi wa kinadharia wa hitimisho la sura ya 3 juu ya wamachinga kuungana ili kupigania mabadiliko ya kisera na kisheria. Sura hii inautanua mjadala na kutoa dira ya kinadharia inayopaswa kuongoza mapambano ya wamachinga. Dira hii ni haki-jiji. Japokuwa dhana ya haki-jiji iliibuliwa na mwanazuoni wa kimapinduzi Henri Lefebvre mwaka 1967, ukweli ni kwamba dhana hii imeanzia mtaani kwa watu wa tabaka la chini wakipigania haki na usawa katika jiji, haki ya kukaa na kutumia maeneo ya jiji na pia kushiriki kikamilifu katika kuliendeleza jiji kwa viwango vinavyokidhi matamanio ya mioyo yao[10]. Hata nukuu za wamachinga wenyewe zilizotolewa mwishoni mwa sura ya 1 ya kitabu hiki zinathibitisha hivyo. Sura hii ya 4 inatofautisha mitazamo miwili ya haki-jiji: mtazamo wa kimapinduzi na mtazamo wa kimageuzi. Mtazamo wa kimapinduzi umelenga kuondoa misingi mikuu ya ubepari ili kujenga jiji jipya. Mtazamo wa kimageuzi unakusudia kufanya mageuzi

[10]David Harvey, *Rebel Cities: From the Right to the City to the Urban Revolution* (London: Verso, 2012), x-xii & 4.

madogo ili kutoa unafuu kwa watu wanaokandamizwa. Kumekuwa na mjadala mkubwa baina ya wanazuoni na wanaharakati juu ya mitazamo hii miwili huku baadhi wakilazimika kuchagua upande. Hata hivyo kitabu hiki kinashauri kuwa mitazamo yote miwili inaweza kutumika katika mapambano, mtazamo wa kimageuzi ukiongoza madai ya muda mfupi ili kuleta unafuu na mtazamo wa kimapinduzi ukitoa dira kwa madai ya muda mrefu ili kujenga jiji jipya lisilo na chembe za ubepari. Mifano dhahiri ya mapambano ya wamachinga katika kuzilazimisha serikali kutambua haki zao imetolewa ikigusia nchi za India na Brazil ambako sera na sheria zinazotambua haki-jiji zimetungwa kutokana na msukumo wa wavujajasho wa mijini!

Sura ya 5, iliyoandikwa na **Michaela Collord** inaendeleza pale sura ya 4 ilipoishia. Iwapo mifano ya mapambano iliyotolewa katika sura ya 4 iligusia mapambano katika ngazi ya kitaifa na kimataifa, basi sura ya 5 inatoa mifano ya mapambano ya kila siku ya wamachinga katika ngazi ya mtaa, yenye lengo la kusimika haki-jiji katika maeneo ambako wamachinga wanafanyia kazi. Mapambano hayo yaliyotokea katika majiji ya Durban (Afrika Kusini) na Ahmedabad (India) sio tu kwamba yalifanikisha kuzuia timua timua za wamachinga katika ngazi ya mitaa bali pia yalikuwa sehemu ya harakati zilizofanikisha kutambuliwa kwa haki zao katika ngazi ya mtaa na baadaye kusimikwa na mageuzi katika ngazi ya kitaifa. Kisa cha wamachinga wanawake walioongoza mapambano

ya kudai haki-jiji huko Ahmedabad ni cha kusisimua. Licha ya vitisho na vikwazo kutoka katika mamlaka za serikali, wanawake hao mashujaa walisimama kidete na hatimaye wakafanikiwa kupata ushindi.

Ukiachilia mbali ujasiri, silaha nyingine za mapambano zilizotumiwa na wanawake wa Ahmedabad ni umoja na mshikamano pamoja na dira ya kuongoza mapambano yao. Mshikamano ulionekana pale ambapo wamachinga wanaume pamoja na wateja waliungana na wanawake hao katika kudai haki yao ya kufanya kazi katika maeneo ya katikati ya jiji. Vilevile, **Collord** anatudokezea kuwa wanawake hao mashujaaa "walikuwa sehemu ya umoja (Chama cha Wanawake Waliojiajiri) uliojumuisha muungano na pia ushirika." Anaendelea kutufahamisha kuwa "Ushirika ulitoa mikopo kwa wanawake kununua bidhaa kutoka kwa wauzaji wa jumla kwa kiwango cha ushindani" wakati ambapo Muungano ulikuwa ukijadiliana na mamlaka za serikali kuhusu madai ya wanawake hao.

Mjadala wa ushirika kama chombo cha upiganiaji na utekelezaji wa haki-jiji unaendelezwa katika sura ya 6 iliyoandikwa na **Christina Mfanga**. Kama ilivyofafanuliwa katika sura ya 4, haki-jiji ni haki ya pamoja (*collective right*) na sio haki ya mtu mmoja mmoja. Pili, kati ya misingi mikuu ya dhana ya kimapinduzi ya haki-jiji ni umiliki wa pamoja na ushiriki wa pamoja. Katika mfumo wa kibepari, ushirika ni kati ya vyombo muhimu vinavyowaleta

wavujajasho katika kujenga nguvu ya pamoja ili kukabiliana na wanyonyaji wao na kujenga mbadala. Kwa ufupi, ushirika ndicho chombo cha utekelezaji wa haki-jiji.

Licha ya manufaa hayo ya ushirika, bado leo hii ukitaja neno ushirika kwa wavujajasho hususan wa vijijini watakwambia kuwa ushirika ni chombo cha kinyonyaji na hivyo hawataki kujiunga. Ni kwa nini imetokea hivyo? Swali hili linajibiwa kwa ustadi mkubwa na **Mfanga** ambaye anaidurusu historia ya ushirika nchini Tanzania, tangu kuanza kwake wakati wa ukoloni hadi leo hii. Historia hii inadhihirisha kuwa kwa upande wa wavujajasho, hasa wakulima vijijini, ushirika ulikuwa chombo cha kuwaunganisha ili kupambana dhidi ya wanyonyaji wao, hasa wafanyabiashara wenye asili ya Kiasia waliokuwa wakilangua mazao kwa bei ya chini na kuyauza nje kwa bei ya juu. Dola la kikoloni halikutaka vyama vya ushirika viwe huru, hivyo basi, lilitunga sheria zilizowapatia warasimu nguvu ya kuingilia mambo ya ndani ya vyama vya ushirika. Sheria hizo pia zililipatia dola haki ya kukusanya tozo kutoka kwa wakulima kupitia vyama vya ushirika.

Baada ya uhuru kupatikana, mahusiano kati ya dola na vyama vya ushirika hayakubadilika. Badala yake, dola liliongeza juhudi katika kuhamasisha uundaji wa vyama vya ushirika, kinyume na misingi ya ushirika inayotaka vyama viwe huru na viundwe kwa hiyari ya wanachama.

Mwaka 1976, dola la Tanzania lilifuta vyama vikuu vya ushirika (*cooperative unions*) na nafasi yake ikichukuliwa na mamlaka za mazao za serikali. Baada ya kutoka madarakani, Mwalimu Nyerere alikiri kuwa kati ya makosa ambayo serikali yake iliwahi kufanya ilikuwa ni kufuta vyama vya ushirika na serikali za mitaa[11].

Japokuwa serikali ya Mwalimu Nyerere ilirekebisha makosa hayo kwa kurejesha serikali za mitaa na vyama vya ushirika mwaka 1982, vyombo hivi havikuwa huru kwa namna yoyote. Vilihodhiwa na kudhibitiwa na dola badala ya wanachama (kwa upande wa vyama vya ushirika) na wananchi (kwa upande wa serikali za mitaa). Mifano halisi ya uhodhi na udhibiti huu kupitia sheria umetolewa vema katika kitabu hiki.

Itoshe kusema kuwa, wakati vyama vya ushirika vinarejea, vilirejea katika zama mpya, zama za mpito kutoka ujamaa kuelekea soko huria. Ilipofika miaka ya 1990, Mwalimu Nyerere akiwa ameshang'atuka madarakani, vyama vya ushirika vilianza kuhujumiwa na kufilisiwa. Warasimu serikalini na katika chama tawala walikuwa wameshalipiga teke Azimio la Arusha na hasa miiko ya uongozi ambayo ilikuwa imewazuia viongozi kuwa mabepari. Zilikuwa zama mpya, zama za 'Azimio la Rushwa,' lililosimika misingi ya ulafi, unyonyaji, ubinafsi na uporaji. Kulikuwa na

---

[11]Julius K. Nyerere, *Hotuba ya Mwisho ya Rais J.K. Nyerere katika Bunge* (Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers, 2022), 32.

mgawanyo wa kazi katika uporaji wa mali za umma: mabepari kutoka nje walikabidhiwa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa ilhali mabepari uchwara wa ndani pamoja na watawala waligawana mali za vyama vya ushirika. Kufumba na kufumbua, viwanda vya kuchambua pamba, mashamba, majumba, magari na mali nyingine zilizokuwa zikimilikiwa na vyama vya ushirika zikawa mali za watu binafsi. Vyama vya ushirika vikahujumiwa na kufilisiwa. Baadhi vikafa, na vile vilivyobakia vikabadili wajibu: kutoka vyombo vya kuwaunganisha wazalishaji dhidi ya wanyonyaji kuwa vyombo vinavyotumika kama mawakala wa walanguzi. Wazalishaji vijijini wakapoteza imani navyo.

Ni katika kipindi hiki ndipo vilipoibuka vyama vipya vya ushirika - ushirika wa kuweka na kukopa - na sehemu kubwa ya vyama hivyo vikiwa katika maeneo ya mijini. Sababu zilizopelekea uibukaji wa ushirika huu mpya hazitofautiani na zile zilizopelekea uundwaji wa ushirika wa zamani. Iwapo ushirika wa zamani ulianzishwa ili kupambana na walanguzi katika sekta ya mazao katika uchumi wa kikoloni uliotegemea usafirishaji wa malighafi kwenda nje, basi ushirika mpya ulianzishwa kwa ajili ya kuwakinga wavujajasho dhidi ya unyonyaji na uporaji unaofanywa na benki katika uchumi wa soko huria ambako kila kitu kiligeuzwa kuwa bidhaa na kuuzwa sokoni. Hata hivyo, kama ilivyokuwa katika ushirika wa mwanzo, ushirika mpya nao umeangukia katika mbawa za dola na makucha ya soko huria. Hii imepelekea vyama

vipya vya ushirika kugawanyika katika makundi mawili: ushirika tegemezi na ushirika mbadala.

Ushirika tegemezi hutegemea ufadhili kutoka kwa wahisani na umefungamanishwa na benki pamoja na taasisi za mikopo midogo.  Ushirika huu hutumika kama vyombo vya kuendeleza unyonyaji na uporaji wa mali za wavujajasho pamoja na kupigia chapuo maadili ya soko huria kama ubinafsi, ubidhaishaji, ulimbikizaji mtaji, na mgawanyo wa kitabaka. Ushirika mbadala kwa kiasi kikubwa hautegemei ufadhili, umejiengua katika taasisi za kifedha, hususan taasisi za mikopo midogo. Ushirika huu hutumiwa na wavujajasho kama ngao ya kuwakinga dhidi ya makali ya maisha, unyonyaji na uporaji unavyosababishwa na ubepari. Pia, ushirika huu hutumiwa na wavujajasho kama jukwaa la kudai haki zao. Maadili yanayopigiwa chapuo ni yale ya umoja, mshikamano, usawa, madai ya huduma za kijamii zinazogharamiwa na umma, nk.

Ni ushirika mbadala ndio utakaoweza kutumiwa na wavujajasho walio katika sekta ya umachinga kama vyombo vya kimapambano katika kusimika haki-jiji ya kimageuzi wakati wakiendelea na mapambano ya kufanikisha haki-jiji ya kimapinduzi. Ushirika mbadala utapaswa kujifunza kutokana na mapungufu ya vyama vya ushirika vya mwanzo ili kuweka misingi imara kwa wavujajasho wa mijini kujikomboa.

Kama ambavyo **Mfanga** anafafanua katika kitabu hiki, ushirika mpya wa kidemokrasia utakuwa na manufaa

kwa wavujajasho, na hasa wamachinga, katika nyanja zote za maisha. Kiuchumi, ushirika unaweza kutumiwa na wamachinga kama vyombo vya umiliki na uendeshaji wa pamoja wa maeneo wanayofanyia biashara. Kisiasa, ushirika utasaidia kutimiza lengo la ushiriki wa pamoja. Demokrasia shirikishi iliyomo ndani ya vyama mbadala vya ushirika itakuwa msingi wa ujenzi wa demokrasia mbadala ndani ya nchi. Vyama vya ushirika, pamoja na vyombo vingine vya wavujajasho, vitakuwa vitovu muhimu na mbadala katika kuhakikisha wavujajasho wanashiriki katika maamuzi ya msingi ndani ya nchi yao, ikiwemo kushinikiza mabadiliko ya sera na sheria ili ziendane na matakwa na maslahi ya wavujajasho.

Kijamii, vyama vipya vya ushirika vinaweza kuwa nguzo ya "ujamiishaji wa malezi ya watoto." Imezoeleka kumwona mwanamke ambaye ni mmachinga akienda na mtoto wake mchanga katika eneo la biashara, ambapo mtoto, kama alivyo mzazi, hushinda juani au kupigwa na mvua, jambo ambalo ni hatari kwa afya na makuzi yake. Kupitia ushirika mpya, huduma za malezi ya watoto wachanga zinaweza kutolewa katika eneo la kazi au hata makazi ili kuhakikisha kuwa watoto wanapata malezi bora na mahitaji muhimu wakati wazazi wao wakihangaika kutafuta riziki. Mifano lukuki juu ya jitihada za ujenzi wa ushirika mpya nchini Tanzania na nje ya nchi imetolewa.

Ni vigumu kufupisha kila kilichomo katika kitabu hiki kwani kimesheheni masuala mengi ya muhimu kwa

wavujajasho katika mapambano yao ya kujenga majiji yenye usawa kwa watu wote. Ni matumaini yetu kuwa kitabu hiki kitasomwa na wamachinga wenyewe, viongozi wa jumuiya za wamachinga pamoja na wavujajasho wengine mijini na vijijini. Kitabu hiki kinawakilisha mchango wetu mdogo, ulio sawa na kijito kiingiacho baharini, bahari yenyewe ikiwa ni mapambano ya kudai haki-jiji. Wamachinga wenyewe ndio wamekuwa wakiyaendesha mapambano hayo miaka nenda, miaka rudi.

Kadhalika, tunaamini kuwa kitabu hiki kitawafaa viongozi na watumishi wa serikali wa ngazi zote, wakufunzi na wanafunzi wa vyuo, wanahabari, wanaharakati na watu wote wenye nia ya dhati ya kujifunza kuhusu haki-jiji na namna bora ya kupangilia, kuendeleza na kuendesha miji na majiji kwa kutimiza matakwa na matamanio ya walio wengi.

## Vuguvugu la Haki-Jiji Litafanikiwa

Agosti 2, 1972, Mwalimu Nyerere alizungumza na walimu na wanafunzi wa Chuo cha Ualimu, Chang'ombe, jijini Dar es Salaam. Katika hotuba yake, Mwalimu alizungumzia juu ya "vuguvugu... linalozuka dunia nzima," la "watu kukataa kusukumwasukumwa na watu wengine," vuguvugu "la kutaka kukomesha binadamu asimnyonye binadamu mwenzake." Alibainisha kuwa vuguvugu hilo la kupinga uonevu na unyonyaji lililokuwa limeenea "dunia nzima" lilijumuisha "hata miongoni mwa watu waliomo

katika nchi za kibeberu". Mwalimu alitoa utabiri kuhusu vuguvugu hilo akisema kuwa "vuguvugu hilo litafanikiwa; hatima yake ubeberu na ubaguzi wa rangi yatakuwa sura moja tu itakayoandikwa katika historia ya mwanadamu: tutasikia habari zake katika majumba ya makumbusho tu!"[12]

Wakati akiandika maneno hayo, sehemu kubwa ya nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa chini ya tawala za kikoloni, iwe ni Wareno ndani ya Msumbiji na Angola, walowezi huko Zimbabwe au makaburu Afrika Kusini, Namibia na Lesotho. Nchini Uganda, utawala wa kifashiti wa Idd Amin ndio kwanza ulikuwa umempindua Milton Obote, ukiungwa mkono na Uingereza. Marekani ilikuwa ikiendeleza vita Vietnam na kwingineko. Nelson Mandela alikuwa akitumikia kifungo cha maisha huko Afrika Kusini. Kwa ufupi, mabeberu na vibaraka wao walionekana kuwa na nguvu. Kwa Mwalimu, ubeberu na ukaburu haukuwa tofauti na wanyama wa kale ambao walishindwa kubadilika kuendana na mazingira katika safari ya mabadiliko ya viumbe (*evolution*). Aya hizi kuntu katika hotuba ya Mwalimu zinapaswa kunukuliwa kama zilivyo:

> *Binadamu amepita katika hatua nyingi tangu alipoanza safari yake ya kujitambua utu wake. Na mazingira yetu yanatuonyesha kwamba maisha*

[12]Julius K. Nyerere, *Binadamu na Maendeleo* (Dar es Salaam: Oxford University Press, 1974), 118.

*ya viumbe vyote hayaendelei namna ile ile. Masokwe, ambao wakati mmoja tulishabihiana sana, wamepita katika njia ya maendeleo iliyowakwamisha. Na wako viumbe wengine ambao sasa wametoweka: meno yao yalikua yakawa makubwa mno, au miili yao ilitokea kuwa mizito mno, hata wasiweze kuyakabili mazingira yaliyokuwa yanabadilika; wakafa wakamalizika! Mimi naamini kwamba katika historia ya maendeleo ya binadamu, mabeberu na wabaguzi wa rangi vile vile watatoweka. Sasa hivi wana maguvu mengi sana, lakini wanafanana sana na hili dudu - jiumbe la ovyo lililopotea njia. Tofauti iliyopo tu baina ya mabeberu na manyama haya ni kwamba meno na makucha ya mabeberu ni makali zaidi na yanaumiza zaidi. Hata sasa tunashuhudia unyama huko Vietnam. Lakini kushindwa kushirikiana ni dalili ya unyama; si tabia ya utu. Mabeberu na wabaguzi wa rangi watatoweka; Vorster na wenzake kama yeye watazuka na watatoweka. Kila beberu na mbaguzi wa rangi duniani ni mnyama wa aina fulani; na aina zote hizo za unyama hazina nafasi ya kudumu. Hatimaye zitatoweka! Afrika lazima ikatae kusukumwasukumwa na kunyonywa. Na kwa dhamiri hiyo hiyo lazima nasi tukatae kudharau, kunyonya na kusukumasukuma wengine. Hatuna budi kuonyesha dhamiri hiyo kwa vitendo, siyo kwa maneno matupu[13].*

[13]Kama hapo juu.

Nasi leo tunasema kwa kujiamini kuwa vuguvugu la haki-jiji, lilioenea duniani kote, litafanikiwa. Mifumo ya kale ya upangaji, uendelezaji na uendeshaji wa majiji inayowabagua, kuwapora na kuwajinaisha watu wa tabaka la chini ni mifumo mfu, iliyostawi katika dubwasha la kale: ubepari. Hata kama umejipaka poda na kujivika kilemba cha uliberali mamboleo, ubepari na ukatili wote unaouzalisha, havina nafasi ya kudumu. Watawala wote wanaoamini katika kuwatimua wavujajasho kutoka katika majiji nao pia watatoweka. Kama alivyosema Mwalimu, “tutasikia habari zao katika majumba ya makumbusho tu!” Tunarudia: vuguvugu la haki-jiji litafanikiwa!

**Dar es Salaam**
**Aprili 17, 2023**

## SURA YA 1

# Mfumo wa Ubepari na Athari Zake kwa Afrika

SABATHO NYAMSENDA & ABUNUWASI L. MWAMI

**Utangulizi**

Sura hii ya kwanza inatoa uchambuzi wa mfumo wa ubepari kwa kuainisha tabia zake na kuonyesha hatua ambazo umepitia. Athari ambazo kila hatua ya ubepari imesababisha kwa bara la Afrika zimeainishwa. Sura hii pia imeonyesha kuwa katika hatua na sura zake zote, ubepari umesababisha unyonyaji wa nguvu-kazi na rasilimali za Afrika ambao umestawisha nchi za

Magharibi na kuifukarisha Afrika. Vilevile, sura hii imefafanua namna ambavyo Waafrika wamekuwa wakipambana dhidi ya ubepari katika hatua na sura zake mbalimbali. Mapambano hayo, tangu enzi za Mkwawa hadi zama za Nyerere ni mapambano ya ukombozi. Katika zama za ubepari wa soko huria mapambano dhidi ya unyonyaji na uporaji hayajakoma, iwe ni kwa wakulima vijijini au wamachinga mijini.

## Ubepari na Tabia Zake

Ubepari ni mfumo wa uzalishaji mali unaoweka njia kuu za uzalishaji mali mikononi mwa tabaka la watu wachache, ambao ni mabepari, huku tabaka la walio wengi likiwa halina njia inayowawezesha kuishi isipokuwa kwa kuwatumikia mabepari. Njia kuu za uzalishaji mali ni kama vile mashamba makubwa, migodi mikubwa, benki kubwa, viwanda vikubwa, hoteli kubwa, biashara kubwa za usambazaji wa bidhaa, bandari, n.k. Kwa upande wa mijini, maeneo ya katikati ya jiji hujengwa, kumilikiwa na kutumiwa na mabepari huku wavujajasho wakiwa hawana mahali pa kujipatia riziki zao.

Ubepari una tabia kadhaa. Moja ya tabia hizo ni uwepo wa *matabaka baina ya watu ndani ya nchi*. Nchi ya kibepari ni nchi yenye matabaka yanayotokana na umiliki binafsi wa mali. Kwa upande mmoja, kuna tabaka la mabepari, ambao ni *wavunajasho* na kwa upande wa pili, kuna tabaka la wafanyakazi, ambao ni *wavujajasho*. Japokuwa mabepari hujitapa kuwa ni

watu wenye kufanya kazi kwa bidii, ukweli ni kwamba hawafanyi kazi wenyewe katika uzalishaji. Sehemu kubwa ya shughuli za uzalishaji na usambazaji hufanywa na wavujajasho. Kutokana na kuwa wamiliki wa njia kuu za uzalishaji mali, mabepari huwa na nguvu ya kuchopoa ziada iliyozalishwa na wavujajasho na kuifanya ya kwao.

Kwa uchambuzi wa kitabu hiki, wavujajasho wapo katika makundi mbalimbali kama vile wafanyakazi viwandani, vibarua mashambani na migodini, wakulima wadogo, wavuvi wadogo, bodaboda, wamachinga na wengineo wengi. Baadhi ya wavujajasho ni *wafanyakazi* ambao hawamiliki chochote zaidi ya uwezo wao wa kufanya kazi. Wengine, kama wakulima wadogo, wanamiliki vipande vya ardhi au vitendea kazi ambavyo huvitumia kuzalisha mazao, ambayo mwisho wa siku hulazimika kuyauza kwa mabepari kwa bei rahisi. Kwa ufupi, wavujajasho wote huvuja jasho katika uzalishaji au usambazaji wa bidhaa na huduma lakini wanaishia kuwa mafukara. Kwa kiasi kikubwa, faida inayochumwa kutokana na jasho lao huwafaidisha mabepari na kwa kiasi fulani wataalamu wa ngazi za juu na kati.

Katikati ya wavujajasho na wavunajasho lipo tabaka la kati - tabaka la wataalamu wa kada mbalimbali, kama wanasheria, wahadhiri, wahandisi, maaskari, walimu na wengineo ambao huajiriwa na kampuni au dola la kibepari ili kuutumikia mfumo wa ubepari. Wengi wa wataalamu hawa ni watumishi waaminifu

wa mfumo wa kibepari na wapo tayari kufanya jambo lolote ili mfumo huo uendelee kustawi. Hata hivyo, wapo wachache kati ya wataalam hawa ambao hutumia maarifa waliyo nayo kwa ajili ya kupigania maslahi ya wavujajasho.

Tabia ya pili, ni *uwepo wa matabaka baina ya nchi katika ngazi ya kidunia*. Mgawanyo wa kitabaka unazalisha makundi makuu mawili. Kwa upande mmoja kuna nchi za kibeberu na kwa upande wa pili kuna nchi za pembezoni. Nchi za kibeberu hujulikana pia kama nchi za Magharibi au nchi za Kaskazini. Kwa sehemu kubwa, uchumi wa nchi hizi umejengwa kupitia unyonyaji na uporaji wa nguvukazi na rasilimali za nchi za pembezoni. Uporaji huo ulianza mara baada ya makutaniko baina ya nchi za Ulaya na mabara mengine mwishoni mwa karne ya 15. Kwa Afrika, makutaniko hayo yamepitia vipindi tofauti tofauti vikiwemo biashara ya utumwa, ukoloni na baadaye ukoloni mamboleo ambao unaendelea hadi leo. Nchi za kibeberu zina maendeleo makubwa katika teknolojia, uzalishaji viwandani na hata katika silaha za kijeshi. Sehemu kubwa ya watu wake huishi maisha yasiyo ya dhiki. Nchi za pembezoni, licha ya kuwa na rasilimali nyingi, zina maendeleo duni katika mawanda ya teknolojia, silaha za kijeshi na hata uzalishaji viwandani. Rasilimali za nchi za pembezoni zimekuwa zikiporwa na nchi za kibeberu kwa karne na karne, jambo linalosababisha watu wa nchi za pembezoni kuishi maisha ya kifukara.

Tabia nyingine ya ubepari ni *matumizi ya dola kwa ajili ya kuendeleza unyonyaji na uporaji*. Dola la kibepari lina vyombo vya aina mbili: vyombo vya mabavu na vyombo vya ushawishi[14]. Vyombo vya mabavu ni kama mahakama, polisi, magareza, majeshi, mgambo, n.k. Hivi hutumia mabavu kwa ajili ya kuendeleza mahusiano ya kibepari. Vyombo vya ushawishi ni pamoja na taasisi za elimu, vyombo vya habari, taasisi za kiutamaduni na michezo, n.k. Ukichunguza kwa umakini kazi za vyombo hivi utagundua kuwa vinatumia ushawishi kwa ajili ya kuupigia chapuo ubepari. Chukulia mfano pale wafanyakazi wanapomgomea bepari kwa ajili ya kudai nyongeza ya mshahara. Dola hutuma askari kwa ajili ya kuwadhibiti wafanyakazi na wakati mwingine hata viongozi wa wafanyakazi hukamatwa. Wakati huo huo, vyombo vya habari hutoa matangazo na chambuzi zilizolenga kuwalaumu wafanyakazi pamoja na kupotosha malengo ya mgomo wao. Mfumo wa elimu, ambao unafundisha mtaala wa kuutukuza ubepari, umesukwa katika namna ambayo mwanafunzi anapohitimu anakuwa mtiifu kwa mnyonyaji wake.

Ukiachilia tabia tatu zilizotajwa hapo juu, tabia iliyo kuu, ambayo ndiyo moyo wa ubepari ni ulimbikizaji wa mtaji usio na kikomo. Ulimbikizaji hufanywa kwa njia mbili: njia ya uporaji, na njia ya unyonyaji.

---

[14] Luis Althusser, "Ideology and Ideological State Apparatuses (Notes towards an Investigation)," in *Lenin and Philosophy and Other Essays* (New York: Monthly Review Press, 1970).

*Ulimbikizaji kwa njia ya uporaji* hutokea pale ambapo mabepari hutegemea zaidi mabavu ya dola katika kupora rasilimali, utajiri na nguvukazi ya wavujajasho au nchi za Kusini na kuviweka katika mikono ya mabepari. Biashara ya utumwa, ukoloni na uporaji wa rasilimali kama ardhi, madini na mafuta unaofanywa na makampuni kutoka nchi za kibeberu katika nchi za pembezoni ni mifano michache ya ulimbikizaji wa kiporaji. Mfano mwingine ni pale kampuni inapotaka kutwaa eneo ambalo hutumiwa na wamachinga kuamua kutumia mabavu ya dola kuwafukuza wamachinga na kuwanyang'anya bidhaa zao.

*Ulimbikizaji kwa njia ya unyonyaji* hutokea pale ambapo bepari hutumia nguvu za soko, badala ya mabavu ya dola, katika kuwanyonya wavujajasho. Bepari humnyonya mvujajasho kwa kumpunja malipo ya nguvu kazi yake kupitia mishahara kiduchu au bei ndogo ya mazao yanayozalishwa na mvujajasho.

## Hatua za Ubepari

Ubepari haukuumbwa na Muumba. Ni mfumo ulioibuka baadaye sana katika historia ya mwanadamu. Kabla ya kuibuka kwa mfumo wa kibepari ilikuwepo mifumo mingine ya uzalishaji mali, ambayo ni ujima, utumwa na ukabaila. Mifumo hii ilidumu kwa karne nyingi kabla ya majilio ya ubepari. Hii inatukumbusha kuwa ubepari nao una mwisho wake kama mifumo mingine iliyoutangulia.

Tangu kuibuka kwake mwishoni mwa karne ya 15 huko barani Ulaya, mfumo wa ubepari umepitia hatua mbalimbali. Hapa chini tunazitaja na kuzichambua hatua hizo kwa ufupi, tukionyesha namna ambavyo mfumo wa ubepari ulikuwa ukijidhihirisha katika bara la Afrika katika kila hatua.

(1) *Ubepari wa Kibiashara*: Ubepari wa kibiashara ndio ulikuwa hatua ya mwanzo ya ubepari. Uliibuka mwishoni mwa karne ya 15 na kuendelea hadi katikati ya karne ya 18. Katika kipindi hicho, tabaka changa la mabepari kutoka Ulaya lilijitanua katika mabara mengine kama Afrika, Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini na Asia kwa ajili ya kulowea na kupora rasilimali zinazopatikana katika mabara hayo ili kuitajirisha Ulaya. Huko Amerika ya Kusini na Kasikazini, walowezi kutoka Ulaya waliendesha mauaji ya kimbari dhidi ya wenyeji wa mabara hayo na kisha kupora ardhi ambayo waliitumia kwa ajili ya kilimo na uchimbaji madini. Barani Afrika, mbali na kupora vipusa na madini ya thamani, wazungu waliendesha biashara ya utumwa ambayo ilihusisha uporaji wa watu weusi kutoka Afrika na kuwapeleka katika mabara ya Amerika ambako waliwageuza kuwa watumwa. Lengo la kuwageuza watu huru wa Afrika kuwa watumwa lilikuwa kuwatumikisha katika mashamba na migodi katika Bara la Amerika.

Ndani ya bara la Ulaya kwenyewe kulikuwa na uporaji wa ardhi kutoka kwa wakulima wadogo na kuiweka mikononi mwa wakulima wakubwa ambao hatimaye

walijigeuza na kuwa mabepari. Uporaji uliotokea katika kipindi cha ubepari wa kibiashara ulizalisha matabaka ya ndani katika nchi za Ulaya kutokana na mali kuwekwa mikononi mwa wachache dhidi ya mamilioni ya mafukara wasio na kitu. Matabaka mawili yalizaliwa: tabaka la mabepari ambao ndio waliomiliki njia kuu za kuzalisha mali kama vile ardhi na viwanda, na tabaka la wasiokuwa nacho ambao hawakuwa na namna nyingine ya kuishi isipokuwa kuuza nguvu-kazi yao kwa mabepari. Vilevile, yakazalishwa matabaka duniani kati ya nchi zinazopora na nchi zinazoporwa. Kwa upande mmoja kukawa na nchi tajiri, ambazo ni nchi za Ulaya, zilizotajirika kwa kupora rasilimali za nchi nyingine. Kwa upande wa pili, kukazaliwa nchi maskini ambazo ziliporwa na kutawaliwa na nchi za Ulaya. Afrika ikaangukia katika nchi maskini.

(2) *Ubepari wa Viwanda*: Kuanzia katikati ya karne ya 18, ubepari wa viwanda ulishamiri na uliendelea hadi mwishoni mwa karne ya 19. Ubepari wa viwanda ulitegemea uzalishaji wa bidhaa kupitia viwanda vikubwa ndani ya nchi. Viwanda hivyo vilimilikiwa na watu wachache ambao walikuwa katika tabaka la mabepari. Mabepari hao walikuwa wakishindana wao kwa wao katika kushusha bei na kuwekeza katika ugunduzi wa teknolojia ili kupata faida zaidi.

Lakini swali la kujiuliza ni: mabepari hao walipata wapi mtaji wao wa awali hata kupelekea kumiliki viwanda hivyo vikubwa? Jibu ni kwamba walipata mtaji kwa kupora rasilimali kama vile ardhi na

madini na kwa kutumia nguvukazi za Waafrika waliogeuzwa watumwa. Ndani ya viwanda hivyo walivyomiliki mabepari, siyo kwamba wao ndio waliokuwa wanazalisha mali hizo. Wazalishaji-mali walikuwa wafanyakazi. Mabepari, 'kazi' yao ilikuwa na inaendelea kuwa kunyonya tu.

(3) *Ubepari Hodhi*: Kuanzia mwishoni mwa karne ya 19 hadi leo hii, kuliibuka makampuni machache makubwa ya kibepari ambayo yalihodhi mfumo mzima wa uzalishaji-mali wa kibepari. Ushindani uliokuwa ukifanywa na mabepari katika kushusha bei na kuwekeza katika teknolojia mpya uliwaondoa baadhi ya mabepari katika shughuli za uzalishaji na kubakiza wachache ambao walihodhi mfumo mzima. Ukiachilia mbali ushindani baina ya mabepari, mapambano ya Waafrika yalikuwa kichocheo cha uibukaji wa ubepari hodhi. Waafrika waliogeuzwa watumwa walikuwa wakipambana kuuangusha utumwa, jambo lililolowalazimisha mabepari kuwekeza sana katika teknolojia kiasi kwamba wakawa hawahitaji tena nguvu-kazi ya watumwa na badala yake wakaamua kujitanua zaidi kwenye biashara kwa kutafuta vyanzo vya mali-ghafi na masoko nje ya Ulaya, hususan katika bara la Afrika. Hatua hiyo ya ubepari ambapo makampuni makubwa machache yamehodhi uchumi na kujitandaza duniani kote ndiyo hujulikana kama ubepari hodhi au ubeberu.

Katika bara la Afrika, ubepari hodhi umejidhihirisha kupitia sura mbili: sura ya ukoloni mkongwe na sura

ya ukoloni mambo leo, ambayo inaendelea hadi leo hii. Sura hizi mbili zimefafanuliwa hapa chini.

## Ukoloni Mkongwe

Wawakilishi wa nchi za Ulaya walikutana katika jiji la Berlin, Ujerumani mwishoni mwa mwaka 1884 hadi mwanzoni mwa 1885 kwa ajilli ya kuligawa bara la Afrika katika vipande vipande ambavyo vilifanywa makoloni ya nchi za Ulaya. Walipokuja Afrika, wakoloni walitumia mabavu ya kijeshi na mikataba ya kilaghai ili kukalia bara hili kwa ajili ya kupora rasilimali zake na kutweza utu wa watu wake. Mfano wa mikataba ya kilaghai ni ule unaosemekana kusainiwa kati ya Sultani Mangungo wa Msowero na Karl Peters, ambapo inadaiwa kuwa Mangungo alikubali kutoa ardhi yake yote, watu wake pamoja na vitu vyote vilivyomo ndani himaya yake ili viwe mali ya kampuni ya Karl Peters[15].

Makoloni ya Ulaya barani Afrika yalikuwa chanzo kikuu cha mali-ghafi kwa ajili ya kuhudumia viwanda vya Ulaya. Mali ghafi hizo zilipatikana kwa njia ya uporaji kwa kutumia mabavu pamoja na kupunja bei ya nguvu-kazi ya Waafrika viwandani, migodini na mashambani. Upunjaji huo ulijidhihirisha pia kupitia mazao ambayo Waafrika walilazimishwa kuyazalisha - mazao kama vile kahawa, pamba, chai, katani na kadhalika. Wakati huo huo, uwezo wa kiteknolojia

[15]Sabatho Nyamsenda na Amani Mhinda, *Mikataba ya Uwekezaji kati ya Nchi Mbili (MIUMBI) na Athari Zake kwa Tanzania* (Dar es Salaam: TATIC, 2022), 11-2.

wa Afrika kuzalisha mahitaji yake kama nguo na kadhalika uliharibiwa ili Afrika iwe soko la bidhaa zilizozalishwa katika viwanda vya Ulaya. Hali hii imepelekea utegemezi ambao umeendelea hadi hivi leo.

Ni vema kusisitiza kuwa Waafrika hawakukubali bara lao litawaliwe na kunyonywa na wageni na hivyo walipambana kwa kila hali kuukataa ukoloni. Mapambano hayo, yalianza tangu tu pale wakoloni walipotia mguu Afrika na yaliendelea hadi pale walipoondoka. Hapa chini tutatoa mifano michache ya mapambano yaliyoendeshwa na jamii zilizopatikana katika kipande cha Afrika kinachojulikana kama Tanzania.

*Mapambano ya Jamii ya Wahehe*

Mojawapo ya mifano ya mapambano ya Waafrika dhidi ya uvamizi wa wakoloni ni vita vya msituni vilivyoendeshwa na jamii ya Wahehe mkoani Iringa dhidi ya Wajerumani kuanzia mwaka wa 1891 hadi 1898. Katika pambano la mwaka 1891, jeshi la Wahehe likiongozwa na jemedari wake, Mtwa Mkwawa, lilionyesha ushujaa mkubwa kwa kuwapiga Wajerumani, na kuwauwa askari wao 300, akiwemo kamanda wao aliyeitwa Emily Von Zelewisky. Wahehe walitwaa silaha za Wajerumani, zikiwemo bunduki zaidi ya 300 pamoja na vifaru na mabomu. Wajerumani walisalimu amri na kukimbia kwa ajili ya kujipanga upya. Walirejea miaka mitatu baadaye na kuanzisha

upya mapigano, ambapo Mkwawa alikimbilia msituni na kuendesha vita vya msituni kwa miaka mitatu hadi pale alipozidiwa nguvu mwaka 1898. Licha ya kushinda vita hivyo, Wajerumani hawakufanikiwa kumkamata Mkwawa akiwa hai. Shujaa Mkwawa alijiondoa uhai wake ili kuondoa fedheha ya kukamatwa na manyang'au wa kikoloni akiwa hai[16].

*Mapambano ya Jamii ya Wayao*

Ushujaa kama wa Mtwa Mkwawa ulioelezewa hapo juu ulionyeshwa na Mfalme Machemba ambaye alikuwa ni mtawala wa jamii ya Wayao inayoishi Kusini mwa Tanzania. Mwaka 1890, Hermann von Wissmann, mwakilishi wa mabeberu wa Kijerumani, alimwamuru Machemba ajisalimishe ili himaya yake iwe koloni la Wajerumani. Machemba alimwandikia von Wissmann barua akimjibu:

> *Nimepokea amri yako, lakini sioni sababu ya kuitii. Bora nife kwanza kuliko kujisalimisha... Natafuta sababu kwa nini ninapaswa kukutii na sipati hata chembe ya sababu. Kama ungekuwa unataka urafiki, basi, ningekuwa tayari kuwa rafiki, leo na hata milele. Lakini siwezi kujishusha na kuwa mtawaliwa wako, hilo siwezi kukubali. Iwapo unataka vita, basi niko tayari, lakini sitakubali kukusujudia, kwa sababu wewe ni*

[16]Alison Redmayne, "Mkwawa and the Hehe Wars," *The Journal of African History* 9, No.3 (July 1968).

> *kiumbe wa Mungu kama nilivyo mimi. Mimi ni Mfalme katika himaya yangu, wewe pia ni mtawala katika himaya yako [huko unakotoka]. Mimi sikuamuru ufuate amri yangu, kwani najua kuwa wewe ni mtu huru. Kwa upande wangu sitakufuata, lakini kama unadhani unazo nguvu za kutosha, basi, njoo unikamate*[17].

Tangu alipotuma barua hiyo mwaka 1890, Machemba alipambana na Wajerumani kwa miaka 8 na mara zote aliibuka na ushindi katika uwanja wa vita. Kutokana na ushindi huo alikataa kulipa kodi kwa Wajerumani. Hatimaye, mwaka 1899, Wajerumani wakiwa wamejiimarisha zaidi, walimshinda Machemba, jambo lililomfanya shujaa huyo atoroke na kuhamia Msumbiji[18].

Hata baada ya kuwashinda Wahehe, Wayao na jamii nyingine za Afrika, wakoloni waliendelea kupata upinzani kutoka kwa Waafrika ambao ulijitokeza kwa njia mbali mbali. Kwa mfano, zipo jamii ambazo, baada ya kulazimishwa kulima mazao ya biashara, walipokea mbegu kutoka kwa wakoloni lakini walizichemsha kabla ya kwenda kuzipanda: mbegu hizo hazikuota. Hiyo pia ilikuwa mbinu ya kishujaa ya mapambano!

---

[17]Richard Hodder-Williams, *An Introduction to the Politics of Tropical Africa* (New York: Routledge, 1984), 22

[18]G.C.K. Gwasa, "The German Intervention and African Resistance in Tanzania," in *A History of Tanzania,* eds I.N. Kimambo and A.J. Temu (Nairobi: East African Publishing House, 1969), 113.

*Vita vya Ukombozi vya Maji Maji*

Kati ya mwaka 1905 hadi mwaka 1907, jamii za Kusini mwa Tanzania ziliendeleza mapambano dhidi ya Wajerumani ambayo yanafahamika kama Vita vya Maji Maji. Kiongozi wa Maji Maji aliyeitwa Kinjeketile Ngwale, alifanya jitihada kubwa sana kuunganisha jamii mbalimbali za Kusini kupambana dhidi ya udhalimu ya Wajerumani. Japokuwa Wajerumani walishinda vita hivyo, lakini walijikuta wakilazimika kufanya mageuzi madogo ili kuzuia vita vya aina hiyo visitokee tena. Mojawapo ya mageuzi hayo yalikuwa kupunguza uporaji wa ardhi pamoja na uonevu na ukatili waliokuwa wakiufanya dhidi ya Waafrika[19].

Baada ya Vita vya Kwanza vya Mabeberu (ambavyo kimakosa huwa vinaitwa Vita vya Kwanza vya Dunia), koloni la Tanganyika lilitwaliwa na kukaliwa na Waingereza. Katika kipindi hicho cha ukoloni wa Uingereza mapambano yaliendelea ambapo Waafrika waliunda vyombo mbalimbali vya kimapambano ikiwa ni pamoja na vyama vya wafanyakazi, vyama vya ushirika na vyama vya kijamii. Vyama vya wafanyakazi viliandaa migomo kupinga unyonyaji na mazingira mabaya ya kazi kwa wafanyakazi wa Kiafrika. Vyama vya ushirika vilipinga unyonyaji wa jasho la wakulima uliokuwa ukifanywa kwa kuwapunja bei ya mazao. Vyama vya kijamii, viliwaunganisha Waafrika katika

[19]C.S.L Chachage, "Socialist Ideology and the Reality of Tanzania" (Unpublished Ph.D. Thesis, Glasgow University, 1986), 50.

maeneo walimokuwa wakiishi ili kusaidiana kiuchumi na hasa katika nyakati za shida pamoja na kupinga ubaguzi wa rangi uliokuwa ukifanywa na wakoloni.

Kwa ujumla, utatu huu wa kimapambano ambao uliundwa na vyama vya ushirika, vyama vya wafanyakazi na vyama vya kijamii ndio ulikuwa ni msingi wa mapambano ya kudai uhuru chini ya chama cha Tanganyika African National Union (TANU). Na hatimaye, Tanganyika ikajinyakulia uhuru wake mwaka wa 1961!

## Ukoloni Mamboleo

Nchi nyingi za Afrika zilijipatia uhuru miaka ya 1960. Wakoloni walipoondoka walikabidhi madaraka kwa watawala wa Kiafrika lakini waliacha mfumo wa kiuchumi ambao uliwawezesha kuendelea kupora rasilimali za Afrika na kunyonya jasho la watu wa Afrika. Mfumo huo, unaoziwezesha nchi za kibeberu kuzinyonya nchi za Kiafrika - ikiwa ni pamoja na kupora rasilimali zake na kuamuru aina ya sera ambazo Afrika inapaswa kuzitekeleza -unajulikana kama ukoloni mamboleo[20].

Ukoloni mamboleo hutumia mbinu mbalimbali kama: biashara ya kinyonyaji ya kimataifa, mikopo na misaada, uporaji wa rasilimali za nchi za Kusini, sheria,

[20]Kwame Nkrumah, *Neo-Colonialism: The Last Stage of Imperialism* (New York: International Publishers, 1965).

mikataba na taasisi za kimataifa, uvamizi wa kijeshi, vikwazo vya kiuchumi kwa mataifa yanayopambana na ubeberu, fikra na mawazo yanayoabudu nchi za Magharibi, pamoja na serikali na watawala wanaotumiwa kwa maslahi ya nchi za Magharibi. Kwa kutumia njia hizi na nyingine, nchi za Magharibi zimeendelea kutajirika kwa kutumia rasilimali na jasho la watu wa nchi za Afrika huku Afrika ikiendelea kuwa maskini, tegemezi na ombaomba.

Katika nchi ya Tanzania, ukoloni mamboleo umepitia katika vipindi vikuu viwili: kipindi cha Azimio la Arusha na kipindi cha sera za soko huria. Ufafanuzi kuhusu vipindi hivi umetolewa hapa chini.

*Kipindi cha Azimio la Arusha*

Azimio la Arusha ni waraka uliopitishwa na chama cha TANU mwaka wa 1967 ukitoa mwongozo wa jinsi ya kujenga Tanzania mpya kwa misingi ya Ujamaa na Kujitegemea. Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha, hatua mbalimbali zilichukuliwa, zikiwemo zifuatazo:

(a) Njia kuu za uzalishaji-mali (kama vile viwanda vikubwa, benki kubwa, mashamba makubwa na kadhalika) zilitaifishwa na kuwekwa chini ya umiliki wa serikali. Awali, vyanzo hivyo vya utajiri vilikuwa vikimilikiwa na matajiri wachache kutoka nchi za Magharibi wakisaidiana na watu wenye asili

ya nchi za Asia.

(b) Kutoa huduma za kijamii (kama vile elimu na tiba) kwa watu wote bila malipo.

(c) Miiko ya Uongozi iliwazuia viongozi wa ngazi za juu na kati katika Chama na Serikali kutumia nafasi zao kujilimbikizia mali.

(d) Majaribio ya kujenga uchumi na jamii inayojitegemea kwa kujenga viwanda ili kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje.

(e) Kutoa ruzuku za pembejeo kwa wakulima wadogo vijijini na ruzuku za chakula kwa wakazi wa mijini.

(f) Kulinda na kupigania heshima, hadhi na utu wa Mwafrika pamoja na binadamu wengine wanaokandamizwa popote pale duniani.

Kwa ufupi, Azimio la Arusha lilikuwa dira ya kujenga jamii inayozingatia misingi ya utu, haki na usawa. Na pia, lililenga kuiondoa Tanzania kutoka kwenye makucha ya ukoloni mamboleo. Ndiyo maana, watu wa tabaka la chini, hususan wakulima wadogo, wafugaji wadogo na wafanyakazi, waliandamana nchi nzima kuliunga mkono Azimio la Arusha.

Hata hivyo, malengo mema yaliyowekwa na Azimio hayakuweza kudumu kwani nchi za Magharibi, kwa kushirikiana na vibaraka wao wa ndani, walilihujumu na kufanikiwa kulipindua baada ya Mwalimu Nyerere kuondoka madarakani mwaka wa 1985.

*Kipindi cha Soko Huria*

Sera za Soko Huria zililetwa kwa ajili ya kukomaza na kuimarisha ubepari hodhi kwa kuondoa faida, nguvu, na mamlaka kutoka katika mikono ya tabaka la wavujajasho na nchi za pembezoni na kuviweka katika mikono ya tabaka la mabepari na nchi za kibeberu. Nchini Tanzania, kipindi cha soko huria kilianza baada ya Nyerere kuondoka madarakani mwaka 1985 na kimeendelea hadi leo.

Baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika kipindi cha soko huria ni pamoja na:

> (a) Njia kuu za uzalishaji-mali (kama vile viwanda vikubwa, mabenki makubwa, n.k) zilibinafsishwa na kuwekwa chini ya umiliki wa watu binafsi. Vyanzo hivyo vya utajiri vilivyokuwa mikononi mwa serikali wakati wa Azimio la Arusha viliondolewa na kuwekwa mikononi mwa watu binafsi, wengi wao wakiwa ni wawekezaji kutoka ughaibuni na warasimu kutoka serikalini.

(b) Huduma za kijamii (elimu, tiba, n.k) ziligeuzwa kuwa bidhaa na kuuzwa kwa watu wenye uwezo wa kifedha wa kuzinunua.

(c) Kuondolewa kwa miiko ya uongozi ambako kuliwaruhusu viongozi kutumia nafasi zao kujilimbikizia mali. Hatua hii ilizalisha ufisadi wa kupindukia.

(d) Kuondolewa kwa ruzuku za pembejeo kwa wakulima vijijini na ruzuku ya chakula kwa wakazi wa mijini. Hatua hii iliongeza uduni wa hali ya maisha ya watu wa tabaka la chini.

(e) Kuongezeka kwa utegemezi wa bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi baada ya viwanda vilivyobinafsishwa kufungwa na kugeuzwa kuwa maghala.

(f) Kukua kwa pengo kati ya walionacho na wasiokuwa nacho kutokana na serikali kuwatumikia watu wenye pesa na kuwatelekeza wasio na pesa.

(g) Kushushwa kwa heshima, hadhi na utu wa Mwafrika kutokana na viongozi wa Kiafrika kuwasujudia mabeberu.

(h) Kuongezeka kwa uporaji wa rasilimali za Afrika unaofanywa na makampuni kutoka nje.

(i) Kutoweka kwa ajira za kudumu na zenye staha na kuongezeka kwa ajira zenye sura ya kibarua, zisizo na malipo ya staha na zenye mazingira magumu ya kazi.

Kwa ufupi, mabadiliko kutoka sera za kijamaa chini ya Azimio la Arusha kwenda kwenye sera za soko huria, yalikuwa ni mabadiliko ya kuimarisha ukoloni mamboleo. Iwapo Azimio la Arusha lililenga kulinda maslahi ya watu wa tabaka la chini, basi sera za soko huria zinalenga kulinda maslahi ya wenye pesa. Iwapo Azimio la Arusha lililenga kujenga uchumi na jamii inayojitegemea, basi sera za soko huria zinalenga kujenga utegemezi kwa mataifa ya nje.

Jambo moja ambalo sharti lisemwe ni kuwa, kama ilivyokuwa kwa bibi na babu zao nyakati za utumwa na ukoloni, watu wa tabaka la chini ambao ndio waathirika wa sera za soko huria wamekuwa wakipambana dhidi ya sera hizo. Na mifano ya mapambano hayo ni wafanyakazi wa mashirika ya umma kugomea ubinafsishwaji wa mashirika hayo; wakulima kupambana kurejeshewa ardhi iliyoporwa na inayoendelea kuporwa na wawekezaji; jamii za wafugaji (kama vile Wamasai wa Ngorongoro) kupambana dhidi ya uporaji wa ardhi yao; wanafunzi wa vyuo vikuu kupambana dhidi ya sera zinazogeuza elimu kuwa bidhaa; mapambano ya wafanyakazi dhidi ya ujira mdogo, mazingira hatarishi ya kazi na unyanyasaji katika maeneo ya kazi; na mapambano ya wamachinga wanaopigania haki yao kujipatia kipato

katikati ya jiji. Haya yote ni sehemu ya mapambano ya ukombozi.

## Hitimisho

Sura hii imejadili hatua mbalimbali ambazo mfumo wa ubepari umepitia. Hatua ya kwanza ni ubepari wa kibiashara ambao ulijitokeza katika Afrika kwa sura ya biashara ya utumwa. Hatua ya pili ni ubepari wa viwanda ambao ulizalisha mahitaji ya ukoloni kwa ajili ya kujipatia mali-ghafi kutoka Afrika na soko la Afrika kwa ajili ya kuuza bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya Ulaya. Hatua ya tatu ni ubepari hodhi ambao katika Afrika ulijitokeza katika sura ya ukoloni na baadaye ukoloni mamboleo.

Sura hii imeonyesha kwamba, ukoloni mamboleo pia umepitia vipindi viwili. Kipindi cha kwanza kikiwa ni kipindi cha Azimio la Arusha na cha pili kikiwa ni kipindi cha soko huria. Hivi sasa tuko katika kipindi cha soko huria. Pamoja na kuonyesha namna ambavyo Waafrika walionewa, kunyonywa na kuporwa katika hatua mbalimbali za ubepari, sura hii pia imeeleza ni kwa namna gani ambavyo wamekuwa wakipambana ili kuondoa udhalimu huo. Mapambano hayo yanaendelea hadi leo hii ambapo wavujajasho wa Kiafrika wamekuwa wakipambana dhidi ya sera dhalimu za soko huria[21].

[21]Sabatho Nyamsenda, *Wavujajasho dhidi ya Soko Huria: Uzoefu, Mapambano na Dira Mbadala* (Dar es Salaam: Rosa Luxemburg Stiftung, 2019).



Askari wa Jiji (mgambo) wakiwapora wamachinga bidhaa zao katika eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam tarehe 28 Juni 2013. Hata hivyo, kama inavyoonekana katika picha hapo juu, wamachinga hao, wakiongozwa na wanawake, walipambana ili kuzuia bidhaa zao zisichukuliwe na askari mgambo.

## SURA YA 2

# Wamachinga Ndani ya Mfumo wa Ubepari

SABATHO NYAMSENDA & ABUNUWASI L. MWAMI

**Utangulizi**

Sura hii inawaangazia wamachinga ndani ya mfumo na jiji la kibepari. Inaanza kwa kutoa maana ya mmachinga na sababu za kuibuka kwa umachinga na kuonyesha ni jinsi gani mikanganyiko na mabadiliko katika mfumo wa ubepari vimepelekea uibukaji wa kundi kubwa la watu wasiokuwa na ajira, ambao

hawana namna ya kuishi zaidi ya kujitafutia riziki katika kiitwacho sekta isiyo rasmi. Sura hii pia imechambua historia ya majiji, ikilitazama jiji la Dar es Salaam na namna lilivyosukwa kwa misingi ya ubaguzi wa rangi na wa kitabaka. Hata baada ya ukoloni kuangushwa na ubaguzi wa rangi kukomeshwa, ubaguzi wa kitabaka uliendelea kutamalaki, ukijidhihirisha kupitia mabavu yaliyokuwa yakitumika kuwaondoa wavujajasho kutoka katika maeneo ya katikati ya jiji. Kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa katika sura hii, ujio wa sera za soko huria na dira yake ya ujenzi wa jiji la viwango vya kimataifa umechochea zaidi ubaguzi wa kitabaka huku wamachinga, kama sehemu ya wavujajasho, wakiwa miongoni mwa waathirika wakuu wa ubaguzi huo. Sura hii pia imepaza sauti ya wamachinga juu ya aina gani ya jiji wanalolitaka - jiji ambamo wana haki ya kuyafikia na kuyatumia maeneo yaliyo na mzunguko mkubwa wa watu kwa ajili ya kujipatia riziki zao.

## Mmachinga ni Nani?

Wamachinga ni msamiati unaotumika kutaja kundi la watu wasio na ajira rasmi ambao huuza bidhaa za aina mbalimbali kwa kuzitembeza ili kutafuta wateja au kuzipanga mahali palipo na mzunguko mkubwa wa watu. Mara nyingi bidhaa zinazouzwa na wamachinga huwa ni za bei rahisi na hupatikana kwa rejareja na katika maeneo yanayofikika kirahisi kwa mteja. Kwa hiyo, sekta ya umachinga hutoa huduma muhimu sana kwa jamii ya tabaka la chini katika maeneo ya

mijini na imekuwa chanzo cha maisha kwa kundi kubwa la vijana wasio na ajira. Kwa kuwa uchumi tulio nao ni uchumi wa kibepari, basi umachinga ni shughuli muhimu sana katika mfumo wa uzalishaji-mali wa kibepari kwani uzalishaji wa bidhaa huwa unategemea uuzaji wake.

Kumekuwa na hadaa zinazofanywa na mabepari na mawakala wao kujaribu kuwaaminisha wamachinga kuwa wao ni mabepari watarajiwa (*wajasiriamali)*. Lengo la hadaa hizi ni kumfanya kijana anaetembeza malai (*ice cream*) kwa miguu au baiskeli ajione sawa na bepari anaemiliki viwanda vya kutengeneza *ice cream*. Na kwa kuwa matajiri wengi wa Tanzania wamekuwa wakijinadi kuwa walianza biashara kama wamachinga wa kuuza kalamu au maandazi - jambo ambalo ni uzushi wa mchana - basi kijana mtembeza ice cream huambiwa awe mvumilivu na afanye kazi kwa kujituma bila kulalamika ili nae aweze 'kutoboa'. "Hata mbuyu ulianza kama mchicha," wazungumzaji-wahamasishaji (*motivational speakers*) humwambia kijana huyo.

Mfikirie mmachinga huyo, anayetembea karibuni zaidi ya kilometa 50 kwa siku kutafuta wateja, begani akiwa amebeba kasha la kutunza ubaridi lililojaa *ice cream* za ukwaju. Akirudi nyumbani baada ya kupigwa na jua kutwa nzima anakuwa kajaaa vumbi. Kachoka chakari. Ana njaa, hata pesa ya kula mlo wa usiku hana. Yawezekana kodi ya chumba anachoishi imeisha na hawezi kulipa. Pengine hata nyumba anayoishi

ipo eneo la bondeni lisilo na huduma za msingi na linalokumbwa na tishio la bomoa bomoa ya serikali au dhahma za mafuriko.

Kila kijana huyo anapouza *ice cream*, sehemu kubwa ya faida huenda kwa bepari anaemiliki kiwanda. Wakati kijana akipanda daladala na kutembea kwa miguu, bepari anakuwa kastarehe ofisini akipigwa na kiyoyozi au akipanda ndege kwenda mapumzikoni ughaibuni. Mmachinga huyo anaposhinda njaa na hata kupata maradhi ya vidonda vya tumbo, bepari hula na kusaza, tena chakula akipendacho, kilichoandaliwa na wapishi wenye viwango vya kimataifa nyumbani kwake au katika hoteli yenye hadhi ya nyota tano. Na akijisikia kuchoka anaweza kukodi ndege kwenda mapumzikoni katika mbuga za wanyama nchini au nje ya nchi.

Wazungumzaji-wahamasishaji wanaomtaka mmachinga kujiona kama bepari mtarajiwa wanakuwa na malengo mawili. Lengo la kwanza ni kuficha mbinu chafu na za kikatili zilizotumiwa na mabepari kwa ajili ya kujipatia utajiri wao. Hata hivyo, upo ushahidi wa wazi kuwa sehemu kubwa ya mabepari wa Tanzania walilimbikiza mtaji wa awali kwa kufilisi na kujibinafsishia mashirika ya umma, kupora ardhi ya wanavijiji, kukwepa kodi na kukwapua fedha za serikali kupitia miradi hewa au ya kifisadi.

Lengo la pili ni kuficha mahusiano ya kinyonyaji yaliyopo kati ya mmachinga anayeuza *ice cream* na

bepari anayemiliki kiwanda kinachozitengeneza. Lakini, kama tulivyofafanua hapo juu, bepari anaemiliki kiwanda cha kutengeneza *ice cream* ndiye anayefaidika na nguvu kazi ya kijana huyo. Kwa hiyo, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ufukara wa mmachinga huyo na utajiri wa bepari huyo. Ni sharti mmachinga huyo na wavujajasho wenzake katika mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa wawe maskini ili bepari huyo awe tajiri.

Kwa hiyo, wapiga zumari wa kibepari wanaotaka mmachinga muuza *ice cream* apige kazi bila kulalamika wana lengo la kumhadaa ili asihoji chanzo cha ufukara wake. Kwa kutumia hadaa hizo, wanataka kutengeneza uhusiano usio na mikwaruzo kati ya mtu anayevuja jasho na yule anayevuna jasho ili kuepuka mapambano ya kitabaka.

> *Hii ni sawa na kudhani kuwa simba na mbuzi wanaweza kuwekwa katika zizi moja au papa na samaki mdogo katika bahari moja bila ya simba kumla mbuzi au papa kummeza samaki mdogo. Mtu mwenye udhani huo basi ana nakisi ya uelewa wa tabia za asili za wanyama wa mwituni na majini au ana nia ya kumrahisishia simba/papa kazi ya kupata mlo. Kwa vyovyote vile, kuwafungia simba na mbuzi katika banda moja hakuwezi kuwa kumefanyika kwa maslahi ya mbuzi. Mnufaikaji wa mwisho atakuwa simba. Vivyo hivyo kwa matabaka yenye maslahi kinzani. Ni hulka ya mabepari (wafanyabiashara*

> *wakubwa) kuwanyonya, kuwapora na hata kuwaua wafanyakazi pamoja na wazalishaji wadogo. Kufikiria kujenga uhusiano mwema kati ya matabaka hayo ni kielelezo cha upunguani wa historia ya mapambano ya kitabaka au ni mkakati wa kuwahadaa wavujajasho kwa makusudi ili wawe "kitoweo" cha mabepari*[22] *.*

Upo upofu mwingine wa kinadharia katika mtazamo unaowaona wamachinga kama wajasiriamali/mabepari. Upofu huo unatokana na kutengeneza utengano kati mchakato wa uzalishaji-mali na ule wa usambazaji-mali. Utenganisho huo hufanyika kimakosa kwani michakato hiyo miwili huwa imefungamana na kwa maana hiyo haipaswi kutenganishwa. Mfumo wa ubepari unategemea uzalishaji wa bidhaa ili kuzalisha thamani-ziada (*surplus value*). Uzalishaji wa thamani-ziada hauwezi ukafanikishwa bila kuziuza bidhaa hizo zinazozalishwa. Na katika michakato yote miwili - uzalishaji na usambazaji - kuna wavujajasho ambao ndio uti wa mgongo. Viwandani, kwenye uzalishaji, kuna wafanyakazi. Mitaani, kwenye usambazaji, kuna wamachinga! Wote ni wavujajasho na wote ni wahanga wa mfumo kandamizi wa kibepari.

Kwa hiyo, katika kitabu hiki mmachinga anahesabiwa kama mvujajasho. Japokuwa wapo mabepari uchwara wachache waliojificha katika kivuli cha umachinga

[22] Sabatho Nyamsenda, "Warasimu Wanamhujumu Magufuli?" *Raia Mwema*, December 23, 2015.

kwa minajili ya kukwepa kodi na kunyonya nguvu kazi ya wamachinga, jambo hilo haliwezi kutufanya tukaushe bwawa zima (la umachinga) kwa lengo la kumkamata samaki mmoja (bepari aliyejifanya mmachinga). Sehemu kubwa ya wamachinga ni mafukara wa mijini (*urban poor*) wanaovuja jasho ili kujikimu na, kwa kufanya hivyo, wanaufaidisha mfumo wa ubepari. Kwa mantiki hiyo, maslahi ya wamachinga ni sawa na yale ya wavujajasho wengine kama wakulima wadogo, wavuvi wadogo, wafugaji wadogo, wasusi, mama lishe, madereva bodaboda, madereva bajaji, wafanya usafi, wahudumu wa migahawa, n.k.

Pili, kwa kuwa wanaangukia katika kundi la wavujajasho, wamachinga wengi wamekuwa ni waathirika wa vita vya kitabaka vinavyoendeshwa na wavunajasho na wapambe wao dhidi ya wavujajasho. Mojawapo ya vitu vinavyodhihirisha vita hivyo vya kitabaka ni timua timua ya wamachinga inayofanywa na warasimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa maeneo ya katikati ya jiji yanakuwa stahiki ya watu wa tabaka la juu peke yao. Timua timua hii itokeayo jijini haitofautiani na uporaji wa ardhi kwa kutumia mabavu unaofanywa na mamlaka za dola au wawekezaji uchwara katika maeneo ya vijijini na hivyo kusababisha makundi makubwa ya wazalishaji wa msingi vijijini (wakulima na wafugaji) kubaki bila ardhi. Uporaji huo hutokea pia katika maeneo ya vyanzo vya maji ambapo mabavu yamekuwa yakitumika kuzuia shughuli za wavuvi wadogo. Kwa mantiki hiyo, wamachinga hawana budi

kuungana wao kwa wao na pia kuunganisha nguvu na wavujajasho wengine mijini na vijijini ili waweze kupigania haki zao.

## Uibukaji wa Umachinga

Uwepo wa watu wasio na ajira, ambao ama hugeuka ombaomba au hujitafutia kipato kupitia uchuuzi wa bidhaa, sio jambo jipya katika mfumo wa ubepari. Mfumo wa ubepari una tabia ya kujikita zaidi katika uboreshaji wa teknolojia ili kuifanya mitambo ichukue nafasi ya binadamu katika uzalishaji. Lengo la kufanya hivi ni kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya faida inakwenda kwa bepari badala ya wafanyakazi, ambao nafasi yao inakuwa imechukuliwa na mitambo. Kwa maana hiyo, kunatengenezeka kundi kubwa la watu wasio na ajira ambao huishi maisha ya kifukara. Kundi hilo la watu waliotemwa katika mfumo huwa ni jeshi la akiba la nguvu kazi (*industrial reserve army)* kwa maana ya kwamba uwepo wao husaidia mishahara ya wafanyakazi kuwa chini[23]. Nyakati ambazo mabepari wanahitaji wafanyakazi wanaolipwa ujira kiduchu basi huwapata katika jeshi hilo la akiba na nyakati ambazo hawawahitaji basi huwaondoa kazini. Kwa hiyo, kwa asili yake, ubepari hutengeneza tabaka la mafukara. Mafukara hawa hujikimu kwa kufanya kazi za uchuuzi, uendeshaji wa bodaboda, ombaomba, upigaji debe, uokotaji makopo, ubebaji mizigo, kazi za vibarua, n.k.

[23]Karl Marx, *Mtaji: Tahakiki ya Siasa-Uchumi*, Juz. 1. Taf. ya Abunuwasi L. Mwami (Rasimu ya Tano, 2016).

Kwa upande wa Tanzania, mafukara wa mijini waliongezeka sana baada ya nchi kuhama kutoka sera za ujamaa kwenda kwenye sera za soko huria. Wakati wa sera za ujamaa chini ya utawala wa Mwalimu Nyerere, ufukara kwa wakazi wa mijini haukuwa mkubwa na idadi ya mafukara pia ilikuwa ni ndogo. Hii ilitokana na sababu kadhaa. Kwanza, kama ilivyofafanuliwa katika sura iliyopita, kupitia sera ya kujitegemea, serikali ya Mwalimu Nyerere iliwekeza katika ujenzi wa viwanda na kwa hiyo iliongeza wigo wa ajira. Pili, ilitanua huduma za kijamii ambazo zilitolewa kama haki kwa wote.

Baada ya Mwalimu Nyerere kuondoka madarakani, serikali ya Rais Mwinyi iliamua kukubaliana na masharti ya kurekebisha uchumi ambayo nchi za Magharibi na mashirika ya fedha ya kimataifa yalikuwa yakilazimisha nchi za Kusini ziyafuate.

Mojawapo ya masharti ya sera za soko huria ni kuiondoa serikali katika uchumi na kubinafsisha njia kuu za uzalishaji mali. Sera ya ubinafsishaji ilipotekelezwa nchini Tanzania ilileta madhara makubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu pamoja na tabaka la wafanyakazi. Sehemu kubwa ya viwanda vilivyobinafsishwa vilifungwa na kugeuzwa maghala kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa kutoka nje. Kufungwa kwa viwanda kulisababisha wafanyakazi wengi kupoteza ajira zao na wakahama toka wafanyakazi waliokuwa wakizalisha bidhaa viwandani hadi wamachinga wa kutembeza bidhaa kutoka nje. Rais wa awamu

ya tatu, Benjamin William Mkapa, ambaye alipigia chapuo sera ya ubinafishaji, alionyesha masikitiko makubwa sana kuhusu sera hiyo baada ya kuondoka madarakani. Kwa maneno yake, akimjibu mwandishi Roberto Savio katika mahojiano yaliyochapishwa na gazeti la *Business Mirror* mwaka 2009, Mkapa alikiri kuwa Mashirika ya Fedha ya Kimataifa na nchi za Magharibi yalikuwa yamempatia kitanzi, naye, kwa uaminifu mkubwa, akakitumia kuunyonga uchumi aliokabidhiwa dhamana ya kuufufua:

> *Tulibinafsisha kila kitu kilichokuwa mikononi mwa dola. Kila kitu kilinunuliwa na wawekezaji kutoka nje kwa sababu hatukuwa na mtaji wa ndani wenye uwezo wa kushindana. Makampuni ya nje yakafunga mashirika ya ndani kwa sababu hayakuwa na tija na yakayageuza mashirika haya kuwa wachuuzi wa bidhaa kutoka nje na kwa hivyo kuongeza watu wasio na ajira. Wataalam wa Benki ya Dunia na Shirika la Kitamataifa la Fedha walitabiri kwamba hivyo ndivyo ingekuwa, lakini wakatuambia: Uwekezaji kutoka nje utazaa taasisi za kibiashara za kisasa, zenye uwezo wa kushindana, na teknolojia ya kisasa, na kwa hivyo kujenga misingi ya kudumu ya maendeleo ya kisasa. Hakuna lolote kati ya hayo lililotokea nchini mwetu[24].*

[24] Issa Shivji, *Insha za Mapambano ya Wanyonge* (Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, 2012), 266-7.

Baada ya kuua uzalishaji wa viwandani, sera za soko huria zilirejesha uchumi wa nchi yetu katika misingi ya kikoloni ambapo uchumi ulijikita katika kusafirisha malighafi kwenda nje na kuagiza bidhaa za viwandani zilizozalishwa nje. Uchumi wa aina hiyo ni uchumi uchwara. Mbali na kuwa tegemezi kwa mataifa ya nje, uchumi uchwara una sifa ya kutokuwa na uwezo wa kutengeneza ajira za staha. Kwa kusafirisha malighafi kwenda nje, uchumi uchwara husafirisha pia ajira nyingi ambazo zingetengenezwa kupitia uchakataji wa malighafi hizo katika viwanda vya ndani. Hii ni kusema kuwa uchumi uchwara husafirisha ajira kwenda nchi za ughaibuni katika mfumo wa malighafi na kuagiza umaskini katika mfumo wa bidhaa zilizozalishwa nje. Vijana wa nchi yetu ambao wangeajiriwa viwandani wanabaki kuwa wachuuzi wa bidhaa zilizozalishwa nje.

Sera za soko huria hazikuathiri sekta ya viwanda peke yake bali hata kilimo na maendeleo vijijini. Tukumbuke kuwa serikali ya Mwalimu Nyerere ilikuwa imeweka msisitizo mkubwa katika maendeleo ya vijijini, ikiwemo kutoa ruzuku za pembejeo kwa wazalishaji vijijini, kujenga miundombinu, kutanua huduma za kijamii bila malipo na kulinda bei za mazao. Japo kulikuwa na kasoro kadhaa katika utekelezaji wake, hatua hizi zilisaidia sana kupunguza ufukara vijijini. Baada ya Mwalimu kuondoka madarakani, awamu zilizofuatia ziliamriwa na 'wakubwa wa dunia' kuachana na utoaji ruzuku kwa wakulima na kuachana na maendeleo vijijini. Serikali ikatelekeza

kilimo kwa kuwaacha wakulima 'solemba' ndani ya lindi la ufukara na dhuluma za walanguzi. Wakulima walipunjwa bei ya mazao bila serikali kuingilia kati kusimamia maslahi yao.

Mbaya zaidi, kuliibuka wimbi kubwa la uporaji wa ardhi inayotumiwa na wazalishaji vijijini kwa shughuli za kilimo na ufugaji. Ikawa ni kawaida kuona wanavijiji wakibomolewa makazi yao, mifugo yao kupigwa mnada na mazao yao kuchomwa moto ili kuwaondoa katika ardhi waliyokuwa wakiitumia katika uzalishaji. Katika maeneo yenye vyanzo vya maji, wavuvi walichomewa nyavu zao, kukamatwa na hata kufungwa wakidaiwa kufanya 'uvuvi haramu'. Hali ilikuwa mbaya zaidi katika maeneo ya migodini ambako wachimbaji wadogo ambao ndio waliovumbua madini katika migodi hiyo waliondolewa kwa nguvu ili kupisha kampuni kubwa za wawekezaji kutoka ughaibuni. Kwa mfano, mgodi wa Bulyanhulu, ambao ulivumbuliwa na wachimbaji wadogo mwaka 1975 ulikuwa na wachimbaji wadogo zaidi ya laki tatu kufikia katikati ya miaka ya 1990. Mwaka 1996, wachimbaji hao wote walitimuliwa kwa nguvu ili kupisha kampuni ya uwekezaji kutoka ughaibuni iliyoitwa Sutton Resources ambayo baadae ilinunuliwa na Barrick Gold. Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti uliofanywa na Brian Cooksey, katika purukushani za kuwatimua, wachimbaji wadogo wapatao 54 wanasemekana kufukiwa katika mashimo ya migodi wakiwa hai![25]

[25]Brian Cooksey, *The Investment and Business Environment for Gold Exploration and Mining in Tanzania* (London: Overseas Development Institute, 2011).

Mifano yote iliyotolewa hapo juu inatuonyesha kuwa sera za soko huria ziliongeza ufukara na dhiki katika maeneo ya vijijini, hali iliyowasukuma vijana kukimbilia mijini kwa matumaini ya kupata ajira zitakazowaletea unafuu wa maisha. Hata hivyo, walipofika mijini ajira rasmi hazikuwepo kutokana na viwanda kufungwa na kugeuzwa maghala. Vijana hao wakawa hawana namna zaidi ya kufanya biashara ya kutembeza bidhaa katika kona mbalimbali za jiji kwa lengo la kutafuta wateja.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, sehemu kubwa ya wamachinga walikuwa vijana kutoka mikoa ya Kusini, hasa Mtwara na Lindi, waliokimbilia jijini Dar es Salaam na viunga vyake kwa ajili ya kujitafutia maisha. Kwa kadiri utekelezaji wa sera za soko ulivyoendelea kusababisha hali mbaya ya maisha nchini kote ndivyo vijana kutoka sehemu zote za Tanzania walivyoendelea kumiminika mijini na kujihusisha na umachinga. Mwanzoni kabisa, vijana hawa walijihusisha zaidi na uchuuzi wa nguo za mitumba ambao ni matokeo ya ubinafsishaji wa viwanda vya nguo uliofanywa na watawala baada ya kulitungua Azimio la Arusha katikati ya miaka ya 1980 na kukumbatia sera za kiporaji za soko huria. Sekta hii isiyokuwa rasmi iliendelea kukua na kuhusisha wanajumuiya wengine wa tabaka la wavujajasho kama vile vinyozi, mama lishe, na hatimaye bodaboda, madereva, na wengine kadha wa kadha kama ilivyo sasa hivi.

Leo hii, kazi ya umachinga siyo tena shughuli za mafukara kama ilivyokuwa hapo awali; badala yake, shughuli hizi zimeenea hadi kuwakumba wanajumuiya wa tabaka la wasomi wenye ajira na wasio na ajira. Kutokana na mishahara kuwa midogo kiasi cha kutokidhi mahitaji ya familia, wasomi walioajiriwa huwa na kawaida ya kuongeza kipato chao kwa kufanya shughuli moja au mbili zaidi ya ile kazi yao iliyo rasmi. Kwa wasomi wasio na ajira, umachinga umekuwa ndiyo ajira pekee ya kuwapatia kipato. Kama tulivyofafanua hapo awali, uchumi uchwara wa nchi yetu hauzalishi ajira za kutosha, jambo linalowafanya wengi wa vijana wanaohitimu katika ngazi mbalimbali za elimu kuingia katika sekta isiyo rasmi. Inakadiriwa kuwa kati ya wahitimu milioni 1 wanaoingia katika soko la ajira kila mwaka, ni wahitimu elfu 40 tu ndio wanaopata ajira katika sekta iliyo rasmi. Wengine wote huangukia katika kilimo au shughuli za sekta isiyo rasmi katika majiji kama kutembeza bidhaa mitaani, mama/baba lishe, kuuza genge, bodaboda, ususi, udalali, ujenzi, ufundi makanika, ufagizi maofisini na barabarani, ushonaji cherehani, n.k.

## Wakimbizi Ndani ya Nchi Yao

Katika miji na majiji hapa Tanzania na katika nchi nyingine duniani, wamachinga, na watu wengine wa tabaka la chini, wamekuwa wakiishi kwa mateso makubwa. Mamlaka za miji na majiji zimekuwa zikitumia vyombo vya mabavu, hasa askari wa jiji

(mgambo), kuendesha mazoezi ya timua timua ya wamachinga. Wamachinga wamekuwa wakisumbuliwa kwa kufanyiwa ghasia na kuondolewa kwa nguvu kutoka katika maeneo ya katikati ya jiji na kuhamishiwa pembezoni. Katika timua timua hizo, vibanda vyao huharibiwa, bidhaa zao huchukuliwa kwa nguvu, na miili yao hugeuka uwanja wa kujaribia virungu vya mgambo na risasi za askari. Hali hii imetweza utu wa wamachinga na kuwarudisha nyuma kiuchumi. Mmachinga mmoja, akisimulia manyanyaso anayokumbana nayo alisema kwa masikitiko: "Mara kadhaa nimeshakamatwa na mgambo wa jiji ambao wananinyang'anya bidhaa zangu na hata pesa. Hii imenifanya niishi katika jiji hili kama mkimbizi ndani ya nchi yangu."[26] Mwingine alisema: "Sitaki kukumbuka mambo tunayofanyiwa na serikali yetu. Inawachukulia wamachinga kama wakimbizi - matokeo yake, biashara zao zinaharibiwa." [27]

Ili kuelewa chanzo cha madhila haya, hatuna budi kudadisi namna majiji yetu yalivyosukwa. Japo Afrika imekuwa na majiji kwa karne nyingi kabla ya majilio ya ukoloni, sehemu kubwa ya majiji hayo yaliangushwa na hata kuharibiwa na Wazungu pale walipokuja Afrika na kuanza kupora watu na rasilimali za Afrika kupitia biashara ya utumwa na baadaye ukoloni[28].

[26]A. Brown, C. Msoka and I. Dankoco, "A Refugee in My Own Country: Evictions or Property Rights in the Urban Informal Economy?" Urban Studies 52, no.12 (2015): 22345.

[27]Kama hapo juu.

[28]J.O. Adekunle, "Race and the Rise of Swahili Culture," in *Color Struck: Essays on Race and Ethnicity in Global Perspective*, eds. J.O. Adekunle and H.V. Williams (Maryland: University Press of America, 2010), 30.

Majiji mengi tuliyo nayo leo hii katika nchi za Afrika ni mazao ya ukoloni. Wakoloni waliyasuka majiji hayo kama stahiki ya watu wa tabaka la juu. Mfumo wa kitabaka wakati wa ukoloni ulifungamanishwa na rangi ya ngozi.

Tuchukulie mfano wa jiji la Dar es Salaam ambalo lilistawishwa na wakoloni wa Kijerumani pale walipoamua kuhamisha makao makuu ya serikali yao kutoka Bagamoyo na kuyaleta Dar es Salaam. Jiji hilo lilisukwa katika misingi ya ubaguzi wa rangi, likigawanywa katika kanda tatu. Ukanda wa kwanza, uliojulikana kama *Uzunguni,* ulikuwa na makazi au/na ofisi za raia wa daraja la kwanza (wazungu). Ukanda huu ulipangiliwa, kujengewa miundombinu ya hadhi ya juu na kupewa huduma zote za muhimu. Ukanda wa pili uliitwa *Uhindini* ambako waliishi watu wenye asili ya bara la Asia. Wengi wa watu wenye asili ya Kiasia walikuwa wafanyabiashara na wachache walifanya kazi za kada ya kati katika serikali ya kikoloni. Ukanda huu ulikuwa na hadhi ya kati na ulitumika kama bafa (*buffer*) iliyotenganisha ukanda wa wazungu na Waafrika[29].

Katika ukanda wa tatu, uliojulikana kama Uswahilini, waliishi Waafrika ambao kimsingi hawakuhesabika kama raia bali watawaliwa (*subjects*). Ukanda huu

[29]J.R. Brennan and A. Burton, "The Emerging Metropolis: A History of Dar es Salaam, Circa 1862-2000," in *Dar es Salaam: Histories from an Emerging African Metropolis*, eds. J.R. Brennan, A. Burton and Y. Lawi (Dar es Salaam & Nairobi: Mkuki na Nyota Publishers & British Institute of East Africa, 2007).

haukuwa sehemu ya jiji bali pembezoni. Waafrika hawakutambuliwa kama binadamu kamili bali nusu-wanyama, wakibaguliwa kwa kunyimwa haki zote za kisiasa na kiuchumi. Hawakutakiwa kuishi jijini katika kitovu cha ustaarabu (*civilisation*) bali shamba ambako palionekana kama pori la washenzi (*barbarians*). Kwa kuwa biashara ilikuwa mikononi mwa watu wenye asili ya Asia basi Waafrika wengi waliokuwa jijini waliishi kwa kuchuuza vijibidhaa ambavyo waliuziana wao kwa wao katika maeneo yao[30].

Sera hii ya ubaguzi katika uendelezaji wa miji iliyoanzishwa na wakoloni wa Kijerumani iliendelezwa na wakoloni wa Kiingereza. Waafrika wasio na ajira rasmi waliitwa "wahuni" na walionekana kuwa tishio kwa usalama, amani na ustaarabu wa jiji[31]. Dola la kikoloni liliendesha operesheni mbalimbali za kuwatimua Waafrika hawa ili warejee vijijini ambako ndiko kulionekana kuwa stahiki yao.

Baada ya Tanzania Bara kujipatia uhuru wake mwaka 1961, hatua mbalimbali zilichukuliwa kukomesha ubaguzi wa rangi uliokuwa umewekwa na wakoloni. Mpango wa Kuafrikanisha (*Africanisation*) utumishi wa umma ulifanya nafasi nyingi zilizokuwa zimeshikiliwa

---

[30]Chambi Chachage, "A Capitalizing City: Dar es Salaam and the Emergence of an African Entrepreneurial Elite (C. 1862-2015)" (Ph.D Dissertation, Harvard University, 2018).

[31]A. Burton, "*Wahuni* (The Undesirables): African Urbanisation, Crime and Colonial Order in Dar es Salaam, 1919-1961" (Ph.D. Thesis, University of London, 2000).

na wageni kwenda mikononi mwa Waafrika. Watanganyika walioshika nafasi ya juu walianza kuishi katika nyumba na mitaa ambayo hapo awali ilikuwa ni kwa ajili ya Wazungu au Waasia tu. Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967, ulifanyika utaifishaji wa 'majumba' ya kupangisha ambayo, baada ya kuwekwa katika umiliki wa serikali, yalipangishwa kwa bei nafuu kwa Waafrika. Uboreshaji wa makazi katika baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam, ujenzi wa nyumba mpya za kupangisha kwa gharama nafuu chini ya Shirika la Nyumba la Taifa, ujenzi wa viwanda kwa ajili ya kutoa ajira, uwepo wa huduma za kijamii bila malipo na ruzuku za chakula na maji kwa wakazi wa mijini ni baadhi ya hatua zilizochukuliwa kwa ajili ya kuboresha hali za maisha za wananchi wa tabaka la chini. Hatua hizi, zikichagizwa na mshikamano uliotolewa na Tanzania kwa mavuguvugu ya ukombozi Kusini mwa Afrika, ambayo yalifungua ofisi zake Dar es Salaam, zililiweka jiji la Dar es Salaam katika ramani ya dunia kama 'Jiji la Kimapinduzi'[32].

Licha ya hatua hizo za kimaendeleo, bado tafsiri ya kazi katika awamu ya kwanza ilijikita katika kazi ya kuajiriwa kiwandani au kazi ya kilimo kijijini. Kwa maana hiyo, mafukara wa mijini ambao walijaribu kujitafutia riziki kwa kuchuuza vijibidhaa walionekana watu wazembe na wasiopenda kufanya

[32]George Roberts, *Revolutionary State-Making in Dar es Salaam: African Liberation and the Global Cold War, 1961 - 1974* (Cambridge: Cambridge University Press, 2022).

kazi. Mabavu ya dola yalitumika kuwaondoa mijini na kuwapeleka katika maeneo ya pembezoni mwa jiji au vijijini, ambako walipewa ardhi pamoja na ruzuku za pembejeo ili wajishughulishe na kilimo. Hata hivyo, wengi wa waliopelekwa vijijini walirejea tena mijini kwa ajili ya kuendelea kujitafutia kipato.

Kipindi cha uliberali mambo leo, kilichoanza baada ya Rais Mwinyi kuingia madarakani mwaka 1985, kilirudufisha na kuimarisha fikra na vitendo vya kikoloni kuhusu majiji na nafasi ya watu wa tabaka la chini ndani ya majiji hayo. Ni katika kipindi hiki ndipo iliibuka dhana ya "jiji lenye hadhi ya kimataifa" (*world class city)* ambayo inalenga kustawisha majiji ya Afrika ili yafanane na yale ya nchi za Magharibi. Kwa kuwa baadhi ya majiji ya nchi za Kusini kama Hong Kong (China), Dubai (Umoja wa Falme za Kiarabu) na Seol (Korea Kusini) yaliyofuata njia ya kuiga majiji ya Magharibi na kutambuliwa katika faharasa mbalimbali kama majiji ya kimataifa, basi watawala wa nchi za Kiafrika nao hupambana kuifikisha majiji wanayoyaongoza katika hadhi hiyo[33].

Dhana ya jiji lenye hadhi ya kimataifa inanakili mfumo wa ustawishaji majiji wa mahali kwingine na kuupachika katika nchi ya Kiafrika bila kuzingatia historia, mazingira wala mahitaji ya watu wa nchi za Kusini. Kama alivyoandika Prof. Mike Davis, msukumo

[33]I. Lindell et al. 2016. "New City Visions and the Politics of Redevelopment in Dar es Salaam." Uppsala: Nordiska AfrikaInstitutet

wa ustawi wa majiji ya nchi za Magharibi ulikuwa ni mapinduzi ya viwanda katika karne ya 19. Msukumo wa ukuaji wa majiji ya nchi za Kiafrika katika karne ya 21 sio mapinduzi ya viwanda bali ukuaji wa sekta isiyo rasmi[34]. Kwa kutaka kuiga na kulazimisha kufikia hadhi ya umagharibi, majiji ya Kusini yanataka kuondoa chanzo cha ukuaji wake katika karne ya 21 huku bado yakitaka kuendelea kubakia kuwa majiji. Hii ni sawa na mtu aliekula keki yake kisha akataka kuendelea kubaki nayo.

Jiji la kimataifa, kama lilivyo jiji la kikoloni, ni jiji lisilo na mafukara ndani yake. Kwa maana hiyo, nguvu kubwa hutumika katika kuwaondoa mafukara wa mijini, wakiwemo wamachinga, kutoka maeneo ya katikati ya jiji kwa sababu wanaonekana ni chanzo cha uchafu na uharibifu wa taswira njema ya jiji. Mwaka 2006, kwa mfano, Waziri Mkuu wa Tanzania aliziandikia barua mamlaka za majiji na miji mikubwa nchini na kuziagiza kuwaondoa wamachinga kutoka katikati ya majiji. Katika jiji la Dar es Salaam pekee, wamachinga wapatao milioni 1 waliondolewa kwa kutumia mabavu ya dola, jambo lililosababisha vifo vya watu wawili, majeraha, ulemavu wa kudumu na, upotevu wa mali na vyanzo vya kujikimu vya wamachinga[35]. Timua timua ya wamachinga iliendelea katika kipindi chote

---

[34]Mike Davis, "Planet of Slums: Urban Involution and the Informal Proletariat," *New Left Review* 26 (2004): 5-34.

[35]Colman Msoka and Tulia Ackson, "The Politics and Regulation of Street Trading in Dar es Salaam," in *Rebel Streets and the Informal Economy: Street Trade and the Law*, eds. Alison Brown (London and New York: Routledge, 2017).

cha awamu ya nne na kusababisha maumivu makali kwa wamachinga.

Mabavu yanayotumika dhidi ya wamachinga na wavujajasho wengine wa mijini ni kiashiria kuwa, licha ya kuwepo kwa mageuzi ya kuleta haki za binadamu, utawala bora na demokrasia, uhusiano wa dola la kiliberali mamboleo na watu wa matabaka yanayovuja jasho umebaki kutawaliwa na mabavu. Wanufaika wa demokrasia, utawala bora na haki za binadamu katika kipindi cha uliberali mamboleo ni watu wa matabaka ya juu, na hasa wale wanaomiliki mtaji, na siyo wavujajasho ambao huonewa na kuporwa vyanzo vyao vya kujikimu kila uchao.

Jambo linaloweza kuacha maswali kwa msomaji ni: inawezekanaje kukawa na uporaji wa bidhaa za wamachinga ilhali serikali imekuwa ikijitapa kuwa sera yake kuu ni urasimishaji wa sekta isiyo rasmi? Ndiyo, ajenda ya urasimishaji imo katika Sera ya Maendeleo ya Biashara Ndogondogo na za Kati (*Small and Medium Enterprises Development Policy*) ya mwaka 2002. Kadhalika, mwaka 2003, serikali ilizindua Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Ajenda ya urasimishaji wa biashara ndogo ndogo iliyomo katika Sera na MKURABITA imelenga kumtoza kodi mfanyabiashara mdogo na kumhamasisha kuchukua mkopo kutoka katika taasisi za fedha. Hapa tunaona kuwa lengo kuu la urasimishaji siyo kutoa unafuu kwa mfanyabiashara mdogo bali kumweka katika makucha ya dola na

taasisi za kifedha ili kumpora kipato chake kupitia utitiri wa tozo na kodi (kwa upande wa dola), pamoja na riba na faini za mkopo (kwa upande wa taasisi za kifedha)[36].

Mojawapo ya vigezo vikuu vya urasimishaji ni kufanya biashara katika maeneo yaliyoruhusiwa na serikali. Kwa mantiki hiyo MKURABITA ni moja ya nyenzo zinazotumika kuhalalisha timua timua ya wamachinga ili waende katika masoko au maeneo rasmi, ambayo yamepangwa bila kuwashirikisha wamachinga wala kukidhi mahitaji yao.

Masoko mengi yaliyojengwa kama sehemu ya mpango wa kuwarasimisha wamachinga yameendelea kubaki tupu kwa sababu hayakuzingatia uhalisia na mahitaji ya biashara ya umachinga. Masoko hayo yamejengwa kwenye maeneo yasiyo na mzunguko wa watu na usanifu na ujenzi wake umeiga mitindo ya Kimagharibi na kufanyika kutoka juu bila kuwashirikisha wamachinga. Mfano mzuri ni soko la Machinga Complex lililoko jijini Dar es Salaam ambalo lilianza kujengwa mwaka 2007 na kukamilika miaka miwili baadaye. Tovuti ya Jiji la Dar es Salaam imeweka wazi kuwa lengo la ujenzi wa Machinga Complex, yenye uwezo wa kubeba wafanyabiashara wadogo 4,206, ni "kuwaweka pahala pamoja pa

[36]Faria Shomary, "Vikundi vya Akiba na Mikopo vya Usawa: Njia Mpya ya Wanyonge Kupambana na Unyonyaji wa Benki," katika *Wavujajasho dhidi ya Soko Huria: Uzoefu, Mapambano na Dira Mbadala,* toleo la 3, mh. Sabatho Nyamsenda (Dar es Salaam: Rosa Luxemburg Stiftung - East Africa, 2021)

kufanyia kazi wafanya biashara ndogo ndogo zaidi ya 10,000 walio zagaa katika mitaa mingi ya katikati ya jiji letu." Kwa kufanya hivyo, serikali inadhamiria "kuliweka jiji katika hali ya usafi na serikali kupata mapato yatokanayo na shughuli zinazofanywa na wafanya biashara hao."[37]

Kwa hiyo, lengo kuu la ujenzi wa Machinga Complex linajieleza wazi kuwa ni kumwondoa mmachinga mtaani na kumpeleka katika jengo la kisasa la ghorofa. Wazo zuri, sivyo? Mfikirie mama anaetegemea kuuza karanga za kukaanga kwa wanafunzi wa shule ya msingi pembeni mwa kituo cha daladala. Wataalamu waliobuni Machinga Complex wanamtaka mama huyo kutoka mtaani kwa hiyari, na akigoma ataondolewa kwa nguvu, ili aende kuuza karanga zake katika ghorofa ya nne pale Machinga Complex. Je, atakuwa na uwezo wa kulipia kizimba cha biashara, pamoja na gharama lukuki za uendeshaji hapo Machinga Complex? Je, wateja wake, ambao ni wanafunzi wa shule ya msingi, watapanda daladala kutoka shuleni ili wamfuate mama huyo huko Machinga Complex kwa ajili ya kununua pakiti moja ya karanga? Ni wazi kuwa wabunifu wa wazo hili, walikaa ofisini, wakaja na wazo walilodhani ni zuri lakini halikuzingatia uhalisia wa biashara ya umachinga. Mfumo huu wa ufanyaji maamuzi na upangaji miji kutoka juu umejengwa katika dhana kwamba watu wa tabaka

[37]DCC, "Mradi wa Biashara wa Jiji (Machinga Complex)," (hakuna tarehe). Imepatikana Oktoba 5, 2022 kutoka http://www.dcc.go.tz/project-details/city-business-park

la chini hawana uwezo wa kiakili wa kuamua kuhusu upangaji na uendeshaji miji, na kwa maana hiyo wanapaswa kuwa wapokea maamuzi badala ya wafanya maamuzi. Na wanapoletewa maamuzi kutoka juu, wavujajasho hulazimishwa kuyakubali na kuyashangilia hata kama ni maamuzi mabovu yatakayoathiri ustawi na utu wao.

Wataalamu waliochoma mabilioni kujenga jengo la ghorofa sita, kama kweli walikuwa na nia njema, basi nia hiyo njema ilitumika kupamba njia ya kwenda kuzimu. Lakini upo ushahidi wa wazi unaothibitisha mianya ya ufisadi katika ujenzi wa *Machinga Complex*, na baadae katika uendeshaji wake, jambo lililosababisha hasara kwa Jiji la Dar es Salaam, ambalo limeshindwa kulipa mkopo wa ujenzi wa jengo hilo[38]. Kwa upande wao, wamachinga waligoma kuhamia katika jengo hilo na hivyo kulifanya liendelee kuwa tupu kwa zaidi ya miongo miwili baada ya kukamilika kwake! Hii ilizifanya mamlaka za jiji kuzidisha ukatili katika mazoezi ya timua timua kwa lengo la kuwalazimisha wamachinga kuhamia katika maeneo waliyopangiwa.

Timua timua ya wamachinga ilipungua kwa kiasi kikubwa kuanzia mwaka 2016 pale Rais wa awamu ya tano, John Pombe Magufuli alipoamua kubadili mwelekeo juu ya suala la wamachinga. Mtazamo wa hayati Magufuli ulijikita katika dhana ya kimageuzi

[38]Mwananchi, "Deni la Machinga Complex Mfupa Mgumu," Novemba 15, 2022. Imepatikana Decemba 10, 2022 kutoka https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/deni-machinga-complex-mfupa-mgumu-4020348

ya haki-jiji, iliyowahakikishia wamachinga haki ya kufanya shughuli zao katika maeneo ya katikati ya jiji. Awamu ya tano ilitoa vitambulisho vya wamachinga vilivyolenga kuwapatia ulinzi wamachinga dhidi ya timua timua iliyokuwa ikifanywa na mamlaka za miji na majiji. Wamachinga, ambao siku zote walikuwa wakipambana kwa ajili ya haki yao ya kufanya shughuli zao katikati ya jiji, waliyapokea mabadiliko hayo kwa furaha na kwa mara ya kwanza wakajiona kama raia huru wenye haki ya kujipatia kipato katika maeneo ya katikati ya jiji. Katika mahojiano na Mwananchi Digital, wamachinga walielezea mabadiliko hayo katika utawala wa Magufuli:

> *Kipindi ambacho hatujapata vitambulisho, tulikuwa tunakimbizwa na wagambo, tulikuwa tunafukuzwa sehemu za kazi lakini toka tumeanza kupewa na mheshimiwa Rais [Magufuli] vitambulisho vyake hivi hakuna changamoto yoyote ambayo tunakutana nayo kwa maana ya kubughudhiwa, kufukuzwa au kukimbizwa kimbizwa na wagambo*[39].

Baada ya Rais Magufuli kuaga dunia Machi 17, 2021, awamu iliyofuata iliamua kurejea katika mwelekeo wa sera za "jiji la viwango vya kimataifa". Septemba 13, 2022 Rais Samia Suluhu Hassan aliwaagiza wakuu wa mikoa "kuchukua hatua za kuwapanga vyema wamachinga"

[39]*Mwananchi Digital*, "Wamachinga Wanavyofurahi Mbele ya Mgambo, Meno Yote Nje," Januari 31, 2020. Imepatikana Oktoba 5, 2022 kutoka https://www.youtube.com/watch?app=desktop&v=iiG582tcYDI

ambao alidai kuwa "wameenea kila pahali" na hivyo kuwakinga wenye maduka na kuisababishia serikali upotevu wa mapato. Kufuatia agizo hilo la Rais, wakuu wa mikoa walitoa siku 30 kwa wamachinga kuondoka katika maeneo ya wazi ya katikati ya jiji na kuhamia katika maeneo yaliyoruhusiwa kisheria. Hata kabla ya siku hizo 30 kuisha, mabavu yalianza kutumika dhidi ya wamachinga na kusababisha dhahma kubwa katika mitaa ya Vingunguti Scania na Msimbazi/Mchikichi jijini Dar es Salaam. Baada ya siku 30, timua timua ya wamachinga ilifanyika nchini kote huku wengi wao wakiondolewa katika maeneo ya katikati ya jiji na kupelekwa maeneo ya pembezoni, yasiyo na miundombinu wala wateja. Sio ajabu kwamba wamachinga hawakukaa katika maeneo hayo na wameanza kurudi katika maeneo ya katikati ya jiji walikofukuzwa, jambo linalopelekea mapigano yasiyoisha kati ya wamachinga, wanaojitafutia riziki katikati ya jiji, na mgambo, wanaoagizwa na mamlaka za majiji kuwaondoa wamachinga. Mapigano ya hivi karibuni yametokea tarehe 8 Februari 2022 jijini Mwanza na kupelekea maandamano katika maeneo ya Makoroboi, Sahara na Lumumba. Wakizungumza kwa uchungu wakati wa tukio hilo, wamachinga walisema:

> *Serikali itamke wazi kama imefikia hatua ya kuwagawa Watanzania kwa grade (madaraja): hawa wa mjini, hawa wa porini; hawa wa kushinda njaa, hawa wa kula. Imefikia mwisho, tuheshimiane. Sote ni Watanzania, tuna haki katika nchi hii. Wao ni viongozi: wanakula*

> *wanashiba, sisi tunakufa na njaa. Kuanzia leo hii, sisi wafanyabiashara ndogondogo tutafanya biashara mjini kama walivyo watu wengine, na sisi ni Watanzania kama walivyo wao... Ninyi ni waandishi, hampajui Bango la Zain, mkitoka hapa mwende kule. [Ni] kilometa 14 kutoka mjini kati. Unauza vitu kama hivi, hivi [ananyanyua na kuonyesha bidhaa zake, ambazo ni pochi za mfukoni za wanaume zilizofungwa katika kamba], utamuuzia nani kule porini?.. Kwa hiyo, tunawaomba watuvumilie, na sisi tuna haki. Magari mazuri wanatembelea wao, mishahara mizuri wao, posho kubwa wao. Wanashindana kuiba, wanashindana. Jana kwenye taarifa ya habari: Halmashauri inayoongoza kwa wizi [ni] Ilemela, pale.Wanashindana kuiba. Kwa hiyo, tunaomba tuvumiliane, na sisi tutafute mia mia zetu watustahimilie. Kama hii kazi ni haramu, watupe kazi zingine*[40]*.*

Maneno kama hayo yaliwahi kutamkwa Oktoba 25, 2021 wakati mazoezi ya kuwatimua wamachinga yakiwa yamekithiri nchini kote. Kutoka katika viunga vya Kariakoo jijini Dar es Salaam, Emmanuel Andrew, mhitimu wa chuo kikuu anayejishughulisha na umachinga, aliunguruma:

[40]*Jambo TV*, "Kimenuka Mwanza, Machinga Waingia Barabarani kwa Nguvu, Watuma Salamu kwa Rais," Februari 9, 2023. Imepatikana Februari 10, 2023 kutoka https://www.youtube.com/watch?v=y9S9M4vAoZE

> *Nani kati yenu nyie wote mlioko hapa nani alishawahi kuwa na kidonda? Nafikiri kila mtu hapa alishawahi kuwa na kidonda. Ni mara ngapi umempiga nzi makofi na bado anarudi kwenye kile kidonda? Uliwahi kujiuliza ni kwa sababu gani anakuja kwenye kile kidonda? Ulitakiwa uelewe hivi, anakuja kwenye kile kidonda kwa sababu pale ndipo anapopata chakula chake. Kila utakapompiga kofi ataondoka, atarudi. Na ukimuua, yule aliyeko jirani yake naye atakuja kula pale[41].*

> *Mmachinga haji Kariakoo kwa sababu anaifuata Kariakoo kama mji. Sisi hatuji kushangaa maghorofa haya. Kama ni maghorofa haya, hata kwenye TV si tunayaona? Kwenye movies [filamu] za Kihindi si tunaona akina Krishna wanaruka kwenye maghorofa? Tunaelewana vizuri? Mmachinga anakuja Kariakoo kwa sababu ndiyo sehemu nyepesi ambayo mzunguko wa pesa upo, yaani money circulation hapa Kariakoo ipo[42] .*

Akifafanua zaidi, Andew alisema kuwa wamachinga "wanauza kwa watu, hawaendi kuuzia miti wala hawauzii wanyama...Tungetaka kuuzia wanyama au miti, tungeenda Serengeti. Kwa nini huyu mtu anakuja kuuza karibu na barabara? Kwa sababu hapo ndipo

---

[41]*Jambo TV*, "Machinga Wasema Wako Tayari Kufa, Hawaondoki; Wamkumbuka Magufuli, Watoa Msimamo wa Mwisho," Oktoba 25, 2021. Imepatikana Septemba 15, 2022 kutoka https://www.youtube.com/watch?v=mDehkHx9K8Q

[42]Kama hapo juu.

panapopita watu."

Nukuu hizo zinatuonyesha kuwa wamachinga wanatazama operesheni za timua timua kama operesheni zenye sura ya kitabaka, zifanywazo na watawala dhidi ya mafukara wa mijini kwa lengo la kuwafukuza wamachinga mijini. Pili, watawala wanawaona wamachinga kama vikaragosi, wasio na uwezo wa kufikiri, na hivyo watawala wameamua kuchukua jukumu la kufikiri na kuamua kwa niaba ya wamachinga. Watawala hufanya maamuzi yao juu ya wamachinga bila kujifunza kuhusu uhalisia na mahitaji ya biashara ya umachinga, na kwa mantiki hiyo, hutumia mabavu ya dola kuwarundika pamoja katika maeneo ya nje ya mji ambako hakuna wateja. Kwa kufanya hivyo, watawala wamezidi kuwaongezea ufukara wamachinga kwa kuua biashara zao. Na kwa kuwa hawana namna nyingine ya kuishi, wamachinga wameamua kurejea katikati ya jiji, 'liwalo na liwe'. Kwa maana nyingine, kama ambavyo nukuu ya Andrew hapo juu kuhusu falsafa ya 'nzi na kidonda' inaonyesha, wamachinga wako tayari kuhatarisha uhai wao wakijitafutia riziki kuliko kufa kwa njaa katika maeneo yasiyo na wateja wanakolazimishwa kwenda.

## Hitimisho

Sura hii imefanya uchambuzi wa nafasi ya wamachinga katika mfumo wa kibepari. Kwa kuanzia, imeonyesha kuwa wamachinga ni wavujajasho, kama walivyo

wafanyakazi au wakulima. Kazi yao huuruzuku mfumo wa kibepari kwa kutoa nguvu kazi ya bei nafuu katika usambazaji wa bidhaa au upishi wa chakula. Pili, sura hii imeainisha historia ya umachinga nchini Tanzania na kuonyesha kuwa ukuaji wake wa haraka kuanzia miaka ya 1990 ulisababishwa na sera za soko huria zilizopelekea uporaji wa vyanzo vya maisha mijini na vijijini na kuua ajenda ya kujenga uchumi unaojitegemea. Tatu, sura hii imeangazia pia historia ya ukuaji na ustawishaji wa miji nchini Tanzania, ikitumia mfano wa jiji la Dar es Salaam. Katika uchambuzi huo, sura hii imeonyesha kuwa jiji la Dar es Salaam lilipangiliwa na kustawishwa kama jiji la kikoloni, ambalo lilibagua mafukara wa mijini kwa kuwanyima huduma za msingi na kuwatimulia mbali. Timua timua hiyo ya mafukara wa mijini imeendelea hata baada ya uhuru na kukomaa zaidi baada ya mageuzi ya sera za soko huria. Licha ya oparesheni za timua timua kuwasababishia hasara kubwa na hata kuhatarisha uhai wao, wamachinga wamegoma kuondoka katika maeneo ya katikati ya jiji wakidai kuwa hata wao ni raia na wanayo haki ya kujipatia riziki ndani ya jiji lao kama walivyo watu wa tabaka la juu. Kwa kuwa timua timua inalindwa na sera na sheria, hasa za mipango miji, basi sura inayofuatia inachambua kwa kina baadhi ya sera na sheria za mipango miji zinazohusiana na wamachinga.

# SURA YA 3

# Mipango Miji na Wamachinga

JOSEPH CHIOMBOLA

**Utangulizi**

Sura hii inaainisha sera na sheria zinazohusu ardhi na mipango miji kwa kuchambua masuala ya muhimu yaliyomo kwenye nyaraka hizo. Masuala hayo ni pamoja na uelewa kuhusu suala la ardhi kwa tafsiri ya sheria; mamlaka za usimamizi kwenye ardhi; umiliki wa ardhi; mamlaka za upangaji wa miji; taratibu

za mipango miji pamoja na haki na wajibu wa kila mmoja kwenye michakato ya upangaji wa miji.

Sura hii inaonyesha pia jinsi sheria, kanuni na miongozo kuhusu masuala ya mipango miji zinavyotumika kama nyenzo ya kuwakandamiza wafanyabishara wadogo maarufu kama wamachinga katika maeneo mbalimbali nchini. Sura hii imeangazia changamoto ambazo wamachinga wanakumbana nazo katika shughuli zao za kila siku katika muktadha wa utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo ya mipango miji nchini.

**Mifumo ya Milki ya Ardhi**

Ardhi ni rasilimali ya msingi kwa maisha ya jamii nyingi za wazalishaji wadogo wanaoishi vijijini na pembezoni mwa miji mikubwa. Jamii za wazalishaji wadogo zinajumuisha wakulima wadogo, wafugaji, wavuvi, jamii za waokota matunda na warina asali hutegemea ardhi kwa asilimia zaidi ya 80 ili kuweza kuendesha maisha yao ya kila siku. Vilevile, kwenye jamii hizo za wazalishaji wadogo ardhi sio tu msingi wa maisha yao bali pia ni alama ya mamlaka, utambulisho wa mila na desturi zao na inabeba historia muhimu ya maisha yao.

Kutokana na umuhimu huo, mfumo wa umiliki wa ardhi unapaswa kuwa shirikishi na wenye demokrasia unaojali maslahi na mahitaji ya wazalishaji wadogo ambao ndio watumiaji wakubwa wa ardhi. Nchini

Tanzania, masuala ya ardhi yameainishwa katika sera na sheria mbalimbali ambapo misingi mikuu imewekwa kwenye Sera ya Taifa ya Ardhi[43], Sheria ya Ardhi[44] na Sheria ya Ardhi ya Vijiji[45]. Masuala ya msingi yaliyomo katika sera na sheria hizo yamechambuliwa hapa chini.

**Misingi Mikuu ya Sera ya Taifa ya Ardhi**

Sera hii imeanisha misingi inayopaswa kuhakikisha kuwa kuna mgawanyo na upatikanaji sawa wa ardhi kwa wananchi wote; kuhakikisha haki za kimila za wazalishaji wadogo zinaainishwa, kufafanuliwa na kulindwa kisheria; kuwepo kwa ukomo wa kiwango cha umiliki wa ardhi ili kuepuka kuhodhi ardhi; kuhakikisha ardhi inatumika kwa uzalishaji ili kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi; kuimarisha mfumo wa usimamizi wa ardhi ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za ardhi; kuimarisha mfumo wa taasisi za usimamizi wa ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi ili kuongeza uwazi; kuimarisha mfumo wa utoaji taarifa za ardhi; na kuilinda ardhi dhidi ya uharibifu kwa maendeleo endelevu.

[43] Ya Mwaka 1995

[44] Namba 4 ya mwaka 1999

[45] Namba 5 ya mwaka 1999

## Milki ya Hatma

Hii ni mamlaka ya maamuzi ya mwisho katika ardhi ambapo Sera ya Taifa ya Ardhi inaainisha[46] kwamba ardhi yote iliyopo Tanzania ni ardhi ya kiumma[47] chini ya udhamini wa Rais. Mamlaka hiyo ya udhamini inajumuisha mamlaka ya utwaaji, kuchukuliwa kwa ardhi kwa maslahi ya umma kama ilivyoanishwa kwenye *Sheria ya Utwaaji* namba 47 ya mwaka 1967. Pia mamlaka ya uhawilishaji, ubadilishwaji wa ardhi kutoka kundi moja kwenda kundi jingine kama ilivyoanishwa kwenye *Sera ya Taifa ya Ardhi, Sheria ya Ardhi* namba 4 ya 1999[48] na *Sheria ya Ardhi ya Vijiji* namba 5 ya mwaka 1999[49]. Vilevile, mamlaka ya udhamini inajumuisha uwezo wa kufuta hati ya umiliki wa ardhi kwa mtu yeyote iwe alipata ardhi hiyo kwa njia halali au haramu kama ilivyoainishwa kwenye *Sera ya Taifa ya Ardhi*[50], Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999[51] na *Sheria ya Ardhi ya Vijiji* namba 5 ya mwaka 1999[52].

[46]Tamko la Sera 4.1.1 (i)(a)

[47]Tamko hili la Sera lina lengo la kuanisha ardhi na siyo kumilikisha ardhi kwa mamlaka za usimamizi.

[48]Kifungu cha 5(1)

[49]Kifungu cha 4 na 5

[50]Sehemu ya Tatu ya Sera

[51]Kifungu namba 45 (3)

[52]Kifungu namba 44 (1)

## Maana ya Ardhi

Sheria ya Ardhi namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 za mwaka 1999 zimefafanua[53] kuwa ardhi inajumuisha vitu vyote vinavyopatikana juu na chini ya uso wa nchi ikiwemo mazao, uoto wa asili na maendelezo yoyote yaliyokusudiwa kudumu katika ardhi isipokuwa madini, mafuta na gesi. Hii ina maana kuwa madini, mafuta na gesi si sehemu ya ardhi kwa mujibu wa sheria ya ardhi na usimamizi wa maada hizo upo chini ya mamlaka husika. Matumizi ya rasilimali za madini, mafuta na gesi zinapaswa kutumika kwa maslahi ya Watanzania wote ndio maana hakuna mtu anayeruhusiwa kujimilikisha rasilimali hizo kwa maslahi binafsi.

## Makundi ya Ardhi

Ardhi iliyopo nchini imegawanyika katika makundi ili kuweza kurahisisha mfumo wa usimamizi wa ardhi. Ardhi imegawanyika katika makundi matatu ambayo ni Ardhi ya Jumla, Hifadhi na Kijiji ambapo:

(i) Ardhi ya Jumla ni ardhi yote ya umma ambayo sio ya kijiji wala ya hifadhi. Hata hivyo, ardhi ya kawaida inajumuisha pia ardhi ya kijiji ambayo, haikaliwi wala kutumiwa na wanavijiji;

[53]Kifungu namba 2 cha Sheria ya Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999

(ii) Ardhi ya hifadhi ni ardhi ambayo imetengwa kwa ajili ya matumizi maalumu ya uhifadhi kama vile hifadhi ya misitu, mabwawa ya mikoko na matumbawe, ardhi oevu, visiwa vilivyopo karibu na fukwe za bahari au maziwa, ardhi inayotumiwa kutupa taka zenye sumu, ardhi yote iliyo ndani ya meta sitini (60) kutoka ukingo wa mto au ziwa, ardhi yenye miteremko mikali, mbuga za wanyamapori, hifadhi za taifa, vyanzo vya maji, barabara, na ardhi yenye madhara na;

(iii) Ardhi ya Kijiji ni ardhi yote ambayo ipo ndani ya mipaka ya Kijiji. Sheria zinazotambulisha ardhi ya kijiji kulingana na uundwaji wa kijiji husika ni pamoja na; *Sheria ya Makazi ya Vijiji* namba 27 ya 1965, *Sheria ya Vijiji na Vijiji vya Ujamaa* ya 1975, Sheria ya *Serikali za Mitaa (Tawala za Wilaya*) namba 7 ya 1982 na *Sheria ya Ardhi ya Vijiji* namba 5 ya 1999.

## Usimamizi wa Ardhi

(i) *Kamishna wa Ardhi*

Kamishina wa Ardhi ndiye msimamizi mkuu wa ardhi yote ya jumla na amepewa majukumu ya kiushauri kwenye ardhi ya vijiji. Vilevile, Kamishna wa Ardhi ana jukumu la kutoa maelekezo kwa Halmashauri ya Kijiji kuhusu usimamizi wa ardhi ya kijiji na vijiji vinapaswa kutekeleza ushauri watakaopewa na Kamishna wa Ardhi.

(ii) *Halmashauri ya Kijiji*

Halmashauri ya Kijiji ni msimamizi wa ardhi ya kijiji na itawajibika kusimamia ardhi yote ya kijiji kwa niaba ya wanakijiji wote kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya vijiji. Katika utekelezaji wa mamlaka hiyo Halmashauri ya Kijiji inapaswa kutoa taarifa ya usimamizi wa ardhi kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji, chombo ambacho hutoa uamuzi wa mwisho kuhusu ugawaji na matumizi ya ardhi ndani ya kijiji.

(iii) *Mamlaka za Usimamizi wa Ardhi za Hifadhi*

Ardhi za hifadhi husimamiwa na mamlaka mbalimbali kutegemea na aina ya hifadhi husika. Kwa mfano kama ni hifadhi ya mbuga za wanyama basi husimamiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Mbuga za Taifa (TANAPA); ardhi ya hifadhi ya barabara husimamiwa na wakala za barabara nchini ambazo ni TANROADS na TARURA; na hifadhi ya vyanzo vya maji huwa chini ya mamlaka za mabonde ambayo chanzo hicho hupatikana.

## Mfumo wa Umiliki

Zipo aina mbili za umilikaji wa ardhi nchini Tanzania: umilikaji wa ardhi kimila na umilikaji wa ardhi kwa hati.

(i) *Umilikaji Ardhi Kimila*

Huu ni utaratibu wa umilikaji ardhi kwa kufuata taratibu za kimila na desturi za jamii husika. Kila koo na

jamii zilikuwa na taratibu zake za kupata, kutumia na kugawa ardhi ambazo zilikuwa zikitumika tangu enzi za mababu. Taratibu hizi zimeendelea kutambulika na kulindwa kisheria. Kabla ya Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 umiliki huu ulionekana ni wa hadhi ya chini kuliko ule wa hati.

(ii) *Umilikaji Ardhi kwa Hati*

Chimbuko la aina hii ya umiliki ni sheria ya wakoloni wa Kiingereza ya mwaka 1923 ambayo ilitamka kwamba ardhi yote ni mali ya umma na hakuna mtu yeyote mwenye haki ya kufanya chochote juu ya ardhi hiyo bila idhini ya dola hasa mhimili wa utendaji au serikali kama inavyojulikana. Ni kutokana na sheria hii ndiyo Gavana akaidhinisha ugawaji wa ardhi kwa walowezi kwa kutumia hatimiliki kwa vile wasingeweza kumiliki ardhi kimila. Hadi leo utaratibu huu wa hati unatumika na kutolewa katika kundi la ardhi ya kawaida. Kwa utaratibu huu, mtu yeyote ambaye ni raia anaweza kumiliki ardhi kwa hati ya miaka 33, 66 au 99. Hata hivyo, mmiliki huyo anakuwa na hadhi ya mpangaji tu kwa vile mfumo wa umilki wa ardhi Tanzania haumruhusu mtu kumiliki ardhi kama mali yake moja kwa moja.

## Masuala Muhimu Kwenye Sheria ya Mipango Miji

Mipango miji ni mfumo wa upangaji na matumizi ya ardhi mijini kwa kuzingatia mahitaji au vipaumbele katika eneo ili kukidhi mahitaji ya mji na maendeleo

kwa ujumla. Msingi wa masuala ya mipango miji umewekwa katika *Sera ya Taifa ya Ardhi* ya mwaka 1995, *Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi* ya mwaka 2000 pamoja na *Sheria ya Mipango Miji* ya mwaka 2007. Vilevile zipo kanuni zilizotengenezwa chini ya Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 ambazo ni *Urban Planning (Use Groups and Use Classes) Regulations, 2018* na *The Urban Planning (Planning Space Standards) Regulations, 2018.*

*Mamlaka za Upangaji Miji*

*Sheria ya Mipango Miji* ya mwaka 2007 inaratibu mchakato wa mipango miji ambapo imeainisha kuwa halmashauri za majiji, manispaa, miji na miji midogo ndizo zenye mamlaka za upangaji miji na inapotokea mipango ikameza vijiji basi vijiji hivyo vitafutwa. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI amepewa mamlaka ya kutangaza (*gazette*) eneo kuwa eneo la mipango miji na katika tangazo hilo ni lazima eneo linaloingizwa kwenye mipango miji liwe na mipaka iliyofafanuliwa.

Kabla eneo halijatangazwa kuwa la mipango miji ni lazima litanguliwe na masuala muhimu ambayo ni: (i) mwitikio chanya (*favourable response*) katika mikutano ya umma iliyofanywa kwenye eneo husika; (ii) maazimio ya mamlaka ya upangaji kutoa maoni ya eneo kuwa la mipango miji; na (iii) maoni chanya kutoka Sekretariati ya Mkoa.

Baada ya eneo kutangazwa hatua zinazofuata ni kuwajulisha na kuhamasisha wananchi walio ndani ya eneo lililotambuliwa; kufanya uthamini wa maendelezo ndani ya eneo na kulipa fidia. Kisha mamlaka za upangaji miji hubuni michoro ya makazi na matumizi ya ardhi na kuiwasilisha kwa mjadala na kupitishwa kwenye Kamati ya Mipango Miji na Mazingira ya halmashauri husika, kisha Waziri na mwisho kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipango Miji.

Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa taratibu hizi hasa kwenye suala la ushirikishwaji na kupatikana kwa ridhaa ya wananchi kukubali kuwa sehemu ya mipango miji. Maamuzi mengi ya kuingizwa maeneo kwenye mipango miji yanafanywa na warasimu na wakati mwingine huwa na msukumo wa kisiasa au wa kifedha nyuma yake. Ndio maana kwenye maeneo mengi ya mipango miji, wenyeji wengi hawawi sehemu ya mipango hiyo pale inapokamilika kutokana na kujikuta wamepoteza ardhi zao na pia kuwepo kwa shughuli na masharti ya umiliki ambayo hayaendani na mfumo wa maisha waliozoea.

*Majukumu ya Maafisa Mipango Miji kwenye Upangaji*

Baada ya eneo kutangazwa na kuingizwa kuwa sehemu ya mipango miji, maafisa mipango miji hupaswa kuanza maandalizi ya mipango kabambe (*general planning scheme*) na mipango kina (*detailed planning scheme*) ya uendelezwaji wa mji. Mchakato

huo hutekelezwa katika hatua zifuatazo:

(i) Uhamasishaji wa madiwani, watendaji na watoa huduma muhimu za kijamii, kiuchumi na kitaasisi.

(ii) Uandaaji wa ramani ya msingi (*base map*).

(iii) Ukusanyaji wa takwimu na uchambuzi na tathmini ya takwimu za kimaendeleo na kimazingira.

(iv) Maandalizi ya rasimu ya mpango na ramani husika.

(v) Kufanya mkutano mkuu wa majadiliano/mashauriano na wadau husika.

(vi) Uainishaji wa masuala muhimu ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.

(vii) Kuandaa mpango endelevu wa mji pamoja na michoro/ramani husika.

(viii) Kuwasilisha mpango kwa wadau wa Halmashauri kwa maafikiano ya kukubaliwa au kukataliwa, kisha mpango huwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya mipango miji na kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipango Miji.

Uhalisia kwenye mchakato wa mipango miji huonyesha kuwa taratibu hukiukwa na hasa linapokuja suala la kuitisha vikao vya uhamasishaji na ukusanyaji wa maoni kuhusu mipango miji. Warasimu huitisha vikao vya wakazi wa eneo husika huku wakiacha wadau ambao sio wakazi wa eneo hilo ila hulitumia eneo hilo kwa shughuli mbalimbali za kujikimu ikiwemo biashara ndogondogo.

Katika mchakato wa mipango miji, kundi la wamachinga huathirika zaidi kwa kuwa maoni yao hayakusanywi kwa sababu wengi wao sio wakazi wa maeneo husika. Hii hupelekea maslahi yao kutoingizwa kama sehemu ya mipango miji na ndio maana ramani za matumizi za ardhi zinapotoka kwenye maeneo mengi ya mipango miji hazijatenga maeneo ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wadogo maarufu kama wamachinga.

Dhana ya uendelezaji miji kwenye mipango miji mingi iliyopitishwa hapa nchini haiakisi uhalisia kwa sababu imeshindwa kuweka shughuli ambazo zitawawezesha watu wa kada zote kujipatia kipato kupitia maeneo ya katikati ya miji. Madhara yake ni kupelekea wengi wao kufukuzwa katika maeneo ambayo awali walikuwa wakifanya biashara zao ndogondogo bila ya kupewa eneo mbadala la kuendesha biashara zao.

Vilevile, mawazo ya kuendeleza miji kwa kuweka vituo vya biashara kwa mfumo wa biashara kubwa kama vile *supermarkets* ni uthibitisho wa wazi kuwa

waliobuni mipango miji hiyo hawakufikiria au kutaka wamachinga kuwa sehemu ya miji hiyo. Warasimu wamekuwa wakiwahusisha wamachinga na vitendo vya uchafuzi wa mazingira, wizi, kusababisha msongamano wa barabara, kukwamisha ufanyaji usafi, kuzuia biashara kubwa, kupunguza mapato ya serikali, kuhatarisha usalama na ukwepaji wa kodi, hivyo basi, sio rahisi kwa viongozi wenye mtazamo huo kutenga maeneo ya wamachinga kufanyia biashara kwenye mipango miji.

## Sheria na Taratibu Zinazoathiri Shughuli za Wamachinga

### *Sheria Ndogo*

*Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* ya mwaka 1977 kama ilivyorejewa mara kwa mara, ibara ya 63(3)(d), imetoa mamlaka ya utungaji wa sheria nchini kuwa chini ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mamlaka hii ya utungaji wa sheria imekasimishwa kwa serikali za mitaa kuweza kutunga sheria ndogo ambazo zinatumika kwenye maeneo yao ya kiutawala kusimamia masuala mbalimbali. Sheria zinazotoa mamlaka kwa serikali za mitaa kutunga sheria ndogo ni *Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya)*[54] na *Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji)*[55].

[54]Sura ya 287 ya Sheria za Nchi

[55]Sura ya 288 ya Sheria za Nchi

Ni katika muktadha huo ndipo halmashauri za wilaya, manispaa, miji midogo na majiji zimeweza kutunga sheria ndogo zinazotumika kwenye maeneo yao ikiwemo sheria ndogo za mazingira, usafi, soko, ushuru na udhibiti wa shughuli za wafanyabiashara ndogondogo maarufu kama wamachinga. Utaratibu wa kisheria unaopaswa kutumika katika utungwaji wa sheria ndogo umeainishwa kwenye kifungu cha 90 cha *Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji)* ambao ni pamoja na:

(i) Kutolewa kwa notisi ya kusudio la kutungwa kwa sheria ndogo husika kwa wakazi wa eneo hilo na wadau wengine ambao wataathirika na utekelezaji wa sheria ndogo hiyo. Notisi yapaswa kutolewa kwa muda usiopungua wiki mbili na kuwekwa kwenye maeneo yote ya umma na maoni yatakusanywa kutoka kwa wadau.

(ii) Mara baada ya kuisha kwa notisi na utoaji wa maoni, sheria ndogo huandaliwa kwa kuzingatia maoni ya wadau na sheria nyingine za nchi kisha kuingizwa katika vikao mbalimbali vya kamati na mwisho hujadiliwa na kupitishwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

(iii) Rasimu ya sheria ndogo hizo hupitishwa kwenye ngazi ya mkoa ingawa sio utaratibu unaoonekana moja kwa moja kwenye sheria

kisha huwasilishwa kwa Waziri wa TAMISEMI halafu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Baada ya kuidhinishwa, sheria ndogo huchapishwa kwenye gazeti la serikali na kuanza kutumika rasmi toka tarehe ilipopewa namba na kuchapwa.

Kwenye halmashauri za majiji na manispaa, kuna sheria ndogo ambazo zimekuwa na muingilino wa moja kwa moja na shughuli za wamachinga. Baadhi ya sheria ndogo hizo ni pamoja na Sheria Ndogo za Afya na Usimamizi wa Mazingira, *Sheria Ndogo za Uratibu na Usimamizi wa Wamachinga na Sheria Ndogo za Ushuru wa Masoko na Magulio.*

Sheria ndogo hizo zimeweka masharti mbalimbali ikiwemo mahitaji ya vibali, kusajiliwa kwa wamachinga, ulipaji wa tozo na ushuru mbalimbali, kufanya usafi, biashara kwenye maeneo yaliyotengwa tu. Baadhi ya masharti yaliyowekwa katika sheria ndogo hizo hayaendani na uhalisia wa shughuli za wamachinga. Mathalani, suala la wamachinga kuwa na vizimba na maeneo maalumu ya biashara halikuzingatia wamachinga ambao hutembeza vitu kutoka mtaa mmoja hadi mwingine kila siku au ambao hupanga vitu katika maeneo ya pembezoni mwa barabara.

Vilevile, sheria ndogo hizi zinatoa adhabu kwa makosa mbalimbali ya ukiukaji wa masharti yaliyoandikwa kwenye sheria ndogo hizo. Adhabu zilizoainishwa

kwenye sheria ndogo hizo zinaanzia elfu hamsini hadi milioni moja ambapo kwa hali halisi ya kipato cha wamachinga faini hii ni kubwa isiyoweza kulipwa hivyo kupelekea kuwekwa vizuizini katika vituo vya polisi na mali zao kuchukuliwa bila kurudishwa kwao pale mashauri waliyofunguliwa yanapofikia mwisho.

Pia, sheria ndogo hizo ndizo hutumika katika Mahakama ya Jiji ili kutoa adhabu mbalimbali kama zilivyoanishwa kwenye sheria ndogo hizo. Utaratibu unaotumika ni wa kusomewa mashtaka yako na kutakiwa kukiri ili taratibu za kufifilishwa kwa makosa ziweze kufanywa na faini inayopangwa ilipwe ili mtuhumiwa aachiwe huru na iwapo atashindwa basi atumikie kifungo kilichoainishwa.

*Mahakama ya Jiji*

Hii ni mahakama iliyoanzishwa kwa ajili ya kusikiliza mashauri yote yanayotokana na utekelezaji wa sheria ndogo zinazotungwa na Halmshauri za Jiji na Manispaa zilizopo katika Jiji la Dar es salaam. Mahakama hii ina historia ya muda mrefu ya uanzishwaji wake ambao ulitokana na utekelezaji wa maamuzi ya mashauriano kati ya Rais, viongozi na madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam yaliyofanyika tarehe 10 Februari 1983 katika ukumbi wa Karimjee.

Katika kikao hicho, moja ya hoja zilizoibuka, kujadiliwa na kufanyiwa maamuzi ilikuwa tatizo la mashauri yanayotokana na sheria ndogo (*by-laws*) za jiji ambapo

Mheshimiwa Rais aliagiza *"Halmashauri ya Jiji iwe na mahakama yake yenyewe ya kushughulikia wavunjaji wa by-laws zake"*. Katika utekelezaji wa maamuzi hayo, Katibu Mkuu Wizara ya Sheria alitoa maagizo kwa Halmashauri ya Jiji kutafuta jengo la mahakama hiyo na kwa Mahakama kutoa Mahakimu watakaosikiliza mashauri hayo.

Kama ambavyo lengo lake lipo wazi, Mahakama ya Jiji hutumia sheria ndogo zinazotungwa na Halmashauri ya Jiji na Manispaa ili kusikiliza na kuamua mashauri yanayotokana na makosa yaliyoanishwa kwenye sheria ndogo hizo. Jiji la Dar es Salaam linazo sheria ndogo mbalimbali ikiwa ni pamoja na *Sheria Ndogo za Ada na Ushuru*; *Sheria Ndogo za Kudhibiti Omba Omba; Sheria Ndogo za Uendeshaji wa Soko la Samaki Feri Magogoni; Sheria Ndogo za Ulinzi wa Umma; Sheria Ndogo za Afya na Usimamizi wa Mazingira; Sheria Ndogo za Ada na Vibali vya Shughuli za Kiutamaduni; Sheria Ndogo za Uratibu na Usimamizi wa Wamachinga; na Sheria Ndogo za Ushuru wa Masoko na Magulio.*

Mahakama ya Jiji haionekani kwenye mfumo rasmi unaojulikana wa mahakama na hivyo hata taratibu zake za uendeshaji wa mashauri hazijulikani kwa wananchi walio wengi. Uzoefu kutoka kwa wananchi waliowahi kufikishwa katika mahakama hiyo unaonyesha kuwa mtu hupelekwa kusomewa mashtaka yanayomkabili na kutakiwa kulipa kwa njia ya kufifilishwa kwa kosa (*compounding of offenses*). Viwango vya adhabu vinatofautiana kuanzia

shilingi elfu hamsini (Sh.50,000/=) hadi milioni moja (Sh.1,000,000/=) pamoja na kifungo cha jela cha kati ya miezi 6 hadi miezi 12.

Wafanyabiashara wadogo, maarufu kama wamachinga, wamekuwa wahanga wa utekelezaji wa sheria ndogo na mahakama hii ya jiji kutokana na wengi wao kujikuta wamefikishwa kwenye mahakama hiyo kwa makosa mbalimbali kama vile madai ya uchafuzi wa mazingira, kufanya biashara sehemu isiyoruhusiwa, kuzurura, kufanya biashara bila kibali, n.k. Sheria ndogo pamoja na Mahakama ya Jiji zimekuwa mwiba mkali kwa wamachinga kutokana na wengi wao kutofahamu sheria na taratibu za sheria hizo ambazo ni kandamizi, na hivyo kuishia ama kulipa faini au kwenda jela au vyote viwili kwa pamoja.

Kutokana na kukosekana kwa sheria inayoonyesha utaratibu wa uendeshaji wa mashauri katika Mahakama ya Jiji, maafisa wanaosimamia utekelezaji wa sheria ndogo za halmshauri ndio wamekuwa wakamataji, walalamikaji na waendesha mashauri. Uzoefu wa wamachinga waliofikishwa kwenye mahakama hiyo unaonyesha kuwa mshtakiwa husomewa mashtaka na kutakiwa kukubali kosa na kusainishwa fomu ya kufifilishwa kwa kosa hilo.

Utaratibu huu ni kandamizi kwa kuwa haumpi nafasi mshtakiwa kujieleza na kujitetea kwa kosa analoshtakiwa nalo kinyume kabisa na taratibu za haki asili (natural justice) zinazotaka mshtakiwa

kupewa nafasi ya kusikilizwa kabla ya kuhukumiwa. Kwa mazingira ya utekelezaji wa sheria ndogo za halmashauri na usikilizaji wa mashauri kwenye Mahakama ya Jiji, mmachinga huweza kukamatwa asubuhi halafu mchana akafikishwa kwenye mahakama hiyo ya jiji na kufikia saa tisa akajikuta anaingizwa gerezani.

## Changamoto za Wamachinga Katika Muktadha wa Sheria na Miongozo ya Mipango Miji na Sheria Nyingine

Wamachinga wamekuwa wahanga kutokana na utekelezaji wa sheria mbalimbali ikiwemo ya mipango miji na sheria ndogo zinazotungwa na Halmshauri ya Jiji. Baadhi ya hoja za msingi ni pamoja na:

(i) Ushiriki na ushirikishwaji hafifu wa wamachinga katika michakato ya kupanga mipango miji na utungwaji wa sheria ndogo zinazogusa maslahi yao. Taratibu za mipango miji zinahitaji mchakato wa kupanga mji uwe shirikishi kwa kuzingatia maslahi ya watumiaji wote wa ardhi ila kinachofanyika ni kinyume. Kwa kuwa wamachinga hawaishi kwenye maeneo ya katikati ya miji wanakouzia bidhaa zao, basi hawashirikishwi kwenye vikao kwa hoja kuwa vikao hivyo vinahusisha wakazi pekee. Taratibu hizo huwatenga wamachinga ambao huja kufanya biashara asubuhi na jioni kurudi kwenye makazi yao pembezoni mwa miji.

(ii) Mamlaka za upangaji zimeshindwa kutekeleza kikamilifu malengo ya misingi mikuu ya *Sera ya Taifa ya Ardhi na Sera ya Maendeleo ya Makazi* kama ilivyoainishwa kwenye *Sheria za Mipango Miji*. Kifungu cha 3(c) cha *Sheria ya Mipango Miji* kinataka watu wote na mamlaka zinazosimamia utekelezaji wa *Sheria ya Mipango Miji* kuhakikisha utekelezaji wa mipango miji unatengeneza fursa za ajira na kupunguza umaskini.

Vilevile, kifungu 3(i) cha *Sheria ya Mipango Miji* kinahakikisha kuwa sheria za upangaji, kanuni za ujenzi na viwango zinakidhi mahitaji na maazimio ya makundi mbalimbali katika jamii. Vifungu hivi vimeshindwa kutekelezwa na hili linajidhihirisha wazi kwa mipango miji mingi kutoweka vipaumbele vya kutenga au kutambua maeneo ya wamachinga kufanya biashara.

(iii) Uwepo wa sheria ndogo na mapendekezo ya sheria ndogo ambayo yana lengo la kuharamisha shughuli za wamachinga mjini. Sheria ndogo mbalimbali ikiwemo zile zinazohusu udhibiti wa taka na utunzaji wa mazingira; uratibu na usimamizi wa wamachinga; na afya na usimamizi wa mazingira zimekuwa zikitumika kudhibiti shughuli za wamachinga kutokana na wengi wao kushtakiwa kwa makosa yanayotokana na sheria hizo.

(iv) Kumekuwepo na matamko na maamuzi mbalimbali ambayo yanatolewa na viongozi wa serikali ambayo yamekuwa na athari kwa shughuli za wamachinga. Kwa mfano, katika awamu ya tano, maamuzi ya serikali yalitengeneza fursa kwa wamachinga kufanya biashara katika maeneo ya katikati mwa miji bila kufukuzwa lakini serikali ya awamu ya sita imefanya uamuzi wa kuwafukuza wamachinga kutoka katika maeneo ya katikati mwa miji na kuwapeleka pembezoni. Hatua hii imekuwa na athari hasi kwa shughuli zao ambazo kwa kawaida hufanyika kwenye maeneo ambayo yana mikusanyiko ya watu kama vile eneo la Kariakoo, Karume, na kwenye kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani kijulikanacho kama Stendi ya Mabasi ya Magufuli.

(v) Kukosekana na mfumo thabiti wa ushirikishwaji ambao hupelekea wamachinga kuishia kuwa wapokeaji wa maamuzi badala ya kushiriki katika utoaji wa maamuzi ya masuala yanayohusu maslahi yao. Kundi la wamachinga limekuwa likipokea tu maelezo kutoka kwa wenye mamlaka kuhusu utaratibu wa kuendesha biashara zao bila ya wao kushiriki kwenye uamuzi uliofanywa.

Kwa mfano, uamuzi wa kujengwa kwa jengo la kufanyia biashara jijini Dar es Salaam maarufu kama *Machinga Complex*

halikushirikisha wala kuchukua maoni ya walengwa ambao ni wamachinga na matokeo yake mpaka leo bado jengo hilo halitumiki jinsi ilivyokusudiwa kutokana na kutoendana na mahitaji halisi ya wamachinga wenyewe.

(vi) Mipango miji kutozingatia matumizi ya ardhi ya makundi ya watumiaji wote wa ardhi kwenye eneo husika. *Sheria ya Mipango Miji* na hasa kanuni zake[56] , zimeanisha matumizi mbalimbali ya ardhi kwenye mipango miji ikiwemo kutengwa kwa maeneo ya biashara na viwango vya ukubwa wa maeneo hayo. Ukiangalia mipango miji inayotengenezwa maeneo mbalimbali nchini haijatenga maeneo ya wamachinga. Hii inatokana na wamachinga kutoshirikishwa wakati wa uandaaji wa mipango hiyo.

## Hitimisho

Uchambuzi katika sura hii umeainisha kwa kina masuala ya msingi kuhusu ardhi na mipango miji nchini kwa kuangalia sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali iliyotungwa kusimamia masuala ya ardhi na mipango miji. Suala dhahiri linalojitokeza ni namna ambavyo nyaraka hizo zinatumika kama nyenzo ya kulinda maslahi ya tabaka tawala huku zikiendelea kuwakandamiza wazalishaji wadogo

[56]*Urban Planning (Use Groups and Use Classes) Regulations, 2018 na The Urban Planning (Planning Space Standards) Regulations, 2018.*

wakiwemo wamachinga. Pia, ni wazi kuwa mchakato wa utungwaji wa sheria hizi unaendeleza misingi ile ile ya ukoloni kwa kutozingatia ushirikishwaji na maoni ya wazalishaji wadogo. Hii hupelekea utungwaji wa kanuni na miongozo kandamizi, ambayo huishia kuwatoza wazalishaji/wasambazaji wadogo, na hasa wamachinga, faini kubwa ambazo wengine hushindwa kuzilipa na kuishia jela huku wakipoteza mali zao zote kutokana na kutaifishwa na warasimu. Ipo haja ya wamachinga kuendelea kupaza sauti zao na kuungana ili kuongeza nguvu ya pamoja katika kupambana dhidi ya sera, sheria, kanuni na miongozo kandamizi ambayo inatweza utu wao na kuathiri mifumo yao ya kujipatia kipato halali kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kila siku.




Wamachinga wakiandamana kupinga bomoa bomoa iliyofanyika mwishoni mwa 2021.

# SURA YA 4

# Dhana na Misingi ya Haki-Jiji

SABATHO NYAMSENDA

**Utangulizi**

Sura hii inatoa ufafanuzi kuhusu dhana ya haki-jiji. Inatofautisha kati mitazamo miwili juu ya haki-jiji: mtazamo wa kimageuzi na ule wa kimapinduzi. Inatoa hoja kuwa, kwa kujifunza kutokana na mapambano ya wamachinga, dhana ya haki-jiji ndiyo imebeba maono, matamanio na kilio cha wavujajasho katika

majiji, ambao ndio wengi. Japokuwa wanaharakati wa kimaendeleo walio wengi wameukumbatia mtazamo wa kimageuzi wa haki-jiji huku wanazuoni wa mrengo wa kushoto wakishikilia ule wa kimapinduzi, sura hii inatoa hoja kwamba hakuna haja ya wavujajasho kuchagua mtazamo mmoja kati ya hiyo miwili (*either... or*) bali waitumie yote kwa pamoja (*both*): mtazamo wa kimapinduzi ukiwa ni kituo kikuu cha mwisho wakati mtazamo wa kimageuzi ukiwa ni kituo kidogo cha njiani. Yaani, mwisho wa safari yao ya mapambano uwe ni kufanikisha kuisimika haki-jiji ya kimapinduzi, japo katikati ya safari wanaweza kufanikiwa kulilazimisha dola kufanya mabadiliko yanayoongozwa na mtazamo wa kimageuzi ya haki-jiji.

## Mitazamo Miwili ya Haki-Jiji

Tofauti na wataalamu wa mipango miji ambao hulitazama jiji kutokea juu (kwa kutumia ramani na picha za satelaiti), wavujajasho hulitazama jiji kutokea chini, wakiyatazama maeneo yanayowazunguka. Wavujajasho huumizwa na dhuluma kuu ifanyikayo katika jiji ambalo limejengwa, kustawishwa na kuhudumiwa kwa jasho na damu yao. Lakini kwa nini hawana haki ya kufurahia, kujipatia maisha na kushiriki kufanya maamuzi katika jiji hilo? Hivyo, wavujajasho hutoa madai na hupambana kupata haki yao katika jiji.

Mtazamo wa wavujajasho kuhusu jiji umejengwa kwenye msingi wa mapambano na haki. Mapambano

yanahusu wavujajasho kubaki ndani ya jiji, kujipatia riziki kupitia fursa zipatikanazo ndani ya jiji, kudai huduma bora ndani ya jiji na kuwa na maamuzi kuhusu namna jiji linavyopangwa, kujengwa na kuendeshwa. Ndio maana, hata wakitimuliwa kwa virungu na mitutu watarudi tu kwani wanaliona jiji ni haki yao na kwa hiyo wanapambana kuisimika haki hiyo, ambayo watawala na mabepari hawaitambui. Kila uchao, watawala na mabepari huongeza vitisho, hadaa na ukatili ili kuwapora wavujajasho haki yao ya kuwepo katika jiji. Lakini wavujajasho hawakati tamaa bali wanaendelea kupambana kubaki katika jiji. Hivyo, jiji hugeuka kuwa uwanja wa mapambano.

Tabaka la wavujajasho ni tabaka ambalo limejaa ubunifu wa hali ya juu. Kila mara watawala wanapozidisha ukatili dhidi yao, wavujajasho hubuni mbinu mpya ya mapambano itakayowafanya waendelee kuwepo katika jiji na kufaidika na fursa zitolewazo na jiji. Mvujajasho ni mtu ambaye, ukimpora embe tamu na kumbakizia ndimu chachu basi atatengeneza sharubati ya ndimu na kuitia madoido ikawa tamu kiasi cha kumfanya yule bepari mlafi au mshika dola fisadi aliyemnyang'anya embe arudi tena na kumnyang'anya hiyo ndimu alimradi tu mvujajasho abaki hohe hahe, asiye na a wala ba. Upambanaji na ubunifu wa wavujajasho ndio unaopaswa kuamua kuhusu hatma ya jiji. Na tukitumia kigezo cha idadi, kwa kuwa wavujajasho ndio wengi basi ndoto, matamanio na mahitaji yao ndiyo yanayopaswa kuongoza namna jiji linavyopaswa

kuendelezwa na kuendeshwa. Kwa hiyo, haki-jiji ni haki ya wavujajasho kuishi na kufurahia uwepo wao katika jiji pamoja na kushiriki moja kwa moja katika uendeshaji na ustawishaji wa jiji hilo.

Ipo mitazamo miwili ya haki-jiji: mmoja ni wa kimageuzi na mwingine ni wa kimapinduzi. Mapinduzi hulenga kubomoa mfumo kandamizi unaowapora wavujajasho haki yao ya kuwemo katika jiji ili kujenga mfumo mpya unaozingatia utu, haki, uhuru na usawa. Mageuzi hulenga kufanya maboresho kidogo katika mfumo kandamizi ili kuleta unafuu kwa wanyonge. Katika mfumo wa kimapinduzi, wale waliokuwa wakikandamizwa ndio hushika hatamu. Katika mfumo wa kimageuzi, wakandamizaji huendelea kushika hatamu. Mitazamo hii miwili kuhusu haki-jiji imefafanuliwa hapa chini.

## Haki-jiji kwa Mtazamo wa Kimageuzi

Kwa mujibu wa taasisi ijulikanayo kama *Global Platform for the Right to the City*, haki-jiji ni "haki ya wakazi wote, wa sasa na wajao, wa muda na wa kudumu, kuishi, kutumia, kukalia, kuzalisha, kushiriki katika maamuzi na kufurahia majiji, vijiji na makazi ya watu yaliyo jumuishi, salama na endelevu, ambayo yanatafsiriwa kama mali ya pamoja (*commons*) ambayo ni muhimu kwa maisha timilifu na ya staha."

Haki-jiji ni haki ya pamoja yaani *collective right*. Inalitazama jiji kama milki ya pamoja inayopaswa

kuwanufaisha watu wote (*common good*) waishio na kufanya kazi katika jiji.

Kwa hiyo, kwa mtazamo wa kimageuzi, dhana ya haki-jiji ina vipengele kadhaa:

(i) *Hakuna ubaguzi*: Jiji lisilo na ubaguzi kwa wakazi wake kwa misingi ya kabila, rangi, dini, kipato, jinsia, utamaduni, n.k.

(ii) *Usawa wa kijinsia*: Jiji linaloheshimu, kuzingatia na kutekeleza usawa wa kijinsia. Hatua zinachukuliwa kuondoa ubaguzi, udhalilishaji na uonevu wa watoto wa kike na wanawake.

(iii) *Uraia jumuishi*: Jiji linalotoa haki sawa za uraia kwa wote. Watu wote wanaoishi, kupita au kufanya kazi katika jiji wanapaswa kupewa haki zao zote za kiraia.

(iv) *Kuimarisha ushiriki wa kisiasa*: Watu wote wanaoishi au kufanya kazi katika jiji wana haki ya kushiriki katika ufanyaji wa maamuzi ya msingi kama upangaji na upitishaji wa bajeti, mipango miji na maamuzi mengine yote.

(v) *Utimizaji wa majukumu ya kijamii*: Jiji linalotimiza majukumu yake ya kijamii kwa kuhakikisha wakazi wake wote

wanapata makazi bora na huduma nyingine zinazopatikana ndani ya jiji kwa usawa.

(vi) *Uchumi jumuishi*: Jiji linalotoa uhakika katika upatikanaji wa vyanzo vya maisha na kazi za staha kwa watu wote.

(vii) *Utoaji wa huduma bora za kijamii na maeneo ya umma*: Jiji linalozingatia haki-jiji linapaswa kutoa huduma bora za kijamii kwa watu wote pamoja na kuwa na maeneo ya wazi ya umma yanayotumiwa na watu wote kwa ajili ya kupumzika, kufanyia shughuli za kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Pia, jiji linapaswa kuwa na maeneo ya wazi ya umma yanayotumiwa na watu wa kipato cha chini kwa ajili ya kujitafutia riziki.

(viii) *Mahusiano jumuishi kati ya miji na vijiji*: Jiji linalojenga mahusiano jumuishi kati ya miji na vijiji kwa lengo la kuhakikisha kuwa mahusiano hayo yanawafaidisha watu wa tabaka la chini mijini na vijijini, kuimarisha uhuru wa chakula na kulinda mazingira na bayoanuai.

Dhana ya kimageuzi ya haki-jiji hulipatia dola wajibu wa kuiweka haki-jiji katika vitendo kupitia sera, sheria pamoja na utekelezaji wake. Kwa hiyo, katika mtazamo wa kimageuzi, haki-jiji huhesabiwa kama haki nyingine za binadamu (*human rights*) inayopaswa

kutekelezwa na dola. Kama inavyoonyeshwa hapa chini, baadhi ya serikali pamoja na mashirika ya kimataifa yamekubali msukumo wa asasi za kiraia na hata kupitisha sera, sheria na maazimio kwa ajili ya kutambua na/au kutekeleza haki-jiji.

## Maazimio ya Kimataifa

Mojawapo ya maazimio yaliyopitishwa na asasi za kiraia ni Mkataba wa Ulimwengu juu ya Haki-Jiji (*World Charter for the Right to the City*)[57]: Mkataba huu ulipitishwa mwaka 2005 katika Jukwaa la Kijamii Duniani (*World Social Forum*) lililofanyika jijini Porto Alegre, Ufaransa. Jukwaa hilo hukutanisha mavuguvugu ya kijamii pamoja na asasi zisizo za kiserikali kutoka sehemu mbalimbali duniani kwa ajili ya kupigania mageuzi yanayotoa haki kwa wavujajasho. Kati ya matatizo ambayo mkataba huo unayataja ni:

> *kukithiri kwa timua timua ya watu wa tabaka la chini, kuongezeka kwa sera zilizotungwa kwa ajili ya kuzuia watu wa tabaka la chini kuwepo katika jiji na kutumia maeneo ya jiji, na kuongezeka kwa ubaguzi wa kijamii unaofanya ukatili kwa maisha ya jiji na kupuuza mchango wa wavujajasho katika ujenzi wa jiji na uraia."*[58]

[57]World Social Forum, "World Charter for the Right to the City," *Global Platform for the Right to the City*. Imepatikana Septemba 15, 2022 kutoka https://www.right2city.org/document/world-charter-for-the-right-to-the-city/

[58]Kama hapo juu.

Ibara mbili za mwanzo za mkataba huo zinahusu haki-jiji na misingi yake. Misingi mikuu ya haki-jiji iliyowekwa katika ibara ya 2 ya mkataba huo ni: haki ya kutimiza kikamilifu majukumu ya kiraia na uendeshaji wa kidemokrasia wa jiji; jiji kutimiza wajibu wa kijamii kupitia rasilimali zake (zitakazotoa uhakika kwa wakazi wote wa jiji kuwa na haki ya kutumia na kunufaika na rasilimali hizo kwa usawa); kujenga usawa na kuondoa ubaguzi wa aina zote; kutoa ulinzi maalumu kwa makundi na watu wanaoishi katika mazingira magumu; sekta binafsi kusaidia utekelezaji wa shughuli za kijamii, na jiji kusaidia katika kuhamasisha na kukuza uchumi wa mshikamano na sera za kimaendeleo za kodi. Ibara ya 3 hadi ya 5 zinaipatia serikali ya jiji wajibu wa kuweka mifumo itakayohakikisha usawa, maendeleo endelevu pamoja na ushiriki wa wananchi katika upangaji, uendeshaji na uendelezaji wa jiji. Kuanzia ibara ya 6 hadi 11, mkataba huo unaweka haki zifuatazo kwa wakazi wa jiji: haki ya kupata taarifa za umma; haki ya uhuru na heshima; haki ya wakazi wa jiji kushiriki katika maamuzi ya kisiasa moja kwa moja na/au kupitia wawakilishi; haki ya kuuda jumuiya, kukusanyika, kuandamana na kutumia maeneo ya umma kwa ajili ya hiyo; haki ya kutendewa haki katika vyombo vya kisheria na jiji kuweka mifumo ya ulinzi wa umma, maendeleo ya pamoja na mshikamano miongoni mwa wakazi wake.

Haki zingine zilizomo katika Mkataba wa Ulimwengu juu ya Haki-Jiji ni pamoja na haki ya kupata huduma za

kijamii kama maji safi na salama, nishati, mawasiliano ya simu, huduma za utoaji wa maji-taka, pamoja na miundombinu ya huduma za afya, elimu, usambazaji wa mahitaji ya msingi, na maeneo ya kupumzika. Haki za kupata huduma za usafiri na kwenda mahali popote mtu atakapo katika jiji nazo zimewekwa katika mkataba huu, kama zilivyo pia haki ya kufanya kazi, haki ya kupata makazi, na haki ya kuishi katika mazingira salama na endelevu.

Azimio lingine la kimataifa ni Mkataba wa Ulaya Kwa Ajili ya Kulinda Haki za Binadamu katika Jiji (*The European Charter for the Safeguarding of Human Rights in the City*) uliopitishwa mwaka 2001 katika eneo la Saint Denis, jijini Paris, Ufaransa. Hadi kufikia mwaka 2018, inasemekana mamlaka za majiji zipatazo 30 barani Ulaya zilikuwa zimeridhia mkataba huo na kuanza utekelezaji wake. Misingi mikuu na vipengele vya mkataba wa Ulaya vinafanana kwa kiasi kikubwa na vile vya Mkataba wa Ulimwengu ambao umechambuliwa hapo juu.

## Umoja wa Mataifa na Ajenda Mpya ya Miji

Ajenda Mpya ya Miji (*New Urban Agenda*) ilipitishwa na Kongamano la Tatu la Umoja wa Mataifa juu ya Makazi na Maendeleo Endelevu ya Miji (*Habitat III*) uliofanyika mjini Quito, Ecuador kuanzia tarehe 17 hadi 20 Octoba 2016. Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa liliidhinisha Ajenda hiyo tarehe 23 Desemba 2016. Kama ambavyo andiko juu ya *Ajenda Mpya ya Miji*

linavyojieleza, ukuaji wa miji duniani unakabiliwa na matatizo kadhaa, yakiwemo kukua kwa matabaka, ubaguzi wa kiuchumi pamoja na ubaguzi katika utumiaji wa maeneo ya miji, huku watu wa kipato cha chini wakiwa wahanga wakuu wa matatizo hayo[59] . Kupitia *Ajenda Mpya ya Miji*, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ziliahidi kufanya mabadiliko makubwa ya fikra na mtazamo (*paradigm shift*) juu ya namna miji inavyopangwa na kuendeshwa ili kuleta haki na usawa kwa makundi yaliyo pembezoni. Dira inayoongoza Ajenda hiyo ni haki-jiji na ina lengo la kujenga majiji kwa ajili ya wote (*cities for all*) ambapo wakazi wote, wa sasa na baadaye, wanakuwa na haki sawa katika kutumia, kufurahia na kuendeleza majiji na makazi ya binadamu kwa ajili ya maisha bora kwa wote. Misingi ya mtazamo wa kimageuzi wa haki-jiji iliyo katika maazimio mengine ya kimataifa, imo pia katika Ajenda hiyo. Katika vifungu vya 17 hadi 22, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa wanaweka dhamira ya kutekeleza Ajenda Mpya ya Miji katika nchi zao wakiweka wazi kuwa Ajenda hiyo ni "dira ya pamoja na dhamira ya kisiasa katika kuchavisha na kufanikisha maendeleo endelevu mijini."[60]

Ukiachilia mbali Ajenda Mpya ya Miji, lengo la 11 kitika Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals*) nalo limelenga kupatikana kwa majiji ya wote kufikia mwaka 2030.

[59]United Nations, *New Urban Agenda* (Qiuto: Habitat III Secretariat, 2017).

[60]Kama hapo juu, uk. 11.

## Sheria ya Jiji (*City Statute*) nchini Brazil

Sheria ya Jiji (*City Statute*), iliyopitishwa mwaka 2001 nchini Brazil, ni zao la mapambano ya kudai haki-jiji yaliyoongozwa na mavuguvugu ya wavujajasho wa mijini. Kwa upande wa kisiasa, kulikuwa na Chama cha Wafanyakazi (*Partido dos Trabalhadores - PT*), chini ya uongozi wa Lula da Silva, ambacho kilibeba ajenda za wavujajasho katika kupigania mageuzi. Kwa upande wa kijamii, asasi iliyoitwa Vuguvugu la Kitaifa la Kudai Mageuzi ya Miji (*Movimento Nacional de Reforma Urbana - MNRU*) iliundwa mwaka 1982, ikileta pamoja jumuiya za mashinani, vyama vya wavujajasho, asasi zisizo za kiserikali, vyama vya wafanyakazi, n.k. Mapambano ya muda mrefu yaliyoongozwa na mavuguvugu haya yalipelekea kutambuliwa kwa haki-jiji katika 'katiba mpya' ya Brazil iliyopitishwa mwaka 1988. Ibara namba 5, 182 na 183 za Katiba hiyo zinatamka ardhi/mali kutumika kwa manufaa ya kijamii. Manispaa ambazo ndizo hupewa jukumu la mipango miji zinatakiwa kuhakikisha kuwa mipango miji inakuwa shirikishi na kwamba ardhi, kama rasilimali, iwe na manufaa ya kijamii[61].

Kutokana na kuwa sehemu ya vuguvugu la kudai haki-jiji, chama cha PT kilipochaguliwa kuongoza halmashauri za majiji ya Porto Alegre na Belo Horizante miaka ya 1980, kilianza kutekeleza mageuzi ya haki-

[61]Abigail Friendly, "The Place of Social Citizenship and Property Rights in Brazil's 'Right to the City' Debate," *Social Policy and Society* 19, Na.2 (2020).

jiji. Majiji yaliyoongozwa na PT yalisifika kwa kuwa na mifumo ya demokrasia shirikishi katika utengenezaji wa bajeti na upangaji wa miji[62]. Mfumo shirikishi wa utengenezaji wa bajeti (*participatory budgeting*) uliotekelezwa na chama cha PT ulijizolea sifa duniani kote kwa namna ulivyowezesha wananchi kuweka vipaumbele vyao katika mgawanyo wa rasilimali za jiji. Majiji yaliyotekeleza mfumo huo yalipata matokeo ya aina mbili: mosi, sehemu kubwa ya bajeti katika majiji hayo ilienda kutoa huduma za kijamii na kutimiza mahitaji ya wananchi wa tabaka la chini. Pili, hali ya maisha kwa wananchi wa tabaka la chini ilizidi kuwa bora zaidi. Kwa mfano, vifo vya watoto wachanga vilipungua kwa asilimia 10 hadi 20 katika majiji hayo, ukilinganisha na majiji ambayo hayakufuata mfumo wa bajeti shirikishi[63].

Mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa mageuzi ya haki-jiji katika majiji yaliyoongozwa na chama cha PT ulizidi kuchochea moto vuguvugu la kudai sheria ya jiji kitaifa ndani ya Brazil. Hatimaye, mwaka 2001, Sheria ya Jiji ilipitishwa kwa ajili ya kuweka miongozo ya kisheria na mifumo ya utekelezaji wa haki-jiji ambayo ilikuwa imesimikwa na katiba ya mwaka 1988, yaani mipango miji shirikishi na mali/ardhi kutimiza

---

[62]William R. Nylen, "The Making of Loyal Opposition: The Workers' Party (PT) and the Consolidation of Democracy in Brazil," in *Democratic Brazil: Actors, Institutions, and Processes*, eds. P. Kingstone na T.J. Power (Pittsburgh: University of Pittsburgh Press, 2000).

[63]Sónia Gonçalves, "The Effects of Participatory Budgeting on Municipal Expenditures and Infant Mortality in Brazil," World Development 53 (2014).

mahitaji ya kijamii[64].

Ifahamike kuwa Katiba ya 1988 na Sheria ya Jiji ya 2001 havikukomesha umiliki binafsi wa mali/ardhi bali viliweka misingi ya kudhibiti mali binafsi ili kuongeza manufaa kwa jamii. Vivyo hivyo, havikuondoa uwepo wa dola bali viliiongezea wigo wa ushiriki wa wananchi katika upangaji na uendeshaji wa jiji.

## Sheria ya Wamachinga Nchini India

Sheria ya Wamachinga nchini India ilipitishwa mwaka 2014. Kupitishwa kwa sheria hiyo kulikuwa kielelezo cha mafanikio ya mapambano ya vyama vya wamachinga, ambavyo vilipigania kutungwa kwa sera na sheria ya wamachinga. Vyama vitatu vya wamachinga vilivyokuwa mstari wa mbele katika mapambano ni Shirikisho la Wamachinga (*National Hawker Federation - NHF*), Umoja wa Wamachinga India (*National Association of Street Vendors of India - NASVI*) na Umoja wa Wanawake Waliojiajiri (*Self-Employed Women's Association - SEWA*). Muongo mmoja kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya Wamachinga, vyama hivyo vilifanikisha kutungwa na kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Wamachinga wa Mijini (*National Policy on Urban Street Vendors*) ya mwaka 2004, ambayo ilihuishwa na kutolewa upya mwaka 2009. Kabla ya kuchambua sera na sheria tajwa ni vema kudurusu,

[64]Abigail Friendly, "The Right to the City: Theory and Practice in Brazil," *Planning Theory & Practice* 14, Na. 2 (2013).

japo kwa ufupi, historia ya mapambano ya haki-jiji nchini India iliyofanikisha upitishwaji wa sera na sheria hizo.

*Hukumu za Mahakama Kuu*

Safari ya kupambania wamachinga kutambulika kisheria nchini India ilikuwa ndefu, ikianza na mapambano ya kisheria katika vyombo vya utoaji haki. Katika kipindi cha miaka ya mwisho ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980, mhimili wa mahakama nchini India uligubikwa na mashauri mengi yenye lengo la kutetea haki za umma yaliyojulikana kwa Kiingereza kama *public interest litigation au social action litigation*. Kufunguliwa kwa mashauri hayo kuliuchochea mhimili wa mahakama kutoa maamuzi yaliyolenga kutimiza haki za wanyonge, kiasi cha kuwafanya majaji kuonekana kama wakijihusisha na harakati za kimahakama (*judicial activism*). Hata hivyo, hali ilikuja kubadilika kuanzia miaka ya 1990 ambapo India, kama zilivyo nchi nyingine, ilianza kutekeleza mageuzi ya soko huria na mahakama nazo zikaanza kutoa maamuzi yaliyoegemea katika kutetea maslahi ya matabaka ya juu[65].

Mwaka 1985, Mahakama Kuu ya India ilitoa hukumu katika mashauri mawili. Shauri la kwanza ni lile lililofunguliwa na Olga Tellis dhidi ya Shirika la

[65]Joshi, K., "'Conditional' Citizens? Hawkers in the Streets (and the Courts) of Contemporary India." *Journal of Urban Research* 17-18 (2018).

Manispaa ya Bombay[66] mwaka 1981 na kutolewa hukumu miaka minne baadaye ambapo Mahakama Kuu ilitoa tafsiri ya haki ya kuishi (inayolindwa na ibara ya 21 ya Katiba ya India) inayojumuisha haki ya mafukara wa mijini kuishi na kujipatia kipato katika maeneo ya wazi. Mahakama ilitamka kuwa "hakuna mtu anayeweza kuishi bila chanzo cha maisha, yaani chanzo cha kujikimu" (*no person can live without the means of living i.e. the means of livelihood*). Hukumu ya pili ni ile ya shauri la Umoja wa Wamachinga wa Jiji la Bombay dhidi ya Shirika la Manispaa ya Bombay, ambapo Mahakama Kuu ya India ilitambua umachinga kama kazi inayolindwa kikatiba na kuweka utaratibu wa kutoa leseni na kuratibu sekta ya umachinga.

Mwaka 1989, Mahakama Kuu ya India ilitoa hukumu katika shauri lililofunguliwa na Sodan Singh dhidi ya Kamati ya Manispaa ya Jiji la New Delhi[67]. Mahakama Kuu ilisisitiza kuwa haki ya kufanya kazi au biashara imelindwa katika Ibara ya 19(1)(g) ya Katiba. Mahakama ikatamka kuwa, iwapo kutakuwa na uratibu mzuri wa sekta ya umachinga, haki ya wamachinga kutumia maeneo ya kando kando ya barabara "haiwezi kukiukwa kwa hoja kwamba barabara za mitaa zipo kwa ajili ya kupita na sio kwa ajili ya matumizi mengine"[68]. Mahakama ikaenda mbali na kutamka kwamba "hakuna sababu inayoweza kuhalalisha

---

[66]*Olga Tellis v. Bombay Municipal Corporation, 1985.*

[67]*Sodan Singh v. New Delhi Municipal Committee, 1989*

[68]Imenukuliwa kutoka Shalini Sinha and Sally Roever, "India's National Policy on Urban Street Vendors," WIEGO Policy Brief (Urban Policies) No. 2 (2011).

ukiukwaji wa haki ya wananchi kujitafutia riziki kwa kutumia maeneo ya wazi ya mitaa kwa ajili ya biashara."[69]

*Azimio la Bellagio*

Mbali na kupigania haki zao kupitia mahakama, wamachinga wa India waliungana na wenzao kutoka nchi zingine ili kuendeleza mapambano katika ngazi ya kimataifa. Mwaka 1995, wawakilishi wa wamachinga kutoka mabara yote walikutana katika jiji la Bellagio nchini Italia ambapo walitangaza Azimio la Bellagio (*The Bellagio International Declaration of Street Vendors*). Azimio hilo lililopitishwa November 23, 1995 lilizitaka serikali kupitisha sera ya wamachinga kwa ajili ya kutambua na kutoa ulinzi wa kisheria kwa wamachinga na shughuli zao. Azimio la Bellagio lilizidi kuchochea vuguvugu la wamachinga nchini India, kwani baada ya kupitishwa kwake ndipo vyama vya wamachinga vya kijimbo vilipoungana na kuunda vyama vya kitaifa kwa ajili ya kudai sera ya wamachinga. Chama cha NASVI kiliundwa mwaka 1998 na kusajiliwa rasmi miaka mitano baadaye[70].

*Sera ya Wamachinga*

Serikali ya India ilikubali madai ya kutungwa kwa sera ya wamachinga mwaka 2001 ambapo iliunda

[69]Kama hapo juu.

[70]Kama hapo juu.

kikosi kazi kwa ajili ya kuandika sera hiyo. Kikosi kazi kilijumuisha wawakilishi kutoka taasisi za wamachinga kama SEWA na NASVI. Kikosi kazi kilifanya kazi yake na hatimaye sera ya wamachinga ikapitishwa mwaka 2004. Hata hivyo, kutokana na malalamiko ya wamachinga kwamba sera hiyo haikutoa ulinzi wa kutosha, sera hiyo ilifanyiwa mapitio na hivyo kupelekea kutolewa kwa sera mpya ya wamachinga mwaka 2009.

Kipengele namba 1.3 cha Sera ya Taifa ya Wamachinga wa Mijini ya mwaka 2009 imeitambua misingi ya haki-jiji iliyosimikwa na Mahakama Kuu ya India katika hukumu ya Sodan Singh dhidi ya Kamati ya Manispaa ya Jiji la New Delhi ya mwaka 1989 iliyonukuliwa hapo awali[71]. Kwa kufuata misingi hiyo, pamoja na haki ya kufanya kazi iliyowekwa na Katiba ya India, Sera ya Wamachinga inawatambua wamachinga na mchango wao katika kutoa ajira na kupambana na umaskini, pamoja na kuihudumia jamii kupitia usambazaji wa bidhaa na huduma kwa bei rahisi na katika maeneo yanayofikika kirahisi. Sera hiyo inajiwekea malengo kadhaa[72], yakiwemo:

(i) Kutungwa kwa sheria itakayowatambua na kuwalinda wamachinga kwa pamoja ikiwa ni pamoja na ikiwa pamoja na kuhuisha mipango ya maendeleo na uendelezaji miji ili

[71]Government of India, *National Policy on Urban Street Vendors, 2009* (New Delhi: Ministry of Housing & Urban Poverty Alleviation, 2009), 1.

[72]Kama hapo juu.

itambue masoko asilia yaliyo pembezoni mwa barabara yanayotumiwa na wamachinga.

(ii) Kuunda mfumo shirikishi wa maamuzi unaojumuisha wawakilishi wa wamachinga, serikali pamoja na asasi za kiraia.

(iii) Kusaidia uundwaji wa vyama na jumuiya za wamachinga kwa ajili ya kuwaunganisha wamachinga na kuboresha ustawi wao.

(iv) Kusaidia uundwaji wa mfumo wa uratibu wa pamoja utakaowapatia wamachinga nafasi ya kujiratibu wenyewe katika maeneo wanayofanyia kazi.

(v) Kutoa huduma za kijamii katika maeneo yanayotumiwa na wamachinga.

(vi) Kufuta mfumo wa leseni ambazo hutolewa kwa matakwa ya serikali na kuanzisha mfumo wa vitambulisho vya wamachinga ambao utampatia haki kila mmachinga anaefanya kazi mwenyewe au kwa kusaidiana na wanafamilia wake.

Baada ya kupitishwa kwa sera hiyo, mapambano yaliendelea kuweka shinikizo kwa serikali za majimbo kuiridhia na kuanza utekelezaji wake pamoja na kuilazimisha serikali kuu ya India kutunga Sheria ya Wamachinga iliyotajwa kwenye sera. Mapambano hayo

yalichukua sura mbalimbali, ikiwemo maandamano na mashauri katika mahakama.

*Sheria ya Wamachinga*

Sheria ya Wamachinga (*Street Vendors [Protection of Livelihood and Regulation of Street Vending] Act, 2014*) iliyopitishwa mwaka 2014 inatoa ulinzi wa kisheria kwa wamachinga na shughuli zao. Baadhi ya mambo ya msingi yaliyomo katika sheria hiyo ni pamoja na haki na wajibu wa mmachinga; vyombo shirikishi vya kuteua maeneo ya wamachinga; mifumo ya utatuzi wa malalamiko ya wamachinga pamoja na taratibu za kufuata katika kuwahamisha wamachinga. Kifungu cha 27 kinaweka zuio kwa vyombo vya mabavu na mamlaka za serikali kuwanyanyasa wamachinga wanaofanya shughuli zao kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria ya Wamachinga.

Chombo kikuu katika uratibu wa sekta ya umachinga ni Kamati ya Kuratibu Umachinga (*Town Vending Committee - TVS*) inayopaswa kuanzishwa katika kila ngazi ya utawala, kuanzia ngazi ya eneo, mtaa, kata, wilaya na hata jimbo. Asilimia 40 ya wajumbe wa TVS watakuwa wamachinga. Pamoja na kufanya uamuzi juu ya maeneo ya kando kando mwa barabara yanayofaa kwa umachinga katika eneo husika, kamati hiyo imepewa jukumu la kufanya sensa ya wamachinga katika maeneo yao na kutoa cheti/kitambulisho kwa mmachinga. Mmachinga anayepewa kitambulisho ni yule anayetimiza

masharti yafuatayo: (i) awe anaendesha biashara yeye mwenyewe au mwanafamilia wake (ii) asiwe na chanzo kingine cha mapato (iii) hatauza au kukodisha cheti chake (na kwa maana hiyo eneo alilopangiwa kufanyia shughuli) kwa mtu mwingine. Masharti haya, yaliyowekwa katika kifungu cha 5 cha Sheria ya Wamachinga, yana lengo kuhakikisha kuwa maeneo ya wamachinga hayavamiwi na watu wenye nguvu za kiuchumi au madalali wa kukodisha/kuuza maeneo.

## Haki Jiji kwa Mtazamo wa Kimapinduzi

Dhana ya *haki-jiji* ilitumiwa kwa mara ya kwanza na mwanazuoni wa kimapinduzi kutoka Ufaransa aliyeitwa Henri Lefebvre mwaka 1967. Mwanazuoni huyu aliukosoa mfumo wa kibepari na jiji linalozalishwa na mfumo huo, jiji lililojikita katika kuzalisha faida kwa ajili ya wachache huku wengi wakiishi maisha ya ufukara, jiji lililo chini ya utawala wa dola la kibepari linalowanyima watu walio wengi nafasi ya kufanya maamuzi juu ya matumizi ya maeneo ya jiji, mgawanyo wa rasilimali na uendeshaji wa jiji kwa ujumla.

Haki-jiji, Lefebvre aliandika, ni "kilio na dai" (*a cry and demand*) kwa wakati mmoja juu ya "haki ya kuishi katika mji iliyobadilishwa na kurejeshwa upya."[73] Maana yake ni kuwa kilio na dai la haki jiji havilengi

[73]Henri Lefebvre, *Writings on Cities* (Cambridge, MA: Blackwell Publishers, 1996), 158.

kurejesha jiji la zamani ambalo tayari limeshapotea bali jiji jipya na mfumo mpya wa maisha ambao unaweka mbele watu badala ya faida. Wenye kudai haki hiyo ni wakazi (*inhabitants*) ambao maisha yao ya kila siku yapo katika jiji hilo. Katika fikra za Lefebvre, ni tabaka la wavujajasho ndio wakazi halisi wa jiji, tofauti na mabepari na washika dola ambao siku zote ni watu wa kuzunguka, kutoka hoteli moja hadi nyingine, kasri moja hadi jingine, mji mmoja hadi mwingine na nchi moja hadi nyingine.

Kupata taswira ya *maisha ya kila siku* ya mkazi wa jiji, tumfikirie mama anaeamka asubuhi kutoka Mbezi Makabe: anakimbia kuwahi daladala kwa ajili ya kwenda kununua dagaa katika eneo la Ferry Posta kisha kwenda kuwakaanga na kuwauza katika eneo la pembezoni mwa barabara huko Goba. Anarudi nyumbani usiku akiwa amechoka ambapo anajipumzisha kwa saa chache kabla ya kurudia ratiba ile ile kwa siku inayofuata. Adha anazokutana nazo ni pamoja na msongamano wa watu katika vituo vya daladala, foleni za barabarani, kufukuzwa na mgambo ambaye anampora dagaa wake, n.k. Yawezekana pia mama huyu ni mgonjwa lakini hawezi kwenda hospitali kutibiwa kwa sababu hana fedha. Yawezekana amelazimika kupanga mbali na mahali anapojipatia kipato kwa sababu ya ukubwa wa kodi ya nyumba. Ndani ya taswira ya mateso anayoyapitia mama huyu ipo pia taswira ya mambo yanayopaswa kufanyika ili kuondoa mateso hayo. Taswira hiyo mbadala, iliyolenga katika kutimiza mahitaji ya watu

wa tabaka la chini, ndiyo taswira ya haki-jiji.

Ndio maana Peter Marcuse anaandika kuwa, "Haki-jiji haitoi madai ya haki zote kwa watu wote... viongozi wa kampuni kubwa za kibepari, matajiri na wenye mamlaka tayari wanazo haki zote wanazohitaji. Na katika mfumo wa kisheria uliopo wana haki nyingi kuliko wanazoweza kudai mbele ya sheria."[74] Kwa hiyo, kilio cha haki-jiji kinatoka kwa walalahoi ambao waliotengwa, kunyonywa na kupunjwa malipo na kuingizwa katika ajira za vibarua zisizo na malipo ya staha.

Haki-jiji, katika fikra za Lefebvre, ina nguzo kuu mbili: umiliki wa pamoja na maamuzi ya pamoja.

(i) *Umiliki wa Pamoja*

Umiliki wa pamoja wa maeneo ya jiji hulifanya jiji na maeneo yake kuwa mali ya pamoja inayotumika kwa manufaa ya wote. Maana yake ni kuwa wakazi wa jiji, na hasa wale wa kipato cha chini, hupata haki ya kutumia maeneo ya katikati ya jiji kwa ajili ya mambo mbalimbali kama vile kujitafutia riziki, kufanya shughuli za kijamii na kiutamaduni, n.k. Kwa hiyo, dhana ya kimapinduzi ya hakijiji ni kinyume cha dhana ya kibepari ya jiji ambayo hulifanya jiji na maeneo yake huwa milki ya watu wachache wenye

[74]Peter Marcuse, "Whose Right(s) to What City?" In *Cities for People, Not for Profit: Critical Urban Theory and the Right to the City,* eds, N. Brenner et al. (London and New York: Routledge, 2012), 35.

nguvu ya fedha na mamlaka ya kidola. Umiliki wa pamoja hufuta umiliki binafsi wa maeneo ya jiji na hivyo kuliweka jiji na maeneo yake katika mikono ya wengi. Umiliki binafsi hufaidisha wachache, umiliki wa pamoja hujenga ustawi wa wengi.

Katika umiliki binafsi wa kibepari, maeneo ya jiji huwa na thamani mauzo (*exchange value*) ilhali katika umiliki wa pamoja, maeneo ya jiji huwa na thamani mafao (*use value*). Thamani mauzo huyageuza maeneo ya jiji kuwa bidhaa na hivyo kuhodhiwa na kundi la wateule wachache wenye fedha au mamlaka ya dola na hutumika katika kusaidia ulimbikizaji wa mtaji wa tabaka la mabepari. Chukulia mfano wa maeneo ya katikati ya jiji: yamejengwa 'maghorofa' kwa ajili ya ofisi, 'mahoteli' ya nyota tano, maduka makubwa na makazi kwa ajili ya watu wenye fedha. Hata kama zikijengwa sehemu kwa ajili ya burudani na kupumzika nazo pia hugeuzwa bidhaa na chanzo cha kutengeneza faida kwa watu wachache. Kwa hakika, wanaofaidika na maeneo hayo ni kundi la wenye fedha.

Thamani mafao huyageuza maeneo ya jiji kuwa manufaa ya pamoja na hutumika kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya wavujajasho, ambao ndio wengi. Kwa mfano, japokuwa fukwe za bahari ni maeneo ya wazi chini ya umiliki wa serikali kumekuwa na msukumo mkubwa wa kuzibinafsisha. Na katika baadhi ya maeneo, tayari fukwe zimebinafsishwa kwa kujengwa hoteli za kitalii na makasri ya watu wenye

fedha. Ubinafsishaji wa fukwe ni kilelezo kimojawapo kinachodhihirisha jinsi umiliki binafsi unavyojali fedha na faida kwa maslahi ya wachache badala ya utu na mahitaji ya wengi. Iwapo fukwe zitawekwa katika umiliki wa pamoja bila shaka walio wengi hawatakubali kwamba ili kukanyaga mchanga laini na kupunga upepo mwanana wa baharini ni lazima mtu alipe fedha! Umiliki wa pamoja utayafanya maeneo haya yawe ni kwa manufaa ya wote.

Katika maeneo ya katikati ya jiji, wamachinga wanapotimuliwa, nafasi yao huchukuliwa na mwekezaji ambaye hukabidhiwa eneo hilo kwa ajili ya kujenga hoteli, kituo cha mafuta, ghala la kuhifadhi bidhaa au jengo la kupangisha. Je, ni kwa vipi wamachinga elfu tano wapoteze chanzo cha maisha ili tu kumwezesha mtu mmoja apate 'haki' ya kulimbikiza mtaji? Hayo yote ni kwa sababu ya mfumo wa uchumi uliojikita katika umiliki binafsi na thamani mauzo. Katika umiliki wa pamoja, wamachinga hao elfu tano ndio wangeamua hatma ya eneo husika na hakuna shaka kwamba wangechagua litumike kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya wengi badala ya kushibisha matumbo ya wachache.

(ii) *Ushiriki wa Pamoja*

Kupitia ushiriki wa pamoja, wavujajasho katika jiji hujenga mfumo mpya wa maamuzi unaowapa haki na nguvu ya kuamua kuhusu upangaji, ustawishaji na uendeshaji wa maeneo ya jiji. Maana yake ni kuwa

nguvu kuhusu upangaji, ustawishaji na uendelezaji wa miji huondolewa kutoka mikononi mwa dola na kuwekwa mikononi mwa wananchi walio wengi. Kama aandikavyo Profesa Mark Purcell:

> *Tofauti na demokrasia ya kiliberali ambayo kiasili haina ushiriki wa moja kwa moja wa wananchi ambapo sauti za wananchi huchakachuliwa kupitia taasisi za dola, haki-jiji hutoa uhakika wa wakazi wa jiji kushiriki moja kwa moja katika maamuzi yote yanayohusu uendelezaji wa maeneo ya jiji.*[75]

Kadiri wavujajasho wanavyoshiriki moja kwa moja katika maamuzi na kuunda vyombo mbadala vya ushirikishwaji basi haja ya uwepo wa dola kama chombo cha mabavu na maamuzi kutoka juu inafifishwa. Taratibu dola litaanza kupoteza umuhimu katika maisha ya wavujajasho na litaanza kutoweka kidogo kidogo. Kwa kupitia ushiriki wa pamoja, wavujajasho hujiongoza wenyewe (*self-management*) kwa kushiriki moja kwa moja katika maamuzi ya muhimu yanayohusu jiji lao na nchi yao, yakiwemo maamuzi juu ya vipi, kwa namna gani na kwa faida ya nani maeneo ya jiji yanapaswa kupangwa, kujengwa na kuendeshwa[76]. Watu wote hushiriki kupanga, kustawisha, kuendesha na kuliendeleza jiji kwa

[75]Mark Purcell, "Excavating Lefebvre: The Right to the City and Its Urban Politics of the Inhabitant," *GeoJournal* 58, No. 2 -3 (2002): 102.

[76]Mark Purcell, "Possible Worlds: Henri Lefebvre and The Right To The City," *Journal Of Urban Affairs* 36, No. 1 (2013): 146-50.

kuzingatia mahitaji yao na matamanio yao ya kujenga jamii mpya yenye kuzingatia misingi ya utu, haki, uhuru na usawa.

Nguzo hizi mbili za dhana ya kimapinduzi ya haki-jiji zinapowekwa katika vitendo hujenga jiji jipya, jamii mpya, mfumo mpya wa uzalishaji mali na mfumo mpya wa ufanyaji maamuzi. Umiliki wa pamoja huondoa umiliki binafsi ambao ndio msingi wa unyonyaji. Ushiriki wa pamoja katika maamuzi huondoa maamuzi ya wachache ambayo ndio msingi wa ukandamizaji. Kwa maana hiyo, dola la kibepari na mfumo wa kibepari havina tena nafasi katika jamii mpya.

**Hitimisho: Twende na Mtazamo Upi?**

Sura hii imefafanua kwa kina mitazamo miwili ya haki-jiji, ikianza na mtazamo wa kimageuzi na kumalizia na mtazamo wa kimapinduzi. Kama sehemu ya hitimisho, ni vema kuweka wazi kuwa mtazamo wa kimageuzi wa haki-jiji una mapungufu kadha wa kadha. Mosi, baada ya kupigiwa chapuo asasi zisizo za kiserikali pamoja na mashirika ya kiraia, haki-jiji kama dhana ya kimageuzi ikajikita katika haki za binadamu. Maazimio yote ya kimageuzi kuhusu haki-jiji yameorodhesha utitiri wa haki na kuziita haki-jiji kiasi kwamba inakuwa vigumu kujua nini hasa maana ya haki-jiji na kuitofautisha na haki zingine. Hii inaififisha haki-jiji, kuiondolea umahsusi wake na kuifanya iwe dhana butu inayomaanisha kila kitu.

Pili, utekelezaji wa mtazamo wa kimageuzi wa haki-jiji umewekwa mikononi mwa dola. Kwa maana nyingine, mtazamo huo ni tegemezi kwa dola ilhali dola lenyewe ni chombo kinachotumiwa na tabaka la wavunajasho katika kuendeleza unyonyaji na uporaji wao kwa wavujajasho. Kwa hiyo, badala ya kulidumaza na kulififisha dola, haki-jiji ya kimageuzi inaliimarisha kama chombo cha utekelezaji. Tatu, mtazamo wa kimageuzi wa haki-jiji haulengi kuondoa mfumo uliopo wa umiliki binafsi wa njia kuu za uzalishaji mali. Hii ni kusema kwamba mahusiano ya uzalishaji mali ya kibepari, hasa umiliki binafsi na msisitizo katika thamani mauzo, unaendelea kuwepo hata baada ya mageuzi ya haki-jiji.

Mapungufu hayo yaliyo katika mtazamo wa kimageuzi, yanajibiwa katika mtazamo wa kimapinduzi. Ni mtazamo wa kimapinduzi wa haki-jiji ndio, katika utekelezaji wake, unaweza kuondoa kiini cha masaibu wanayokumbana nayo ambacho ni mfumo wa ubepari.

Hata hivyo, haki-jiji ya kimapinduzi haitafanikishwa kwa siku moja. Itatokana na mapambano ya muda mrefu ya wavujajasho. Mapambano hayo yatapaswa kuhusisha ujenzi wa vuguvugu la kimapinduzi linaloongozwa na wavujajasho katika mapambano yao dhidi ya uporaji, unyonyaji na ukandamizaji unaosababishwa na mfumo wa kibepari.
Wakati mapambano hayo yakiendelea, mabepari na washika dola wanaweza kutishika na hata kulazimika kuruhusu mageuzi kidogo ambayo yataleta unafuu kwa

wavujajasho. Yanapokuwa yametokana na msukumo wa wavujajasho, mageuzi hayo, katika muktadha wa jiji, hutumia dhana ya kimageuzi ya haki-jiji. Mageuzi yanayotokana na msukumo wa wavujajasho ni mageuzi yenye mwelekeo wa kimapinduzi (*revolutionary reforms*) tofauti na mageuzi yanayotokana na hisani ya watawala na mabepari (*reformist reforms*) ambayo huwa ni ya kihafidhina[77].

Mageuzi hayo hupunguza ukatili wa mfumo wa kibepari na kutoa unafuu kwa wavujajasho. Kwa mfano, iwapo kabla ya mageuzi wamachinga walikuwa wakiondolewa kutoka katika majiji basi baada ya mageuzi wataruhusiwa kufanya kazi zao katikati ya jiji. Hebu fikiria, mama mmachinga anaeamka asubuhi na kwenda kupanga karanga zake katika eneo la wazi lililoko jirani na kituo cha daladala apate haki ya kuuza na kurudi nyumbani jioni bila kupigwa na mgambo wala kunyang'anywa bidhaa zake! Bila shaka mama huyo atakuwa ameuona unafuu mkubwa.

Hata hivyo, utekelezaji wa dhana ya kimageuzi ya haki-jiji haupaswi kuwafanya wavujajasho wabweteke na kudhani kuwa mambo yameshakuwa 'murua'. Uzoefu unaonyesha kuwa iwapo wavujajasho hawatajizatiti na kuendelea kupambana ili kubadili mageuzi kuwa mapinduzi basi mabepari hutumia fursa hiyo kuwahadaa na kuwapumbaza ili wadhanie kuwa

[77]Issa G. Shivji, "Seven Theses on Reform and Revolution," *Journal of African Marxists* 4 (1983): 45-53.

mwisho wa safari yao ni mageuzi. Wakati wakiwahadaa wavujajasho, mabepari hutumia kipindi cha mageuzi kujiimarisha zaidi na baadaye huondoa unafuu wote waliokuwa wamelazimishwa kutoa kwa wavujajasho.

Uzoefu wa wafanyakazi huko Ulaya ni mfano tosha. Katika kipindi cha mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20, dira ya tabaka la wafanyakazi ilikuwa ni kuleta mapinduzi yatakayobomoa ubepari na kujenga mfumo mpya wa usawa. Hivyo, walianzisha vyama vya wafanyakazi pamoja na vyama vya siasa vya kijamaa na kuunganisha nguvu kwa pamoja kwa ajili ya kupambana dhidi ya ubepari. Kutokana na mapambano ya vyama vya wafanyakazi na vyama vya kijamaa, ubepari ulijikuta katika tishio la kuangushwa katika nchi za Ulaya. Tayari huko Urusi, Chama cha Kikomunisti kuliangusha utawala wa kaizari na kusimika dola la kijamaa mwaka 1917. Hili lilikuwa tishio kubwa sana kwa mabepari wa Ulaya. Mapebari wakalazimika kufanya mageuzi ambayo yalileta unafuu kwa wafanyakazi: siku ya kazi ikafupishwa, kima cha chini cha mshahara kikaongezeka, wafanyakazi wakapata likizo ya mwaka yenye malipo, likizo ya ugonjwa, likizo ya uzazi, pensheni, malipo ya ziada na uhakika wa ajira. Huduma za kijamii zikatolewa kwa wote bila malipo. Vyama vya wafanyakazi vikaruhusiwa kuingia katika meza ya majadiliano na mabepari kwa ajili ya kuwasilisha madai ya wafanyakazi na pia vyama vya siasa vya wafanyakazi vikaruhusiwa kusimamisha wagombea katika chaguzi na hata kupata viti vya

ubunge na udiwani.

Baadhi ya viongozi wa vyama vya wafanyakazi na vyama vya kijamaa wakajisahau na hata kusema kuwa hakukuwa tena na haja ya kuleta mapinduzi kwa sababu ubepari ulikuwa umefanya mageuzi makubwa ambayo yameimarisha haki na ustawi wa wafanyakazi. Wakafanikiwa kuvifanya vyama hivyo viachane na ajenda ya mapinduzi na kukumbatia ajenda ya mageuzi. Nchini Ujerumani, chama cha *Sozialdemokratische Partei Deutschlands* (SPD) ambacho kilikumbatia ajenda ya mageuzi kilitumia nguvu kubwa kupambana na chama cha kijamaa cha *Kommunistische Partei Deutschlands* (KPD) kilichobaki katika ajenda ya kimapinduzi. Kwa kuwa SPD kilikuwa tayari kimeingia katika ushirika na tabaka la mabepari kikaviona vyama vilivyoamua kubaki katika njia ya mapinduzi (kama KPD) kuwa ndio maadui wakuu na hivyo kushirikiana na mabepari kuzima mapambano ya vyama hivyo na hata kuwauwa viongozi wake kama Rosa Luxemburg[78].

Kwa kuwa tabaka la wafanyakazi katika nchi za Magharibi lilikuwa limeacha mapambano ya kimapinduzi, dola la kibepari halikubomolewa wala umiliki binafsi wa njia kuu za uzalishaji mali haukukomeshwa. Kwa maana hiyo, katika kipindi cha

[78]Sabatho Nyamsenda, "'Only One Thing: Socialism' Rosa Luxemburg's Unlikely Re-emergence in Neoliberal Tanzania," Online Publication No.3/2019 (Berlin: Rosa-Luxemburg Stiftung, 2019). Imepatikana Oktoba 30, 2022 kutoka https://www.rosalux.or.tz/wp-content/uploads/2019/06/3-19_Online-Publ_Socialism-1.pdf

mageuzi, ubepari uliendelea kuimarika huku tabaka la wafanyakazi kilizidi kuhadaika. Baada ya miongo michache ya fungate kati ya tabaka la wafanyakazi na tabaka la mabepari huko Ulaya, tabaka la mabepari likashusha nyundo katika miaka ya 1970 ambapo dola la kibepari, sasa likiwa chini ya wahafidhina, likatumia mabavu yake kuondoa unafuu lililokuwa limeutoa kwa wafanyakazi. Huduma za kijamii zikabidhaishwa, ajira za kudumu zikaondolewa, stahiki za wafanyakazi zikawekwa kapuni, vyama vya wafanyakazi vikadhoofishwa, n.k. Ndio maana katika nchi nyingi sasa, huduma za kijamii ni bidhaa na sehemu kubwa ya wafanyakazi wameajiriwa kama vibarua tu wasio na haki zozote wala nguvu ya maamuzi. Mabadiliko hayo, yanayojulikana kwa jina la mageuzi ya soko huria au uliberali mamboleo, yamekwisha fafanuliwa katika sura ya kwanza. Ni mabadiliko yaliyosababisha dhahma kubwa kwa wavujajasho duniani kote huku yakizalisha neema kwa mabepari.

Kutokana na uzoefu wa vyama vya wafanyakazi uliotolewa hapo juu, tunajifunza kuwa mapambano ya kudai haki-jiji ya kimageuzi yanapaswa kuwa njia tu ya kuelekea kusimika haki-jiji ya kimapinduzi. Yatokeapo mageuzi, wavujajasho wayatumie kujiimarisha badala ya kubweteka na kubaki wakiwashukuru mabepari na washika dola. Wavujajasho watambue kuwa tabaka la mabepari halitoi unafuu kwa wavujajasho kama hisani bali linakuwa limebanwa na mapambano ya wavujajasho kiasi kwamba linabaki na machaguo mawili: ni ama lifanye mageuzi na kutoa unafuu

kwa wavujajasho au lisombwe na kutokomezwa na kimbunga cha mapinduzi ya wavujajasho.

Kinachohitajika kwa mavuguvugu ya wavujajasho mijini ni kupambana kwa mbinu mbili. Kwa upande mmoja, kulilazimisha dola litekeleze haki jiji kama dhana ya kimageuzi na kwa upande wa pili, kuendelea kupambana kuudhoofisha na hata kuubomoa mfumo wa uzalishaji mali wa kibepari pamoja na dola la kibepari. Ikifanyika hivyo, utekelezaji wa dhana ya kimageuzi ya haki-jiji unakuwa ni njia tu ya kuelekea kusimika dhana ya kimapinduzi haki-jiji.

Kwa upande wa Tanzania, madai ya kimageuzi ya haki-jiji yanaweza kujumuisha vipengele vifuatavyo[79]:

(a) Kufutwa kwa amri ya kuwahamisha wamachinga kutoka maeneo ya katikati ya miji nchini kote.

(b) Kulipa fidia kwa wamachinga walioathirika na mazoezi ya timua timua yanayofanywa na halmashauri za miji, manispaa na majiji nchini kote.

(c) Kufanya mageuzi makubwa kwenye sera, sheria za ardhi na mipango miji, pamoja na sheria ndongo ndogo za jiji kwa ajili ya

[79]Sabatho Nyamsenda, "Barua ya Wazi kwa Rais Samia Kuhusu Wamachinga," *Udadisi: Rethinking in Action*, Septemba 27, 2021. Imepatikana kutoka Oktoba 31, 2022 kutoka https://udadisi.com/barua-ya-wazi-kwa-rais-samia-kuhusu-wamachinga/

kuziondolea kiini cha ukoloni, ubaguzi na uonevu dhidi ya sehemu kubwa ya wakazi wa jiji ambao hujipatia kipato kupitia shughuli za umachinga. Katika vitendo, hatua hii inapaswa kujumuisha ubunifu mpya wa ujenzi wa barabara, masoko, vituo vya daladala na mabasi, na mpangilio wa miji unaozingatia matamanio na mahitaji ya walio wengi.

(e) Ushirikishwaji kweli wa wamachinga katika ufanyaji wa maamuzi juu ya mipango miji, bajeti ya jiji, usanifu na ujenzi wa miundombinu pamoja na usimamizi na uendeshaji wa maeneo ya wazi ya umma wanayoyatumia. Ushirikishwaji ni lazima ufanyike kwa uwazi kwa kuwashirikisha wamachinga wenyewe katika eneo lao walilopo na lengo lisiwe kuwahamisha bali kuwapa nafasi wajipange na kujisimamia wenyewe katika eneo walilopo na kutoa maoni kwa serikali juu ya nini cha kuboresha.

Kwa mfano, wamachinga wanaposhirikishwa kikamilifu katika usanifu na ujenzi wa barabara bila shaka wanaweza kutoa maoni juu ya haja ya kuongeza mita mbili kila upande katika barabara kwa ajili ya shughuli zao. Kadhalika, wanaweza kupendekeza kuwa, badala ya kuwatimua wamachinga kutoka katika maeneo yenye msongamano wa watu, serikali inunue baadhi ya majengo katika

maeneo hayo ili kutanua eneo linalotumiwa na wamachinga au kufunga baadhi ya barabara ili mitaa hiyo ibaki kuwa mitaa maalumu ya wamachinga.

Madai ya haki-jiji yaliyoorodheshwa hapo juu yanayapaswa kulindwa na sheria mpya itakayoitwa *Sheria ya Wamachinga*. Je, madai haya yanatekelezeka? Jibu ni ndiyo. Uzoefu wa wamachinga katika nchi za India na Brazil ambao umefafanuliwa hapo juu ni kielelezo tosha. Jambo la msingi kwa wamachinga na wavujajasho wengine wa mijini ni kutambua kuwa utekelezaji wa madai ya kimageuzi ya haki-jiji utatokana na msukumo watakaoutoa kwa washika dola na washika mtaji.

# SURA YA 5

# Uzoefu wa Wamachinga wa India na Afrika Kusini

MICHAELA COLLORD

## Utangulizi

Sura hii ina visa viwili vinavyohusu wavujajasho kuja pamoja na kudai haki zao katika majiji mawili, Ahmedabad huko Gujarat, India, na Durban, Afrika Kusini. Masimulizi yanaelezea jinsi ambavyo, licha ya vikwazo vyote, wafanyakazi hawa wa sekta isiyo rasmi walidai washirikishwe kwenye upangaji wa miji. Walidai njia mpya ya uendeshaji wa miji ambayo

itawapa nafasi ya kushiriki moja kwa moja katika maamuzi ili kukidhi mahitaji yao badala ya wao kuendelea kutengwa.

Kuandika hayo masimulizi, nilitumia vyanzo mbalimbali vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Nilivifupisha kwa Kiswahili ili vitumike kama sehemu ya majadiliano na vikundi mbalimbali vya wavujajasho huko Dar es Salaam, Tanzania. Hii ilitokea wakati wa utafiti kuhusu mapambano ya wavujajasho katika sekta isiyo rasmi jijini Dar es Saaam, nilioufanya kwa kushirikiana na Sabatho Nyamsenda na Christina Mfanga. Utafiti huu unaendelea wakati wa kuandika utangulizi huu.

Lengo la masimulizi haya–na sababu ya kuyachapisha tena hapa–lilikuwa kuangazia mifano ya mapambano ya wavujajasho iliyopata mafanikio na kubadilishana mawazo kuhusu namna ya kupambania mageuzi katika upangaji na uendeshaji wa miji. Masimulizi haya, na vyanzo vyao vya kitaaluma (angalia kwenye tanichini kwa marejeo kamili) yanalenga kuwa na manufaa kwa wavujajasho na vikundi/jumuiya zao, wataalamu wa mipango miji, na marafiki wowote wa wavujajasho katika mapambano ya kudai haki-jiji.

## Wanawake wa Ahmedabad, Gujarat, India[80]

Hii ni simulizi kuhusu wanawake wanaofanya biashara ndogo ndogo mitaani huko Ahmedabad, India. Wanawake hawa walikuwa wanafanya kazi zao katika maeneo ya wazi ambayo hayakuwa yameruhusiwa kutumika. Kwa maana nyingine, walitumia maeneo hayo 'kinyume cha sheria.' Polisi walitumia kigezo cha maeneo kutoruhusiwa kisheria kuwanyang'anya wanawake hao pesa na bidhaa zao.

Lakini akina mama hao walichukua msimamo wa pamoja kudai haki yao ya kufanya kazi karibu na wateja wao. Walitumia uasi wa kiraia dhidi ya sheria ambayo ilikuwa yenyewe dhidi ya maskini. Wanawake hao walifanyaje?

Cha kwanza, walikuwa sehemu ya umoja (Chama cha Wanawake Waliojiajiri) uliojumuisha muungano na pia ushirika. Ushirika ulitoa mikopo kwa wanawake kununua bidhaa kutoka kwa wauzaji wa jumla kwa kiwango cha ushindani. Wakati huo huo, muungano huo uliwasaidia wanawake kudai nafasi halali sokoni.

Wanachama wa umoja wa wanawake walianza kwa maandamano katika mji huo. Manispaa haikuwa na namna zaidi ya kukubali matakwa ya wanawake hao. Manispaa iliruhusu maeneo ya pembezoni mwa

[80]Kisa hiki kimefupishwa kutoka Ela R. Bhatt, *We Are Poor but So Many: The Story of Self-Employed Women in India* (Oxford: Oxford University 2006).

barabara kutumika. Ilichora miraba ya futi nne kwa nne kwenye lami, ya kutosha kwa kila muuzaji na bidhaa zake. Huu ulikuwa ushindi wa awali, lakini nusu tu. Makundi yaliyopinga uwepo wa wafanyabiashara ndogondogo mitaani bado yalikuwa makali, haswa polisi na wauzaji maduka, ambao walichukia ushindani kutoka wanawake wanaofanya biashara ndogo ndogo. Hatimaye, polisi walipata kisingizio cha kuwafukuza wanawake wachuuzi tena.

Hata hivyo, kufukuzwa huku kuliwahamasisha wanawake kuchukua hatua ya pamoja na kushinda ushindi mkubwa zaidi. Kwanza, walijaribu–kupitia muungano wao–kukutana na viongozi wa manispaa, wakiwaomba ruhusa ya kuendelea na nafasi zao mtaani, hiyo miraba iliyochorwa awali. Manispaa ilikataa. Kisha, wachuuzi wakaamua kwa pamoja kurejea tena kwenye maeneo yao, bila ruhusa.

Kitendo kilionekanaje? Wachuuzi walifika mapema asubuhi na wakachukua nafasi zao za kawaida. Wenzao wa muungano, wateja na wachuuzi wa kiume ambao tayari walikuwa na leseni za kufanya biashara zao walisimama karibu na wanawake kuwatetea, na hata kuelekeza magari kuzunguka soko wakati polisi walikataa.

Kwa namna hiyo, wanawake walirudisha maeneo yao. Lakini bado matumizi ya maeneo hayo hayakuwa halali, kwa hivyo muungano wao ulirudi kujadiliana na viongozi wa manispaa. Wakati huu, iliamuliwa kuwa

kadi ya muungano ingetumika kama kitambulisho na kuzingatiwa kama leseni halali ya biashara. Kuanzia wakati huo, wanawake hao walifanya kazi kwa amani kwa zaidi ya miaka miwili, hadi chama kilichokuwa kikiongoza manispaa hiyo kilipoondolewa madarakani.

Lakini huo sio mwisho wa simulizi ya wanawake hao. Mapambano yao yaliendelea. Wanawake wafanyao biashara ndongo ndogo walikabiliwa na vikwazo vingine, lakini pia walijipanga upya na, kwa kuungana na wamachinga wenzao, walipata ushindi mkubwa zaidi, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Wamachinga (2014)[81].

## Wamachinga wa Makutano ya Warwick, Durban, Afrika Kusini[82]

Hii ni hadithi kuhusu mabadiliko yaliyotokea eneo la makutano ya barabara lijulikanalo kama Warwick Junction, lililopo jijini Durban, Afrika Kusini, kuanzia miaka ya 1990. Wamachinga, mama lishe, pamoja na

[81]Ramanath Jha, "Strengthening Urban India's Informal Economy: The Case of Street Vending," *Observer Research Foundation*, ORF Issue Brief No. 249 (July 2018): 1-8; Sachin Kumar na Arbind Singh, "Securing, Leveraging and Sustaining Power for Street Vendors in India," *Global Labour Journal* 9, No. 2 (2018): 135-139.

[82]Kisa hiki kimefupishwa kutoka marejeo yafuatayo: Richard Dobson, Caroline Skinner na Jillian Nicholson, "Working in Warwick: Including Street Traders in Urban Plans" (Durban: School of Development Studies, University of KwaZulu-Natal 2009); Sally Roever na Caroline Skinner, "Street Vendors and Cities," *Environment and Urbanization* 28, No. 2 (2016): 359-374; Caroline Skinner, "Challenging City Imaginaries: Street Traders' Struggles in Warwick Junction," *Agenda* 23, No. 81 (2009): 101-109.

wavujajasho wengine walikuwa wakifanya kazi zao hapo Warwick Junction, ambacho ni kituo muhimu cha usafiri chenye wasafiri (yaani wateja) wengi.

Eneo hilo lilikuwa na sifa mbaya ya msongamano, uchafu, na ukosefu wa usalama wenye kiwango cha juu cha uhalifu. Wamachinga pia walinyanyaswa mara nyingi na polisi. Lakini kuanzia miaka ya 1980, wavujajasho wa Warwick Junction walianza kujipanga kudai mabadiliko, na katika miaka ya 1990, walianzisha uhusiano mpya wa ushirikiano na Halmashauri ya Jiji, uhusiano ambao uliwawezesha kushiriki katika mradi wa kuendeleza eneo hilo, yaani kuboresha mapato yao, maisha na mazingira ya kufanya kazi.

Mchakato ulianza na wavujajasho kuunda vyombo vya kuwaunganisha. Kwa mfano, wanawake waliunda Umoja wa Wanawake Waliojiajiri (SEWA), kama walivyofanya dada zao huko Ahmedabad waliojadiliwa katika hadithi iliyopita.

Baada ya kuanguka kwa utawala wa kikaburu, Halmashauri ya Jiji pia ilikuwa na wazo jipya la kufanya kazi kwa ushirikiano na wavujajasho wa mijini ili—badala ya kuwatesa watu—wafikie matokeo ambayo yangesaidia wavujajasho.

Kwa hiyo, nini kilitokea? Yafuatayo ni maelezo ya mabadiliko katika eneo hilo la Warwick, yote yakitokana na matakwa ya wamachinga na wavujajasho wengine kuhusu upangaji, na ushirikiano

makini na Halmashauri ya Jiji:

(i) Barabara kuu ambayo ina mzunguko mkubwa wa watu ilipangwa upya kwa kuchora miraba inayotenganisha kila eneo la wauzaji, ambayo ilirahisisha msongamano ili idadi ya wateja iongezeke na kuwezesha wamachinga wengi zaidi kukaa katika eneo hilo.

(ii) Wamachinga wengine walipata meza zilizoundwa mahususi, ambazo ziliwasaidia kuhifadhi bidhaa zao, kurahisisha mzunguko zaidi, na kuruhusu ufikiaji wa wafagiaji mitaani.

(iii) Vyoo vipya na vituo vya maji viliwekwa.

(iv) Maeneo ya kando ya barabara yanayotumiwa na wamachinga yaliezekwa kwa paa kwa ajili ya kuwahifadhi wachuuzi na wateja wao.

(v) Maeneo mapya ya kuhifadhia bidhaa yalianzishwa na hivyo kuwaondolea wamachinga haja ya kukesha wakilinda bidhaa zao.

(vi) Baadhi ya wachuuzi walinufaika na vibanda, jambo ambalo liliwapa ujasiri wa kufanya biashara ya bidhaa za thamani ya juu.

(vii) Malezi ya watoto yalipangwa ili kuwasaidia wanawake ambao walipambana kuendelea na biashara zao wakati wako na watoto wao.

(viii) Mama lishe walipata eneo jipya la kupika kwa usalama zaidi, jambo ambalo liliboresha usalama wao na pia mapato yao.

Sio wamachinga na mama lishe pekee waliofaidika. Kwa mfano, kituo kipya kilijengwa ili wakusanyaji wa kadibodi waweze kuuza moja kwa moja kwa halmashauri badala ya kupitia madalali, jambo ambalo liliongeza mapato yao mara mbili zaidi.

Majawabu yote haya yalizingatia mazingira ya eneo husika na yalijadiliwa kupitia vyama vya wavujajasho na kisha kupelekwa kwa mashauriano kamili na Halmashauri ya Jiji.

Kisa hiki kinatuonyesha kuwa wavujajasho wakijipanga, wanaweza kudai na kupata haki zao, ikiwemo haki ya kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuunda upya jiji lao kwa ajili yao na wenzao.

# SURA YA 6

# Kuelekea Ushirika Mpya wa Wavujajasho

CHRISTINA MFANGA

## Utangulizi

Sura zilizopita zimejadili kwa kina ukatili ambao wavujajasho wanapitia katika majiji na nyenzo zinazostawisha na kulinda ukatili huo ndani ya mfumo wa kibepari. Kama ambavyo mfumo wa kibepari ulivyo na nyenzo mbalimbali za kufanikisha ukandamizaji na uporaji, vivyo hivyo kwa wavujajasho wanaopambana dhidi yake. Hivyo basi, sura hii itazungumzia ushirika

kama nyenzo muhimu ya wavujajasho kujilinda dhidi ya ukatili wa ubepari na kujenga mfumo mbadala.

Dhana ya ushirika imefafanuliwa kwa namna mbalimbali. Hata hivyo, maana hii ndiyo imebeba sifa zote kuu:

> *Ushirika ni chama huru cha watu walioungana kwa hiari ili kukidhi mahitaji na matarajio yao ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kupitia biashara inayomilikiwa kwa pamoja na kuendeshwa kidemokrasia[83].*

Maana hii ya ushirika inatuonyesha kuwa nguvu ndogo ya kila mmoja katika kundi lenye maslahi yanayofanana huletwa pamoja ili kutengeneza nguvu kubwa ya kuanzisha mradi wa pamoja utakaotatua changamoto zilizoshindwa kutatuliwa na mtu mmoja mmoja. Hapa tunaona kuwa sifa kuu ya ushirika ni kuwa muunganiko wa watu kwanza kabla ya kuwa na shughuli ya pamoja ya kiuchumi. Kwa maana hiyo, maamuzi yote hufanywa na watu, sio nguvu ya mtaji kwa kuwa lengo la kuanzisha shughuli ya kiuchumi ni kukidhi mahitaji yao na sio kulimbikiza faida[84]. Kubwa zaidi ni kwamba matunda ya biashara hiyo humilikiwa na kudhibitiwa na washirika wenyewe kwa uwazi

[83]ICA (International Co-operative Alliance), "Statement on the Co-operative Identity," 1995. Imepatikana Septemba 8, 2022 kutoka www.ica.coop/coop/principles.html.

[84]C.S. Bajo and B. Roelants, *Capital and the Debt Trap: Learning from Cooperatives in the Global Crisis* (Hampshire: Palgrave Macmillan, 2013), 116-117.

na demokrasia. Lyimo anatukumbushakuwa tofauti ya ushirika na vyombo vingine vya kibiashara ni watumiaji wa ushirika kuwa wanufaika wa mojamoja wa maslahi ya msingi[85]:

> *Ushirika ni vyombo vya kibiashara ambavyo ina maslahi matatu ya msingi yaani umiliki, udhibiti na faida. Ni ushirika pekee ndio huweka maslahi yote matatu mikononi mwa watumiaji moja kwa moja[86].*

Vyombo hivi ni matokeo ya uasi wa mfumo wa uzalishaji unaotukuza wachache kumiliki njia kuu za uchumi, kudhibiti kinachozalishwa na kujilimbikizia faida ilhali wazalishaji ambao ndio wengi wakiporwa jasho lao na kutenganishwa na walichozalisha. Ndio maana wanasayansi ya jamii wanahusianisha uibukaji wa vyombo hivyo na mabadiliko ya kijamii katika nyakati za mapinduzi ya viwanda. Miongoni mwa majaribio ya awali katika ujenzi wa ushirika ni pamoja na lile la Robert Owen, aliyejaribu kuanzisha vijiji vya kijamaa miaka ya 1775 -1849 ili kukidhi mahitaji muhimu ya wafanyakazi wa viwandani ambao mishahara yao haukukidhi mahitaji hayo. Na la pili ni la wafanyakazi 28 wa Rochedale walioanzisha ushirika wa walaji mwaka 1844, ambao sehemu kubwa ya misingi yake

[85]F.F. Lyimo, *Rural Cooperation: In The Cooperative Movement in Tanzania* (Dar es salaam: Mkuki na Nyota Publishers, 2011), 2-3.
[86]Kama hapo juu.

ndiyo inayoongoza ushirika wa leo[87]. Majaribio hayo yote yalikuwa sehemu ya wavujajasho kufikiria jamii waliyoitamani ambayo ni tofauti na jamii tuliyonayo iliyojengwa kwenye misingi ya kinyonyaji. Kutokana na majaribio hayo, tunapata misingi ya uendeshaji wa vyama vya ushirika ambayo ni pamoja na:

(i) Uanachama wa hiari
(ii) Udhibiti wa kidemokrasia wa wanachama
(iii) Ushiriki wa wanachama katika shughuli za kiuchumi
(iv) Uhuru na Kujitegemea
(v) Mafunzo, Elimu na Taarifa
(vi) Ushirikiano baina ya vyama vya ushirika, na
(vii) Kurudisha huduma kwa jamii[88].

Kwa kufuata misingi hii kikamilifu, ushirika unakuwa mfano wa kwanza wa mfumo mpya, unaowawezesha wavujajasho kuona thamani ya nguvukazi yao ndani ya ubepari[89].

Ushirika umegawanyika katika aina tofauti kutokana na vigezo mbalimbali. Kigezo cha kwanza, kinachohusu aina ya shughuli inayofanywa na ushirika, kinatupatia ushirika wa uzalishaji, ushirika wa mauzo, n.k. Kwa

---

[87]V. Satgar, "Cooperative Development and Labour Solidarity: A Neo-Gramscian Perspective on the Global Struggle Against Neoliberalization," *Labour, Capital and Society / Travail, Capital et Société* 40, no. 1/2 (2007): 59-60.

[88]ICA, "Statement on the Co-operative Identity."

[89]Karl Marx, *Capital*, (London: Penguin, 1981), 3: 571.

kutumia kigezo cha pili, kinachohusu aina ya kundi la wanaushirika, tunapata ushirika wa wafanyakazi, n.k. Kwa kutumia kigezo cha tatu, ambacho ni ngazi ya utendaji wa ushirika, tunaweza kutofautisha ngazi tatu za ushirika ambazo ni ngazi ya msingi, chama kikuu au shirikisho[90]. Kwa kuzingatia vigezo viwili vya mwanzo, tunapata aina kuu tano za ushirika zinazotambuliwa na wengi. Nazo ni: ushirika wa wazalishaji, ushirika wa walaji, ushirika wa wafanyakazi, ushirika wa kifedha na ushirika wa huduma za kijamii. Hata hivyo aina zingine ndogondogo zipo katika hizo kuu, kwani vigezo hivyo huingiliana.

## Historia Fupi ya Ushirika Tanzania

Vyama vya ushirika ni taasisi zenye historia ndefu nchini Tanzania. Baadhi ya waandishi wamediriki kusema kuwa ushirika ndio taasisi pekee yenye mchango mkubwa katika maisha ya Watanzania[91]. Kama ilivyo kwa vyombo mbalimbali vya kutetea maslahi ya wanyonge, ushirika uliibuka katika mazingira ya uhitaji kwa makundi ya wanyonge na hasa wakulima ambao ndio waasisi wa vyama hivyo nchini. Uibukaji, uimarikaji na hata uangukaji wa vyama vya ushirika nchini umegawanyika katika vipindi vinne: kipindi cha ukoloni mkongwe, kipindi cha uhuru, kipindi cha ujamaa na kujitegemea na

[90]Lyimo, *Rural Cooperation*, 126.

[91]A.S.T. Mchomvu na wengineo, "Social Security Systems in Tanzania, Phase II: Co-operatives and Social Protection," *Journal of Social Development in Africa,* 17 no. 2 (2002): 29-44.

kipindi cha sera za soko huria.

*Ushirika chini ya Ukoloni Mkongwe*

Uchumi wa kikoloni ulibadilisha mfumo na mahusiano ya uzalishaji na kuwafanya wazawa kuzalisha wasichotumia na kutumia wasichozalisha. Ulikuwa ni aina ya uchumi unaotegemea usafirishaji wa malighafi kutoka nchini kwenda kuhudumia viwanda katika mataifa ya wakoloni na kurudisha bidhaa kutoka katika viwanda hivyo kwa ajili ya kuuzwa hapa nchini. Shughuli zote za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na biashara yenyewe, zilidhibitiwa na wakoloni ambao walipanga majukumu kwa kuzingatia misingi ya ubaguzi wa rangi. Kwa kuzingatia msingi huo wakoloni waliwazuia wazawa kujihusisha na biashara na hata walipotokea wazawa wachache wenye mitaji ya kufanya biashara ndogondogo walidhibitiwa ili waendelee kuwa vibarua wao[92]. Biashara ikabaki kuwa ya Waasia na walowezi wa Kizungu huku wazalishaji wa Kiafrika wakilazimika kuuza mazao yao kupitia madalali hawa. Kama walivyo madalali wengine, madalali wa Kiasia na Kizungu nao waliitumia nafasi hiyo kujinufaisha na kuwanyonya wakulima kupitia njia mbalimbali kama vile upunjaji wa bei ndogo ya mazao, udanganyifu katika vipimo na ubora wa mazao, pamoja na uhodhi wa zao la kahawa uliokuwa ukifanywa na walowezi ili kujihahakikishia vibarua

[92]Lyimo, *Rural Cooperation*, 36.

katika mashamba yao[93].

Kero hizo na zingine ziliwasukuma wazalishaji vijijini kujipanga na kuanzisha vyama vyao vya ushirika ili kuuza mazao yao kwa bei nzuri na kukomesha uhodhi wa madalali na walowezi. Kwa mara ya kwanza, wazawa waliunda chama chao mwaka 1925, kilichoitwa *Kilimanjaro Native Planters Association* (KNPA)[94]. Wazawa walilazimika kupambana kutetea chama chao dhidi ya serikali ya kikoloni ambayo ilikipiga vita ili kulinda walowezi na kudhibiti vibarua[95]. Mapambano hayo yaliwafanya wakoloni kubaini kwamba gharama ya kuendelea kuwazuia ni kubwa zaidi kiutawala, na hivyo wakalazimika kuruhusu vyama ushirika viundwe chini ya udhibiti wa dola. Baada ya kupata ushauri juu ya uendeshaji wa ushirika kutoka India[96], wakoloni walinakili sheria ya kwanza ya vyama vya ushirika kutoka huko na kuifanyia maboresho machache[97].

Hatimaye, *Kilimanjaro Native Cooperative Union* (KNCU) kikawa chama cha kwanza kusajiliwa mwaka 1933

[93]Kama hapo juu.

[94]Kama hapo juu.

[95]J. A. Mwami, "The Experiences of Cooperatives in Agriculture in Tanzania," Presented at the Workshop on "National and International Experiences of Agricultural Cooperatives," Organized by the Joshi-Adhikari Institute of Social Studies, New Delhi, India, from 18th March to 23rd March, 2013.

[96]Ally M. Kimario, *Marketing Cooperatives in Tanzania: Problems and Prospects*, (Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press, 1992).

[97]*Cooperative Societies Ordinance* (Cap. 211).

pamoja na vyama vyake vya msingi 11. KNCU ilitokana na chama cha zamani kilichoitwa *Kilimanjaro Native Planters Association* (KNPA) ambacho kilivunjwa rasmi na serikali ya mkoloni na kusajiliwa upya kama KNCU[98]. Huo ukawa mwanzo wa wakulima wazawa kuunda na kusajili vyama vya ushirika katika maeneo mbalimbali yaliyokuwa yakizalisha mazao ya biashara. Mfano wa vyama hivyo ni Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku Mkoani Songea (*Ngoni-Matengo Tobacco Growers Cooperative Union* - NGOMAT), Chama Kikuu cha Wakulima wa Kahawa Bugufi cha Wilayani Ngara (*Bugufi Coffee Cooperative Society*), vyama vikuu vya wakulima wa kahawa na mpunga RACU[99] na Unyakyusa mkoani Mbeya, na vingine vingi. Tanganyika ilifanikiwa kuwa na ushirika mkubwa barani Afrika katika kipindi cha ukoloni, ulioundwa na wakulima wa pamba huko Kanda ya Ziwa kwa jina la *Victoria Federation of Cooperative Unions* (VFCU) na baadaye ukajulikana kama *Nyanza Cooperative Union*[100]. Vyama hivyo vyote vilikuwa na kazi kuu ya kuuza mazao ya wakulima na kukomesha unyonyanji wa madalali. Sambamba na hilo vilitoa pembejeo kwa wakulima pamoja na huduma za kijamii kwa wanachama na jamii iliyowazunguka. Mfano wa huduma hizo ni shule, maktaba za jamii, vyuo n.k. Hata hivyo ingawa ushirika uliwapatia wakulima ahueni katika maeneo yaliyotajwa, bado ushirika huo huo, kupitia udhibiti

---

[98] Lyimo, *Rural Cooperation*, 36.

[99] RACU ni kifupi cha *Rungwe African Cooperative Union*.

[100] Pius B. Ngeze, *Ushirika Tanzania* (Dar es salaam: Dar es salaam Pulishing House 1975).

wa dola la kikoloni, ulitumika kama njia ya uhakika ya wakoloni kupata malighafi na kukusanya kodi za kinyonyaji kutoka kwa wakulima.

*Miaka ya Mwanzo ya Uhuru*

Hadi Tanganyika inapata uhuru mwaka 1961, ushirika ulikuwa umepiga hatua kubwa sana kwa idadi ya vyama vya ushirika na uwezo wa kiuchumi. Katika miaka ya mwanzo ya uhuru, vyama vya ushirika viliendelea kudhihirisha uwezo wao katika kuongeza uzalishaji. Na serikali ilithamini na kuipa kipaumbele sekta ya ushirika kiasi cha kuanzishia wizara maalumu na kueneza ushirika nchi nzima. Ndani ya miaka mitano ya mwanzo uzalishaji uliongezeka kwa zaidi ya tani 500,000, yaani kutoka tani 145,000 mwaka 1960 hadi kufikia tani 628,833 mwaka 1966[101]. Hata hivyo, kutokana na nchi yetu kurithi uchumi wa kikoloni, mazao ya biashara yaliyozalishwa nchini yaliendelea kuhudumia viwanda vya nje. Na licha ya kupata uhuru bado ziada yote iliyozalishwa na wakulima haikurudi kwao kwani serikali ya uhuru iliendelea kuidhibiti ili kumudu gharama za kuendesha nchi. Hivyo, kama ilivyokuwa serikali ya kikoloni, serikali ya uhuru pia ilifanya marekebisho ya sheria pamoja na kutunga mpya ili kuongeza udhibiti wa ushirika[102].

[101]Kimario, *Marketing Cooperatives in Tanzania.*

[102]Shamshad Naali, "State Control over Cooperative Societies and Agricultural Marketing Boards," in The State And Working People In Tanzania, ed. Issa G. Shivji (Dakar: COSDERIA, 1986).

Kati ya mwaka 1961 hadi 1967, sheria mbalimbali za masuala ya ushirika na kilimo zilitungwa huku za zamani zikifanyiwa marekebisho au kufutwa kabisa. Kati ya hizo zilikuwemo sheria mpya za uuzaji wa mazao ya korosho na kahawa, yaani *The Coffee Industry Act No. 20 of 1961, na The Cashew Nuts (Compulsory Marketing) Act No. 2 of 1962*. Nyingine ni sheria ya udhibiti na uuzaji wa mazao ya kilimo ya mwaka 1962 ambayo ilifuta sheria namba 5 ya udhibiti na uuzaji wa mazao ya kilimo ya mwaka 1949 (*The African Agricultural Products (Control and Marketing) Act No.5 of 1949*). Mwaka 1963 sheria ya vyama vya ushirika (*The Cooperative Act*) ilifanyiwa marekebisho na mwaka uliofuata ilitungwa sheria ya bodi za mazao ya kilimo (*The National Agricultural Products Boards Act, 1964*)[103].

Sheria hizo zote zilimdhibiti mkulima na chombo chake, yaani ushirika. Wakulima walidhibitiwa kuanzia ngazi ya uzalishaji hadi uuzaji kwa njia mbalimbali, zikiwemo: (i) Kupewa maelekezo ya kiasi, aina na ubora wa mazao yanayotakiwa kuzalishwa (ii) Kulazimishwa kuuza mazao yao kwa bodi za mazao zilizoundwa (iii) Kukatwa fedha zao kwa ajili ya ushuru na tozo mbalimbali ambazo hawakuwa na maamuzi nazo[104] (iv) Kulazimishwa kufuata maelekezo ya bodi za mazao. Sheria zilifanya ukiukwaji wa maelekezo hayo kuwa kosa la kifungo cha miezi sita au faini ya kiasi kisichozidi shilingi 6,000/=.

---

[103]Kama hapo juu.

[104]*The Coffee Industry (Collection of Levy) Rules No. 243, of 1965.*

Sheria hizo pia zilidhibiti vyama vya ushirika kwa kupoka mamlaka yao na kuyaweka chini ya bodi ambazo zilikuwa ni mkono wa serikali kupitia Waziri mwenye dhamana ya kilimo, aliyekuwa na mamlaka yafuatayo: (i) kuunda bodi za mazao mbalimbali kwa ajili ya udhibiti na uratibu wa zao husika na maeneo ya uuzaji (ii) kuteua wajumbe wa bodi husika (iii) kutoa maelekezo kwa bodi na maamuzi yeyote ya bodi yangekuwa halali kama yangefuata maelekezo hayo. Kwa lugha rahisi, mamlaka ya bodi kupanga bei pamoja na kukata tozo na kodi mbalimbali yalifanywa chini ya maelekezo ya waziri na kiwango chochote kingekuwa batili ikiwa waziri hajaridhia. Hivyo basi, mamlaka ya vyama vya ushirika kuamua juu ya maslahi ya wanachama wake yalipokwa na waziri wa kilimo kupitia mwamvuli wa bodi za mazao.

Katika kuendeleza azma ya kuongeza udhibiti na kutafuta uhalali wa kufanya hivyo, serikali iliunda tume ya uchunguzi kuhusu ushirika mwaka 1966[105]. Pamoja na mambo mengine tume ilidai kubaini uwepo wa matatizo kadhaa ndani ya vyama vya ushirika, yakiwemo (i) wanachama kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya ushirika (ii) utendaji mbovu (iii) kukosekana kwa demokrasia katika vyama vikuu (iv) rushwa pamoja na (v) vyama kuingiliwa na siasa na udhibiti wa serikali[106]. Serikali

[105]Naali, "State Control."

[106]Sam Maghimbi, "Cooperatives in Tanzania Mainland: Review and Growth," CoopAfrica Working Paper no. 14 (Dar es salaam: ILO, 2010).

ilifumbia macho madai ya Tume kuhusu ushirika kuingiliwa na kudhibitiwa na serikali na badala yake, ikatumia kigezo cha rushwa na matumizi mabaya ya fedha za ushirika kuingilia na kuongeza udhibiti zaidi. Udhibiti wa serikali uliongezeka hadi kwenye usajili na mamlaka ya uendeshaji, ambapo sheria iliyofuata ilimpa mrajisi wa vyama mamlaka ya (i) kukubali au kukataa usajili wa chama (ii) kugawanya, kuunganisha au kuvunja chama (iii) kuwafuta viongozi waliochaguliwa kidemokrasia na kuteua maafisa wa kusimamia ushirika (iv) kudhibiti matumizi ya pesa ikiwemo kuamua kiasi cha malipo ya wateule wake[107]. Mabadiliko hayo yalitanguliwa na uanzishaji wa shirikisho la vyama vya ushirika (*The Cooperative Union of Tanganyika* - CUT), ambalo, pamoja na mambo mengine, lilikuwa na jukumu la kuendelea kueneza ushirika nchini.

*Kipindi cha Ujamaa na Kujitegemea*

Sera ya Ujamaa na Kujitegemea iliyoanzishwa mwaka 1967 iliendelea kuthamini ushirika na kuutambua kama chombo cha kuwamilikisha wanyonge njia kuu za uchumi. Azimio la Arusha liliweka bayana kuwa:

> *Namna pekee ya kujenga na kudumisha ujamaa ni kuthibitisha kuwa njia kuu zote za uchumi wa nchi yetu zinatawaliwa na kumilikiwa na wakulima na wafanyakazi wenyewe kwa kutumia*

[107]*The Cooperative Societies Act No. 27 of 1968.*

*vyombo vya serikali yao na vyama vyao vya ushirika.*

Kwa hiyo, Azimio la Arusha liliutazama ushirika kama njia bora ya kujenga ujamaa pamoja na kuleta ukombozi wa kiuchumi. Miongoni mwa mabadiliko yaliyofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na muundo wa ushirika ambapo vijiji vya ujamaa vilifanywa kuwa vyama vya ushirika vya msingi na kuongezewa majukumu ya uzalishaji, uchakataji na uuzaji. Chama cha TANU kupitia Mwongozo wake wa 1971 kilisisitiza juu ya ushiriki wa wananchi katika maamuzi ya shuguli zao za kiuchumi na kijamii[108]. Hili lilikuwa jambo moja la muhimu sana katika ujenzi wa demokrasia ya kweli nchini licha ya kuwa utekelezaji wake ulikwenda kinyume.

Bila shaka sera ya ujamaa ilikuwa na maono mazuri yaliyodhihirika katika maendeleo makubwa yaliyopatikana nchini kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hata hivyo, baadhi ya mapungufu ya kiutekelezaji yaliiathiri sekta ya ushirika kwa kiwango kikubwa. Ingawa sera ya ujamaa ilisisitiza juu ya demokrasia shirikishi pamoja na uwezo wa wanachi kumiliki na kudhibiti njia kuu za uchumi, serikali haikuviacha vyama vya ushirika kuwa vyombo huru vinavyodhibitiwa kikamilifu na wanachama. Kiuhalisia, jukumu la kuanzisha vyama vya ushirika chini ya shirikisho la

[108]Tanganyika National Union, *Mwongozo wa TANU* (Dar es Salaam: National Printing Co. 1971).

CUT lilibadilisha utaratibu wa vyama vya ushirika kuanzishwa kwa juhudi za watu wenyewe. Utaratibu huo ulizalisha aina nyingine ya vyama vya ushirika vilivyotokana na ushawishi na vivutio kama mikopo, n.k. badala ya utashi wa wakulima wenyewe[109]. Uamuzi wa kuvifanya vijiji vya ujamaa kuchukua nafasi ya vyama vya msingi na kuwa mawakala wa serikali ulizidi kupunguza imani ya wanachama kwa vyama vyao. Uamuzi huo ulitokana na kubadilika kwa mtazamo wa serikali ambayo sasa ilivitazama vyama vya ushirika kama vyombo vya unyonyaji. Kubadilika huko kwa mtazamo kulitokana kwa kiasi kikubwa na hofu iliyojengeka miongoni mwa warasimu dhidi ya vyama vya uuzaji wa mazao vilivyokuwa na nguvu na ushawashi katika jamii. Hatimaye, vyama vya ushirika vikafutwa kabisa mwaka 1976 kwa madai kuwa haviwezi kutumika kutekeleza lengo la kujenga ujamaa. Nafasi ya vyama vya ushirika ilichukuliwa na vyombo vya kirasimu, kama bodi za mazao, ambavyo vilikuwa chini ya warasimu wasiojua madhila ya wakulima. Matokeo yake ni kuwa uzalishaji ulishuka na mafanikio ya awali ya ushirika yakapotea.

Miaka sita baada ya kufuta vyama ya ushirika, serikali iliamua kujisahihisha na kurejesha tena ushirika. Hata hivyo, hakukuwa na marekebisho yeyote makubwa ya kuondoa udhibiti wa serikali kwa vyama vya ushirika. Sheria mpya ya ushirika ililazimisha uanachama vijijini, ikaweka ushirika chini ya mbawa za chama

[109]Naali, "State Control."

tawala na kuongeza kamati za kirasimu katika uendeshaji wa ushirika[110]. Ushirika mpya uliorejeshwa haukuwa na nguvu kama ule wa mwanzo: vyama vipya havikuwa tena na uwezo wa kiuchumi, hamasa ya wanachama ilipotea na jukumu lenyewe la ushirika kuwatetea wanachama halikutekelezeka ipasavyo.

*Zama za Soko Huria*

Ujio wa mageuzi ya soko huria kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1980 uliathiri sekta zote, ikiwa ni pamoja na ushirika ambao ndio ulikuwa unaanza tena kujikongoja. Kutokana na sera hizo serikali ililazimishwa kufanya mageuzi kadhaa. Mojawapo ya mageuzi hayo ni serikali kujiondoa katika uendeshaji wa uchumi na kuiachia sekta binafsi. Kwa mfano, serikali ililazimishwa kujiondoa katika kusimamia kilimo pamoja na kuwapatia wakulima ruzuku na kuyakabidhi majukumu hayo kwa sekta binafsi chini ya soko huria. Pia, serikali ilitakiwa kujiondoa katika kugharamia huduma za kijamii kama afya, elimu, na nyinginezo, ili ziuzwe kama bidhaa katika hilo soko huria. Kwa ufupi, sera za soko huria ziliwaondolewa wakulima ulinzi na ruzuku ya serikali na kuwaongezea gharama za maisha.

Mabadiliko hayo ya kisera na kisheria yalivigeuza vyama vya ushirika kuwa vyombo vya ushindani, vinavyotumikia soko badala ya nyenzo za mshikamano

[110] *The Cooperative societies Act No. 14 of 1982.*

kwa maslahi ya wanachama. Hata baada ya kuviondoa vyama vya ushirika chini ya mbaw*a za chama cha CCM na kuund*a shirikisho jipya (Tanzania Cooperative Federation - TFC)[111] , wanachama walizidi kupokwa umiliki wa vyama vyao. Sio kwenye shirikisho hilo wala vyama vikuu ambako maslahi ya wa wanachama wa ushirika hutetewa. Wakati wanachama wanapambana na bei mbovu za mazao, ucheleweshaji wa malipo, mlima wa tozo na gharama kubwa za pembejeo, vyama vikuu ambavyo vilipaswa kuwatetea ndivyo vimegeuka kuwa mawakala wa unyonyaji huo[112]. Siyo tu kwamba sera za soko huria zimezaa ubinafsi na ufisadi ndani ya vyama vikuu bali pia zimevilazimisha kuwa kampuni za kibiashara zinazojali faida kuliko huduma kwa wanachama wake kama njia pekee ya kusalia katika nyakati hizi.

## Uibukaji wa Ushirika wa Kifedha Mjini

Kihistoria, vyama vya ushirika wa kifedha vinasemekana kuanzia huko Ujerumani vijijini, mwanzoni mwa karne ya 19 kabla ya kusambaa mijini[113]. Nchini Tanzania, wavujajasho wamekuwa na utamaduni wa muda mrefu wa kushirikiana ili kukidhi mahitaji yao ya kifedha. Njia mbalimbali za kijumuiya kama

---

[111] *The Cooperative Societies Act, 1991.*

[112] Christina Mfanga, "Nani Atasikiliza Kilio cha Wakulima wa Kahawa Kagera?" Katika *Wavujajasho dhidi ya Soko Huria: Uzoefu Mapambano na Dira Madala*, toleo la 3, mh. Sabatho Nyamsenda (Dar es salaam: Rosa Luxemburg Stiftung - East Africa, 2021).

[113] Satgar, "Cooperative Development and Labour Solidarity," 60.

upatu, vyama vya kufa na kuzikana, pamoja na vyama vya ushirika wa kifedha zilistawi katika maeneo ya mijini katika kipindi cha ukoloni. Hata hivyo, vyama vya ushirika wa kifedha havikuwa na nguvu ukilinganisha na vile vya mauzo ya mazao. Ushirika rasmi wa kifedha umepata umaarufu zaidi katika zama za soko huria, ambazo ziliweka msisitizo kwenye ubidhaishaji wa kila kitu pamoja na fedha yenyewe. Kwa kuwa haujishughulishi na uzalishaji wa moja kwa moja bali huduma za kuhifadhi na kukopeshana fedha umekuwa na majukumu makubwa mawili: kwa upande mmoja, ushirika wa kifedha umekuwa sehemu muhimu ya kuwakinga wavujajasho dhidi ya madhila ya soko huria na, kwa upande wa pili, umepigia chapuo udalali na ulanguzi wa kifedha pamoja na ubidhaishaji wa kila kitu chini ya mfumo wa soko huria. Wachambuzi wa siasa uchumi wanatueleza kuwa ushirika wa kifedha ulipigiwa chapuo zaidi baada ya Tanzania kulipiga teke Azimio la Arusha na kuamua kufuata masharti yaliyotolewa na taasisi za kifedha duniani yaani Shirika la Kimataifa la Fedha na Benki ya Dunia[114].

Mageuzi ya soko huria yaliifanya sekta ya fedha kuwa huria na kuimarisha soko la fedha[115]. Serikali ikakaribisha wanaoitwa wadau wa maendeleo katika sekta ya fedha, ambao kimsingi waliingiza huduma zote za kifedha sokoni[116]. Miaka ya 2000 ilishuhudia serikali

[114]Mwami, "The Experiences of Cooperatives."

[115]*Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya 2017.*

[116]*Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya 2002.*

ikishirikiana na kampuni pamoja na asasi mbalimbali za kiraia kuratibu uanzishaji wa ushirika wa kifedha nchini. Japokuwa wachumi wa kiliberali mamboleo walinadi hatua hiyo kama njia ya kupunguza umaskini, wavujajasho wengi walijikuta wakizama zaidi katika dhiki kuliko walivyokuwa hapo awali. Gharama kubwa za maisha chini ya soko huria, taasisi za fedha zisizo rafiki kwao na ushirika wa kifedha ulioanzishwa kutumikia soko viliwazidishia wavujajasho umasikini. Mazingira hayo yaliwalazimisha wavujajasho kuunda ushirika mbadala wa kifedha, unaopingana na maadili ya sera za soko huria[117]. Hivyo basi, aina mbalimbali za ushirika wa kifedha mijini zinaendelea kuibuka zikianzishwa na taasisi za kinyonyaji kwa upande mmoja, na wavujajasho wanaopambana kujinasua na unyonyaji huo kwa upande wa pili.

Tukitazama mifumo ya uendeshaji pamoja na ukubwa wa mtaji tunaweza kuvigawanya vyama vya ushirika wa kifedha katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza linaundwa vyama rasmi vya ushirika wa kifedha vyenye mtaji mkubwa, ambavyo vinaendeshwa chini ya sheria ya vyama vya ushirika ya mwaka 2013. Vyama hivi hujulikana kama Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*Saving and Credit Cooperative Societies* - SACCOS). Katika kundi la pili, kuna vyama visivyo rasmi vya kifedha ambavyo huwa na mtaji mdogo na huendeshwa katika ngazi ya jamii. Ndani ya kundi hili, kuna Vikundi vya Kifedha vya Kijamii (*Community*

[117]Shomary, "Vikundi vya Akiba na Mikopo vya Usawa."

*Financial Groups* - CFGs) vyenye mifumo mbalimbali ya uendeshaji kama Benki za Kijamii za Vijiji (*Village Community Bank - VICOBA*) pamoja na Ushirika wa Kuweka Akiba na Kukopa kwa Zamu (*Rotating Savings and Credit Association - ROSCA*). Sera mpya ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2017 ilivitambua vyama hivi kama watoa huduma wa kifedha wasio rasmi.

Tukivitazama kwa miwani ya msukumo wa uanzishwaji wake pamoja na mahusiano yake na taasisi za kinyonyaji, tunaweza kuvigawanya vyama vya ushirika wa kifedha katika makundi mawili: ushirika tegemezi na wa kinyonyaji na ushirika mbadala wa wavujajasho.

*Ushirika Tegemezi na wa Kinyonyaji*

Ushirika huu umeundwa kwa usaidizi wa mawakala wa ubepari kupitia kile kinachoitwa miradi ya kupunguza umasikini. Mashirika mbalimbali ya kibeberu kama Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Wakfu wa Bill na Melinda Gates pamoja na mashirika mengine, yamekuwa yakifadhili miradi ya uanzishaji na uwezeshaji wa vikundi vya akiba na mikopo katika miji mbalimbali nchini. Kwa mfano, vikundi vya VICOBA vilianzia visiwani Zanzibar mwaka 2000 na shirika la *CARE International* na kuenezwa nchi nzima kwa ushirikiano wa mashirika mengine kama *World's Conference of Religion and Peace* (WCRP), *World Wildlife Fund* (WWF), *Frankfurt Zoological Society of Tanzania* (FZS), *World Vision,* n.k. Jijini Dar es Salaam, vikundi hivyo vilianzia wilayani Ilala kwa ushirikiano kati ya

WCRP na taasisi ya kijamii iitwayo UYAKODE. Kwa asilimia kubwa, vikundi vya aina hii huwa tegemezi kwa ufadhili wa mradi husika, ambapo asilimia kubwa hufa baada ya miradi hiyo kufikia ukomo. Mfano hai ni vikundi vilivyoanzishwa na *CARE International* ambavyo vingi vimeshakufa. Mfano wa hivi karibuni ni vikundi vilivyotokana na mradi wa kuhudumia waathirika wa VVU chini ya shirika la Walio katika Mapambano na AIDS Tanzania (WAMATA). WAMATA ilianzisha vikundi hivyo chini ya ufadhili wa USAID. Mradi huo ulipofikia ukomo mwaka 2021, vikundi vingi vilikufa isipokuwa vichache vilivyoendelea na ufadhili chini ya Shirika la Kikatoliki liitwalo PASADA (*Pastoral Activities and Services for People with AIDS Dar es Salaam Archidiocese*).

Vipo pia vikundi vya kinyonyaji ambavyo vimeundwa kwa ushawishi wa asasi za kifedha zisizo za serikali, taasisi ndogo za kifedha (*microfinance institutions*) pamoja na benki. Taasisi kama FINCA (*Foundation for International Community Assistance*), BRAC (*Bangladesh Rural Advancement Committee*) pamoja na benki mbalimbali zimekuwa zikihamasisha wavujajasho wa mijini, na hasa wanawake, kuunda vikundi ili waweze kupata mikopo kwa ajili ya kuinua biashara zao. Ingawa vinaelezwa kama njia ya kuwainua wavujajasho kwa kuwapatia mitaji, vikundi hivyo, kiuhalisia, vinaundwa ili kurahisisha uporaji wa kila 'senti' ya wavujajasho, na hasa wanawake wanaofanya

biashara ndogo ndogo[118]. Baadhi ya taasisi za mikopo midogo (kama FINCA) ziliingia nchini kwa mwavuli wa asasi zisizo za kiserikali zenye lengo kupunguza umaskini lakini kutokana na kuchuma faida nene kutoka kwa wavujajasho zimeweza kujibadili na kuwa benki kamili zinazojiendesha kibiashara huku hali za kiuchumi za 'wanufaika' wao zikiendelea kudorora. Vikundi vya kinyonyaji vilivyoanzishwa na taasisi hizi hufa baada ya kuwapora wanyonge kila kitu, kuwavunjia familia, kuwaachia msongo wa mawazo unaopelekea magonjwa ya akili na wakati mwingine kuwasababishia vifo[119]. Licha ya kusababisha madhila yote hayo kwa wavujajasho, taasisi hizo za mikopo midogo huendelea kukua zikitengeneza vikundi vipya na kutumia umaskini miongoni mwa wavujajasho kuendelea kujinufaisha.

Ushirika unaoanzishwa na taasisi za kibepari bila kujali kuwa ni mashirika ya ufadhili au taasisi za fedha sio vyombo vya ukombozi bali mirija ya unyonyaji. Miradi ya ufadhili hutumika kuficha sura halisi ya mfumo wa kinyonyaji. Kwa mfano, FINCA huwaaminisha wanavikundi walio chini yake kuwa biashara zao hazikui kutokana na wao kutokuwa na ubunifu katika biashara, n.k. Lugha hii huficha unyonyaji na uporaji unaofanywa taasisi za mikopo midogo. Nalo Shirika la *Frankfurt Zoological Society* lijulikanalo kwa kupigia chapuo uporaji kupitia uhifadhi limeamua kuwahadaa

[118]Shomary, "Vikundi vya Akiba na Mikopo vya Usawa."

[119]Kama hapo juu.

wanavijiji wanaoishi jirani na hifadhi ya Serengeti kuwa umaskini huo utaondolewa na jitihada binafsi za kujiwekea akiba kupitia COCOBA[120].

Ushirika wa kinyonyaji hustawisha mfumo wa ubepari kwa kupalilia ubinafsi na ushindani kwani msisitizo wake ni kuweka akiba na kukopeshana kwa ajili ya biashara binafsi za kila mwanachama. Kwa maana hiyo, ushirika wa haina hii haujishughulishi na ukusanyaji rasilimali kwa ajili ya kuanzisha miradi ya pamoja itakayoendeshwa kidemokrasia na kugawanya pato kwa usawa. Badala yake, ushirika huo ni sehemu tu ya kupata mitaji ya shughuli binafsi zitakazoishia kunufaisha taasisi za fedha. Ushirika wa kinyonyaji haupambani na unyonyaji uliomo katika soko huria bali unajitambulisha kama sehemu ya sekta binafsi kwa lengo la kuwahadaa wavujajasho huku ukisaidia wachache kufaulu kuingia katika tabaka la mabepari na wengi kubakia katika lindi la ufukara.

*Ushirika Mbadala wa Wavujajasho*

Vyama mbadala vya ushirika wa kifedha huanzishwa na wavujajasho wenyewe kama sehemu ya kujinusuru dhidi ya ushirika wa kinyonyaji pamoja na taasisi za kifedha. Kupitia kanuni wanazojiwekea wenyewe, wavujajasho huanzisha vikundi mbadala vya ushirika

[120]COCOBA ni kifupi cha *Community Conservation Banks*. Hivi ni vikundi vyenye mfumo wa VICOBA kwa ajili ya wananchi waishio maeneo ya hifadhi kuweka akiba na kukopeshana. Maelezo zaidi yanapatikana katika tovuti yao https://fzs.org/en/projects/tanzania/serengeti-ecosystem/.

na kuviendesha kwa uwazi na demokrasia sanjari na kugawana faida kwa usawa[121]. Vipo vikundi vingi vya akiba na mikopo vinavyoendeshwa katika msingi wa kuondoa utegemezi na kujenga mshikamano baina ya wavujajasho. Jitihada za kuanzisha ushirika huu mbadala zimetokana na uzoefu ambao wavujajasho waliupata katika vikundi vya kinyonyaji ambao waliutumia kuanzisha vikundi mbadala kwa ajili ya kusaidiana na kupambana dhidi ya unyonyaji. Katika kata ya Manzese, Dar es Salaam, baadhi ya wanawake waliokuwa katika vikundi tegemezi vya VICOBA walipata uzoefu katika kuendesha vikundi na kutumia ujuzi huo kuanzisha vikundi mbadala vya akiba na mikopo. Vikundi mbadala hivyo viliungana baadaye na kuunda chama cha ushirika kinachoitwa UWAWAMA (Ushirika wa Wanawake Wavujajasho wa Manzese). Mbali na kukopeshana, chama hiki cha ushirika huendesha miradi ya pamoja na kugawana mapato kwa usawa. Pia, chama hiki huendesha mijadala kuhusu masuala mapana ya kijamii na kujenga mshikamano na makundi mengine ya wavujajasho kwa ajili ya mapambano zaidi. Licha ya jitihada hizi za muhimu, wavujajasho walioanzisha vyama mbadala vya ushirika wanapaswa kuvilinda ili visivamiwe na taasisi za kinyonyaji na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa ajili ya kuvifanya viwe tegemezi.

[121]Shomary, "Vikundi vya Akiba na Mikopo vya Usawa."

## Maono na Misingi ya Ushirika Mpya Mijini

Uanzishaji wa ushirika mbadala wa wavujajasho ni ushahidi tosha kuwa bado lipo tumaini la kujenga ushirika mpya kwa ajili ya wavujajasho kujikomboa kutoka kwenye madhila ya ubepari. Ushirika mpya utatoa majibu ya uhakika juu ya masuala ya msingi kama ukosefu wa njia za uzalishaji kama ardhi na viwanda, ukosefu wa ajira na mitaji ya kuanzishia shughuli zao binafsi, uporaji wa kipato kwa njia mbalimbali, pamoja na ukosefu wa huduma muhimu za kijamii. Katibu wa UWAWAMA, Faria Shomari, anaeleza kwa ufupi maono ya wavujajasho juu ya ushirika mpya:

> *Iwapo tutajipanga vizuri, tunaweza tukautumia mfumo wa akiba na mikopo kufungua benki yetu wenyewe - Benki ya Wanyonge. Benki ya wanyonge haitakuwa na makato wala gharama za kufilisiana, na amana tunazojiwekea tunaweza kuzifanyia uwekezaji mkubwa wenye manufaa kwa walio wengi*[122].

Katika majiji mbalimbali duniani, wavujajasho wanayatafsiri maono ya ushirika mpya kwa vitendo kwa kuanzisha vyama vya ushirika ili kupambana na ukandamizaji wanaopitia kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mifano michache ya misingi na maono ya ushirika mpya, pamoja na utekelezaji wake inajadiliwa hapa chini.

[122]Kama hapo juu, 23.

*Ushirika Mpya na Umiliki wa Pamoja*

Ushirika mpya utaweka msingi wa umiliki wa pamoja wa njia kuu za uchumi. Katika miji ambayo wavujajasho wameporwa kila kitu, njia pekee ya kurejesha nguvu yao ya kiuchumi ni kupitia umiliki wa pamoja wa njia kuu za uzalishaji mali kama ardhi, viwanda, n.k. Kwa njia hiyo, wataweza kumiliki uchumi wao kwa manufaa ya wote na kuulinda ili usifaidishe watu wachache. Ipo mifano kutoka nchi mbalimbali inayoonyesha mafanikio ya jitihada za umiliki wa pamoja kupitia ushirika na vyombo vingine vya wavujajasho. Nchini Uruguay, kwa mfano, wavujajasho wameweza kumiliki ardhi na nyumba kwa pamoja kupitia ushirika wa nyumba chini ya shirikisho lao lijulikanalo kama FUCVAM (*Uruguayan Federation of Mutual Aid Housing Cooperatives*)[123]. Huko India katika mji wa Pune wavujajasho waliweza kuokoa ekari 400 zisiporwe kwa kuweka mashamba yao katika umiliki wa pamoja kupitia kampuni yao wenyewe[124]. Mbali na umiliki wa ardhi, vyama mbalimbali vya wavujajasho pia vinavyomiliki viwanda vidogo na vya kati. Tukitolea mfano wa hapa nchini, kabla ya

[123]B. Nahoum and R. Valles, "Re-Shaping the City by Making Urban Land Accessible: The Case of Housing Cooperatives in Uruguay," katika *Take Back the Land! The Social Function of Land and Housing, Resistances and Alternatives*, mh. Charlotte Mathivet (Paris: Ritimo, 2014), 177.

[124]Y. Cabannes, "Cooperative, Communal and Collective Forms of Land Tenure and Their Contribution to the Social Function of Land and Housing," katika *Take Back the Land! The Social Function of Land and Housing, Resistances and Alternatives*, mh. Charlotte Mathivet (Paris: Ritimo, 2014), 132.

kufilisiwa na walafi, Shirikisho la Vyama vya Ushirika Nyanza lilikuwa likimiliki viwanda vya kuchakata pamba. Nchini India pia kipo chama cha ushirika kilichoanzishwa na Muungano wa Wanawake Waliojiajiri (SEWA) kinachomiliki kiwanda cha nguo. Msingi huu wa umiliki wa pamoja unasaidia kujenga uchumi fungamani kwani, kwa nguvu ya pamoja, wavujajasho wanaweza kufungamanisha uzalishaji mashambani na viwandani. Aina hiyo ya uchumi husaidia kupunguza utegemezi na unyonyaji pamoja na kuongeza usawa kwa ajili ya kuwanufaisha zaidi wavujajasho. Wavujajasho hujihakikishia umiliki wa mali na ulinzi dhidi ya uporaji.

Katika suala la akiba na mikopo, Muungano wa Wanawake Waliojiajiri huko India (SEWA) unamiliki benki ya wanawake waliojiajiri (SEWA Bank) inayowapatia wanachama wao huduma mbalimbali za kifedha. Kwa upande wa Tanzania, mfano wa UWAWAMA umekwishatolewa hapo juu. Mifano hii ni uthibitisho kuwa ushirika wa kifedha usio wa kinyonyaji unawezekana.

Kupitia umiliki wa pamoja, wavujajasho hutengeneza ajira zenye staha. Katika majiji yanayozalisha jeshi kubwa la watu wasio na ajira, ushirika wa wavujajasho husaidia kutoa ajira zenye staha kwa wanachama wake na wanajamii wengine. Imethibitishwa kuwa ushirika ndio taasisi zinazoongoza kwa kuzalisha ajira

mpya, zenye staha na zinazodumu kwa muda mrefu[125]. Tafiti zimeonyesha kuwa hata wakati wa majanga ya kiuchumi, vyama vya ushirika vinaweza kubadili shuguli za kufanya badala ya kupunguza wafanyakazi[126]. Sio tu kwamba ushirika umetoa ajira za moja kwa moja au kupitia masoko ya bidhaa bali pia umetambua na kuzipa thamani shughuli zilizodharauliwa. Kwa kufanya hivyo, ushirika umethamini utu wa wavujajasho wanaofanya shughuli hizo. Mifano mizuri ni vyama vya ushirika vya wakusanya taka huko Pune, India (Solid Waste Collection and Handling - SWaCH) na Belo Horizonte, Brazil (Central Cooperative Solidarity Network of Workers of Recyclable Materials of Minas Gerais - Redesol). Kupitia vyama vyao vya ushirika, wakusanya taka wa miji hiyo wamefanikiwa kupata tenda za kukusanya taka katika manispaa zao na kuboresha maisha yao huku wakitetea maslahi yao dhidi ya kampuni binafsi za kukusanya taka zilizokuwa zikiwanyonya hapo mwanzo. Hata hivyo hatua muhimu zaidi ni vyama hivyo kumiliki viwanda vyao vya kuchakata taka hizo ili kudhibiti mchakato mzima wa ukusanyaji taka, uchakataji wake na uuzaji wa bidhaa zake.

*Ushirika Mpya na Demokrasia Shirikishi*

Ushirika mpya unaoendeshwa kidemokrasia utakuwa ni hatua muhimu kwa wavujajasho kushiriki moja kwa

[125]Bajo and Roelants, *Capital and the Debt Trap*, 108-15.

[126]Kama hapo juu.

moja katika maamuzi ya msingi yanayohusu maisha yao. Hivi sasa, wavujajasho hawanufaiki na demokrasia ya kibepari inayokumbatia uwakilishi kwani maamuzi ya wawakilishi hayazingatii maslahi ya wengi. Kwa mfano, sera na sheria za mipango miji zisizozingatia maslahi ya wavujajasho wa mijini zimetungwa na hao hao waitwao wawakilishi. Katika mazingira hayo ni wazi kwamba ujenzi wa majiji jumuishi yatakayolinda haki za wavujajasho, wakiwemo wamachinga, utafanikiwa tu ikiwa mfumo wa maamuzi utafanyika kwa kuzingatia msingi wa demokrasia shirikishi. Vyama vya ushirika ambavyo tayari vinaendeshwa kwa misingi ya demokrasia shirikishi vina uwezo wa kutoa uzoefu huo wa ndani na kushinikiza ushiriki wa wanachama wake katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwemo katika utungwaji wa sera na sheria za upangaji na uendeshaji wa miji.

Ipo mifano kutoka nchi zingine inayoonyesha mchango wa vyama vya ushirika katika kushinikiza demokrasia shirikishi katika nchi. Shirikisho la ushirika wa nyumba huko Uruguay (FUCVAM) lilifanikiwa kushinikiza mabadiliko ya kisheria yaliyowezesha wavujajasho wa mijini kupata haki za ardhi na makazi[127]. Nchini Brazil, chama cha ushirika cha wakusanya taka (ASMARE), kwa ushirikiano na vyama vya ushirika vingine zaidi ya 22, vimeweza kushiriki katika kutunga sera za usimamizi wa taka katika mji wa Belo Horizonte. Mwaka 2001, vyama hivyo viliendesha semina na

[127]Nahoum and Valles, " Re-Shaping the City."

midahalo kupitia jukwaaa lao vikipinga uamuzi wa kuwapiga marufuku waokota taka maskini uliolenga kuzinufaisha kampuni binafsi za kuzoa taka. Mapambano hayo yaliilazimisha serikali kuziamuru mamlaka za miji kutoa ajira mbadala kwa wahanga wa uporaji huo wa vyanzo vya ajira[128]. Ushindi huu wa wakusanya taka wa Brazil unatukumbusha umuhimu wa umoja na mshikamano kati ya vyama vya ushirika vyenyewe kwa upande mmoja na baina ya vyama vya ushirika na mavuguvugu mengine ya wavujajasho kwa upande mwingine. Mshikamano wa aina hiyo ndio uliolisukuma Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini Afrika Kusini (COSATU) kushinikiza serikali kutambua upekee wa vyama vyama vya ushirika katika utunzi wa sheria na sera mbalimbali na kusaidia uanzishwaji wa vuguvugu la vyama vya ushirika kitaifa[129]. Ushirika huu mpya mijini unaweza kabisa kujenga demokrasia shirikishi nchini Tanzania na kupambania maslashi ya wanyonge wote kupitia mshikamano na vyombo vingine vya wavujajasho.

*Ushirika Mpya na Huduma za Kijamii*

Katika majiji yaliyo mengi, maeneo wanayoishi watu wa tabaka la chini hayana huduma na miundombinu ya msingi kama makazi bora, mifumo ya majitaka,

[128]Sonia Dias, "Intergrating Informal Workers into Selective Waste Collection: The Case of Belo Horizonte, Brazil," WIEGO Policy Brief No 4, 2011. Imepatikana Agosti 15, 2022 kutoka http://www.wiego.org/sites/default/files/publications/files/Dias WIEGO PB4.pdf.

[129]Satgar, "Cooperative Development and Labour Solidarity," 74.

huduma za uhakika, pamoja na bora za maji, nishati, afya, bima na nyinginezo. Kustawi kwa ushirika mpya mjini kutakuwa ni hatua muhimu ya kuwarejeshea wavujajasho huduma zote za msingi walizoporwa ndani ya mfumo wa soko huria.

Kupitia ushirika, wavujajasho kutoka nchi mbalimbali duniani wameonyesha uwezo wa kurejesha na kuweka huduma hizo chini ya udhibiti wao kupitia ushirika. Kwa mfano, ushirika wa nyumba umesaidia kutatua tatizo la makazi katika baadhi ya maeneo nchini Kenya ambapo chama cha NACHU (*The National Housing Cooperative Union*) kimewasaidia watu waishio kwenye makazi holela kupata makazi salama. Nchini Sweden, vijana walioshindwa kuondoka kwa wazazi kwa kutomudu gharama za makazi waliweza kupata huduma hiyo kupitia ushirika wa nyumba. Maelfu ya wakazi katika mji wa Montevideo, Uruguay, wamejipatia makazi salama chini ya shirikisho la ushirika wa nyuma FUCVAM. Yapo maeneo mengine mengi yenye makazi holela ambayo yameboreshwa kupitia ushirika.

Ushirika pia umesaidia kutatua kero za maji na umeme kwa wavujajasho. Jiji la Santa Cruz de la Sierra nchini Bolivia linatambulika kwa kuwa na ushirika mkubwa wa watumia maji duniani unaohudumia maelfu ya wakazi na kutoa huduma bora kuliko majiji mengine[130].

[130]Florence Bétrisey, "The Conditions for the Reproduction of the SAGUAPAC Water Cooperative in the City of Santa Cruz de la Sierra, Bolivia: Discourse Analysis," *Articulo-Journal of Urban Research* 7 (July 2015).

Ipo pia mifano ya ushirika wa huduma za umeme, mawasiliano pamoja na usafiri katika miji mbalimbali duniani. Kote huko wavujajasho wameweza kujiletea huduma hizo pale ambapo hazikuwepo au kukusanya nguvu ya pamoja ya kifedha ili kumudu gharama zake.

Ujamiishaji wa malezi ya watoto ni hatua nyingine kubwa ya kimageuzi iliyopatikana katika baadhi ya maeneo ya mijini kupitia ushirika. Nchini India wanawake wavujajasho chini ya SEWA wameanzisha ushirika wa huduma za malezi na kumiliki vituo vya kulelea watoto vinavyoendeshwa kiushirika[131]. Wapo wanawake wavujajasho wengi katika miji yetu ambao shughuli zao za kujitafutia kipato huwa ngumu au kulazimika kusimama kwa muda ili kulea watoto hasa wanapokuwa katika umri mdogo sana. Na ikiwa wametelekezwa na wenza wao hali huwa mbaya zaidi kiasi cha kulazimika kusukuma mzigo huo kwa wazee wao vijijini ili wao waendelee kujitafutia kipato. Katika mazingira hayo ambayo ubepari umemuongezea mwanamke mzigo, mfumo wa ushirika umewaonyesha wanawake mfano wa jamii mpya ambamo suala la malezi litakuwa la kijamii.

SEWA imeliweka wazo la ujamiishaji wa malezi ya watoto katika vitendo na kuwawezesha wamachinga wanawake kufanya shughuli zao bila hofu ya usalama wa watoto wao wala mzigo wa kuambatana nao katika

[131]International Labour Organization, *Advancing Cooperation Among Women Workers in the Informal Economy : the SEWA Way* (Geneva: ILO 2018), 27-31.

shughuli hizo. Wanachama wa ushirika na wazazi wa watoto wanachangia gharama za uendeshaji wa vituo hivyo, na ziada inayopatikana kutokana na michango hiyo hugawanywa kwa wanachama kwa usawa. Vituo hivyo vinaendeshwa kwa kufuata kanuni za soko huria ambazo sio za kimapinduzi lakini uwepo wake ni hatua kubwa kuelekea mapinduzi kamili ya kulifanya jukumu la malezi kuwa la jamii nzima kama alivyowahi kusema mwanamapinduzi Alexandra Kollontai[132]. Mbali na kujamiisha malezi, ushirika umeonyesha njia mpya ya kuondoa unyonyaji katika kazi za huduma za majumbani (*care work*) kwa kuipa thamani nguvukazi ya wahudumu hao kupitia ushirika. Tofauti na vituo vya kuhudumia watoto (*day care*) vya kibiashara vinavyoanzishwa kwa lengo la kutengeneza faida kwa wamiliki wake, vituo vya SEWA vimekuwa sehemu ya huduma kwa wanawake wahitaji, ajira zenye staha kwa wanachama na manufaa ya kiuchumi kwa wote kupitia gawio la ziada kwa wachangiaji wa huduma hiyo.

Ushirika pia unayo nafasi kubwa katika utunzaji wa maliasili na mazingira. Katika kipindi ambacho miji inakumbwa na majanga yatokanayo na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, wavujajasho wanatumia ushirika kuokoa dunia na kuifanya iendelee kuwa sehemu salama. Msingi wa uzalishaji wa kukidhi mahitaji badala ya ulimbikizaji unaifanya

[132]Alexandra Kollontai, "Communism and the Family," in *Selected Writings of Alexandra Kollontai*, trans. Alix Holt (London: Allison and Busby, 1977).

miradi ya ushirika kuwa mfano wa uzalishaji wenye utunzaji endelevu wa rasilimali kwa ajili ya vizazi vijavyo. Hilo limedhihirishwa na ushirika wa wavuvi kisiwani Natividad, Mexico ambao umefanikiwa kufanya uvuvi unaojali mazingira na kutunza rasilimali za bahari. Wanaushirika wamekuwa wakisimamisha shughuli za uvuvi pale inapobidi ili kufidia uharibifu na kutunza mazalia ya samaki[133]. Vipo pia vyama vya ushirika wa nishati jadidifu, kilimo cha kiikolojia na vinavyochakata tena taka ngumu. Hivyo mbali na kuleta tumaini kiuchumi, kisiasa na kijamii, ushirika wa wavujajasho pia unaheshimu mifumo ya kiikolojia inayomwezesha binadamu kuendelea kuishi.

## Hitimisho

Kama tulivyoona katika sura zilizopita, ujenzi na upanuzi wa majiji unaambatana na tabaka la mabepari kudhibiti mfumo wa maisha ya wavujajasho. Mabepari wanadhibiti nguvu kazi na utamaduni wa wavujajasho na kuwapoka haki zote za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Hata hivyo, wavujajasho wameonyesha uwezo, nguvu na nia ya kupambana dhidi ya unyonyaji na udhibiti huo. Mifano ya ushirika iliyojadiliwa katika sura hii ni ushahidi wa uwezo wa wavujajasho kurejesha umiliki na udhibiti wa nguvu kazi yao na kujenga jamii mpya yenye demokrasia kamili na utamaduni wa usawa. Katika majiji kandamizi yanayopora haki za kiuchumi na huduma za kijamii ili kuneemesha ubepari, ushirika

[133]Bajo and Roelants, *Capital and the Debt Trap*, 130.

unapambana kuzirejesha na kuziweka chini ya udhibiti wa wavujajasho kwa maslahi ya jamii nzima. Kwa ufupi, ushirika unatuonyesha uwezekano wa kuwa na jamii isiyo na unyonyaji wala ukandamizaji.

Ni vema kutambua kwamba ili ushirika ufanye kazi inayokusudiwa kikamilifu ni lazima kuuangusha kabisa ubepari na kusimika mfumo mpya wa kiuchumi ambao utaendana na maadili ya ushirika. Katika hali ya sasa ni lazima ushirika wa wavujajasho upambane kujilinda dhidi ya kupokwa malengo yake ili usigeuzwe kuwa chombo cha kustawisha mfumo kandamizi. Hivi sasa, taasisi mbalimbali za kibeberu zinaujumuisha ushirika katika mipango yake inayolenga kustawisha ubepari. Kwa mfano, Umoja wa Mataifa unautaja ushirika kama chombo cha kuyafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals* - SDGs), ambayo, licha ya kuwa na maneno mazuri, hayajielekezi katika kupindua mfumo wa ubepari. Taasisi za kibeberu za kifedha kama Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa zimekuwa zikijumuisha vyama vya ushirika kama wadau wa maendeleo. Hizo zote ni dalili za wavujajasho kuporwa vyombo vyao vya kimapambano ili waendelee kunyonywa na kukandamizwa. Hivyo basi, wavujajasho wanalo jukumu la kulinda ushirika wao ili usiporwe na kubadilishwa malengo yake ili kuutumikia mfumo wa kibepari. Ili kulilinda tumaini la kujenga jamii mpya kupitia ushirika, wavujajasho wana wajibu wa kujenga na kuimarisha ushirika wao kwa ajili ya ukombozi wao wenyewe.

Kitabu hiki kinachambua mtazamo, sera na sheria zinazotumiwa na serikali ya Tanzania katika kupanga miji na kuwaondoa wamachinga kutoka katika maeneo ya katikati ya jiji. Kinaonyesha kuwa zina asili ya uonevu wa kitabaka ulioanza wakati wa ukoloni na kukomaa katika kipindi cha sera za soko huria.

Kila mara wamachinga wanapodai haki yao ya kujipatia kipato katikati ya jiji huonekana kama mahayawani wanaotoa madai yasiyotekelezeka. Kitabu hiki kinayaweka madai ya wamachinga katika muktadha na kuonyesha kuwa sio madai ya kihayawani bali ni madai halisi na yanayotekelezeka, yaliyojikita katika nadharia ya haki-jiji. Uchambuzi wa sera, sheria na maazimio ya kimataifa juu ya haki-jiji pamoja na utekelezaji wake katika nchi mbalimbali umetolewa. Tanzania haipaswi kubaki nyuma. Kitabu hiki kinaunga mkono vuguvugu la wamachinga katika kudai HAKI-JIJI SASA!

*"Kitabu hiki kimepaza sauti zetu sisi wamachinga tulio katika vita kali ya kupambania haki zetu za kuwa huru kufanya biashara na kujipatia kipato ndani ya jiji."*

**Lulu Juma** (Mmachinga, Dar es Salaam).

*"Kimegusa maisha ya watu wengi sana, hasa akina mama wanaofanya biashara ndogo ndogo kandokando ya barabara... Kinaonyesha umuhimu wa ushirika katika kuleta usawa katika jiji."*

**Faria Shomary** (Katibu, Ushirika wa Wanawake Wavujajasho Manzese - UWAWAMA).

*"Kitabu hiki kinatumia nadharia muhimu ya haki-jiji kuonyesha jinsi gani, kwa kupitia dola kandamizi, mfumo wa matabaka unawezesha kundi dogo la walalaheri likishirikiana na kundi la walalahai kunufaika na uchumi wa jijini huku ukizuia 'ufikikaji' huo wa jijini kwa kundi kubwa la walalahoi... Ni andiko adhimu lipaswalo kusomwa hima na wito wake kuitikiwa pima na kila mpenda haki."*

**Chambi Chachage** (Profesa Msaidizi, Chuo Kikuu cha Howard, Marekani).

Kimechapishwa kwa hisani ya:

ROSA LUXEMBURG STIFTUNG
EAST AFRICA REGIONAL OFFICE

**ISBN: 978-9912-41-234-7**